# Nipashe

Jumamosi Novemba 2, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580065

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Mtatiro aagiza wanafunzi watoro wachapwe viboko mbele ya wazazi

UKURASA 3

# Sarakasi kila kona uchaguzi wa mitaa

• **Ofisi** za watendaji zafungwa, wagombea upinzani wadai kunyimwa fomu, Mbatia alia rafu, ACT Wazalendo yatoa neno... *Endelea uk.2*

Distributed via ippmedia



Rais John Magufuli akizungumza na viongozi wa wizara, mikoa, wilaya na taasisi za serikali zinazohusika na mazao ya korosho na ufuta, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Kibabu mbaroni madai ya nyamapori

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## IGP Sirro amtaka aliyetishia bastola

UKURASA 2


MICHEZO ZAHERA KAIMALIZA YANGA KISAIKOLOJIA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# Magufuli aagiza madeni korosho kulipwa leo

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli, ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango leo kutoa Sh. bilioni 40 kwa ajili ya kulipa madeni ya wakulima wa korosho.

Madeni hayo yalitokana na serikali kununua korosho za wakulima katika msimu wa mwaka 2018/19.

Akizungumza na viongozi wa wizara, mikoa, wilaya na taasisi za serikali zinazohusika na uzalishaji na mauzo ya korosho, ambao pia ulihudhuriwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema ni lazima fedha hizo ziwafikie wakulima wote.

Rais Magufuli aliagiza kuwa watendaji wa mikoa na wilaya hizo kuhakikisha fedha zinawafikia wakulima na si vinginevyo na kwamba wahakikishe wanaolipwa ni wanaostahili kupata malipo hayo.

Aidha, alieleza kutoridhishwa na utendaji kazi wa Wizara ya Kilimo, viongozi wa mikoa na wilaya ambao kwenye maeneo yao kumetokea wizi mkubwa wa fedha za wakulima kupitia vyama vya msingi vya ushirika (Amcos).

Rais alisema wizi huo umesababisha wakulima wengi kuishi maisha duni, huku akisikitishwa na viongozi hao kutochukua hatua dhidi ya walioibia wakulima.

Alisema wizi huo ulibainika baada ya kumtuma Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Brigedia Jenerali John Mbungo, na kwamba muda mfupi alibaini wizi wa Sh. bilioni 1.23.

Kwa mujibu wa Rais Magufuli, kati ya fedha hizo Sh. milioni 375 za Mkoa wa Lindi zimerejeshwa. Aliwataka viongozi hao kubadilika na kuhakikisha haki za wakulima zinalindwa ipasavyo kwa kurejesha fedha zilizoibwa na kuzuia mianya yote ya wizi.

"Nataka mfanye kazi, hakuna mtu wa kuwanyanyasa, nendeni mkashughulikie kero za wakulima, mna vyombo vya ulinzi na usalama nendeni mkavisimamie, kinyume na hapo nitakuona hutoshi kwenye nafasi hiyo," alisema.

Kuhusu mnada wa korosho, alitaka uwepo utaratibu wa kufungua mnada kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni na kufungua masanduku yenye zabuni kwa uwazi mara baada ya saa 10 jioni kuheshimiwe, ili kuepusha njama za upangaji wa bei.

# Sarakasi kila kona uchaguzi wa mitaa

**Na Waandishi wetu**

SARAKASI zimetawala kwenye uchukuaji na urejeshaji wa fomu za wagombea wa nafasi za wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji nchini huku baadhi ya wagombea wakidai kufanyiwa fitina.

Mchakato wa uchukuaji na urejeshaji fomu umedaiwa kusababisha baadhi ya wagombea kunyimwa fomu, ofisi za watendaji wa mitaa kufungwa, hujuma na fujo mbalimbali ambazo zimekuwa kikwazo kwa wagombea kutekeleza wajibu wao wa kikatiba.

Takribani kwenye maeneo yote ambako jambo hilo linaendelea, kumekuwa na sarakasi ambazo zina lengo la kuhujumu baadhi ya wagombea na uchaguzi kwa ujumla huku waathirika wakiomba serikali kuingilia kati watendaji ambao kwa makusudi wanakwamisha utekelezaji.

**MBATIA ALIA RAFU**

Katika jimbo la Vunjo, Mbunge wa jimbo hilo, James Mbatia (NCCR-Mageuzi), alisema vituo vingi vya kuchukua na kurejesha fomu havijafunguliwa hatua ambayo imesababisha wagombea wa chama hicho kunyimwa kuchukua fomu.

Alisema baadhi ya wasimamizi wanawatishia wagombea kwamba hata wakishinda hawatatangazwa na sehemu zingine wananyimwa nakala za fomu ambazo ni kwa mujibu wa mwongozo wa uchaguzi huo.

Akizungumza na Nipashe jana kuhusu madai ya kuwapo kwa hujuma, Mbatia alisema amemwandikia barua Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Tukosa Nyavanga, kuomba ufafanuzi wa mwongozo wa kanuni ya 17 (1)-(15) na kanuni ya 18-(1)-(4) pamoja na mwongozo 11:4

Mbatia ambaye pia ni Mwenyekiti wa NCCR Mageuzi Taifa, alisema hali si ya kuridhisha kwa kuwa chama hicho kinaamini katika itikadi ya utu na kwamba hawako tayari kuona amani iliyopo inaharibiwa.

Barua ya Mbatia iliyoandikwa na kutiwa saini na Katibu wa Jimbo la Vunjo, Mathew Temu, ilisema: "Ndugu msimamizi wa uchaguzi, suala hili bado linadhihirisha shaka na sintofahamu kutokana na mkanganyiko unaoendelea

**INAENDELEA UK. 8**



Makamu wa Rais, Samia Hassan, akisalimiana na Rais wa Zambia, Edgar Lungu, walipokutana katika hafla ya kuapishwa Rais Mpya wa Botswana, Dk. Mokgweetsi E. K. Masisi, iliyofanyika, jijini Gaborone, Botswana jana. **PICHA: OMR**

# Sirro amtaka aliyetishia bastola kujisalimisha

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, amemtaka kijana aliyeonekana kwenye video fupi akimtishia kumuua kwa bastola dereva mmoja, ajisalimishe polisi pamoja na silaha yake.

Video hiyo ilisambaa jana kwenye mitandao ya kijamii, ilimwonyesha kijana aliyekuwa na gari ndogo aina ya Toyota Altezza lenye rangi ya bluu, akibishana na dereva mwenzake wa lori na baadaye kumtishia kwa bastola.

Dereva wa lori alisikika kwenye video hiyo akimwambia huyo aliyetoa silaha kuwa: "Wewe umesema utatoa bunduki, toa hiyo bastola na wewe utakufa, huna lolote, mwache aniuwe."

Wakati akitamka maneno hayo, alishuka kwenye lori na kwenda mbele ya gari huku dereva wa Altezza alifungua mlango wa gari lake na kutoka na bastola huku akimtamkia mwenzake (dereva wa lori) kuwa atamuua.

Mabishano hayo wakati yakiendelea, dereva wa Altezza alimwelekezea mwenzake na kumwambia kuwa atampasua kichwa na kumtaka akae chini kitendo ambacho dereva aliyekuwa akitishiwa alikikaidi.

Akitolea ufafanuzi kuhusu tukio hilo mbele ya waandishi wa habari muda mfupi baada ya uzinduzi wa kampeni ya Utatu yenye lengo la kukomesha rushwa barabarani, IGP Sirro alisema wametoa silaha kwa masharti maalum.

"Silaha tumewapa kwa masharti maalum, hatukuwapa kwa ajili ya kuwatishia Watanzania, tukibaini umewatishia Watanzania kama alivyofanya yule kijana, hatujui ugomvi ulikuwa ni nini.

"Lakini je, kama yale yaliyoelezwa, je alikuwa na sababu ya kutoa silaha kumtishia wenzake, kimsingi mtu unapopewa silaha hakikisha unafuata masharti, usipofuata masharti la kwanza tutakunyanganya silaha.

"La pili tutakupeleka mahakamani na la tatu tutamuomba Mungu atusaidie, tukufunge ili ukirudi nyumbani kwa mke wako au mume wako uwe na adabu ya kutunza silaha."

Alisema ameagiza kijana huyo akamatwe lakini amekuwa akipiga chenja hivyo amemtaka ajisalimishe mwenyewe polisi na kwamba afikishwe mahakamani.

Awali, Msemaji wa jeshi hilo nchini, David Misime, aliliambia Nipashe kuwa uchunguzi wa tukio la kijana huyo umeanza kufanyika.

Aidha, alifafanua taratibu za kisheria za umiliki wa silaha kuwa ni kumpa mtu kibali cha kumiliki silaha na akawa nayo ili alinde maisha yake na mali zake.

"Mmiliki wa silaha atatumia silaha anayomiliki pale tu anapoona maisha yake yako hatarini au mali yake na si kuitumia kutishia watu au kuionyesha onyesha ili wajue kwamba ana miliki silaha au kwa ajili ya sifa," alisema.

Kamanda Missime alisema kitendo kama hicho kinachoonekana kama ndiyo uhalisia wenyewe na hakuna nia ovu wakati wa kuandaa picha hiyo na kuisambaza ni kinyume na masharti ya kumiliki silaha.

## HABARI KITAIFA



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala, wilayani Kibaha mkoani Pwani, jana. Bandari hiyo, itakuwa na uwezo wa kupokea kontena 3,000 kwa wakati mmoja kutoka Bandari ya Dar es Salaam, na kupunguza adha ya msongamano wa magari. **PICHA: MARY GEOFREY**

# Babu matatani madai ya uwindaji haramu

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WATU 10 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa makosa mbalimbali akiwemo mzee wa miaka 65 ambaye alikamatwa na wenzake wawili kwa tuhuma za uwindaji haramu wa wanyamapori baada ya kukutwa na vipande tisa vya nyama ya nyati.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, wakati akizungumza na waandishi wa habari jana, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Zephania Furahisha (65), Alfred Mwanogile (42) na Zakayo Jackson (30) wote wakazi wa Kijiji cha Bintimanyanga wilayani Chunya.

Alisema watuhumiwa hao wa uwindaji haramu walikamatwa Oktoba 30 saa 6:30 mchana wakiwa na nyama hiyo ambayo inasadikika kuwa waliwinda bila kuwa na kibali.

"Watuhumiwa walikamatwa wakati wa oparesheni iliyowashirikisha Askari Polisi na Askari wa Wanyamapori (KDU) kutoka mkoani Iringa na hawa ni wawindaji haramu maana hawana vibali vinavyowaruhusu kuwinda," alisema.

Katika hatua nyingine, Jeshi hilo linawashikilia watu sita kwa tuhuma za kukutwa wakitengeneza na kuuza pombe haramu aina ya gongo kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Kamanda Matei aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Ambokile Mwaisabila (38), Isaya Christopher (28) na Zaina Kasim (26) wote wakazi wa Kijiji cha Kibisi wilayani Rungwe ambao walikamatwa na lita 12 za gongo.

Alisema watuhumiwa hao ni watengenezaji, wauzaji na wanywaji wa pombe hiyo haramu na kwamba walikamatwa Oktoba 30, mwaka huu, majira ya saa 4:00 asubuhi.

Matei aliwataja wengine kuwa ni Tunu Kijumile (21) mkazi wa Kijiji cha Itete Halmashauri ya Busokelo wilayani Rungwe ambaye alikutwa na lita tatu za pombe hiyo, Damin Mpinga (71) mkazi wa Igwa wilayani Mbarali ambaye alikutwa na lita 10.

Mwingine aliyenaswa na gongo ni Mariam Sipo (42) mkazi wa Matundasi wilayani Chunya ambaye alikamatwa na lita tisa za gongo akiwa ameihifadhi kwenye madumu.

Tukio la mwisho ni la mtu mmoja ajulikanaye kwa jina la Abrahamu Nason (27) mkazi wa Mji wa Kasumulu wilayani Kyela kunaswa na dawa za kulevya aina ya bangi yenye uzito wa kilogramu 23 akiwa ameihifadhi nyumbani kwake.

Kamanda Matei alisema mtuhumiwa alikamatwa kufuatia operesheni iliyofanyika katika mji huo na kwamba mtuhumiwa alikuwa ameihifadhi bangi hiyo kwenye mifuko miwili ya sandarusi.

Distributed via ippmedia

# DC aagiza wanafunzi watoro kuchapwa mbele ya wazazi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MKUU wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, Julius Mtatiro (pichani), amemwamuru mmoja wa walimu wa Shule ya Sekondari Ligoma kuwaadhibu wanafunzi watatu ambao ni watoro sugu kwa kuchapwa viboko vinne kwa kila mmoja kutokana na kutoonekana kwenye shuleni kwa muda mrefu.



Akizungumza na Nipashe jana, Mtatiro alisema kwa sasa wilaya yake bado inaendelea na kampeni ya kupambana na utoro sugu, nidhamu kwa wanafunzi na mimba za utotoni, hivyo amelazimika kuwaelekeza walimu kuona umuhimu wa kuwaadhibu wanafunzi sugu kwa utoro mbele ya wazazi wao na amezionya pande zote zinazohusika na uzembe kama huo.

Katika kampeni hiyo, aliwataka wazazi wa wanafunzi ambao ni watoro sugu na watoto wao wafanye wajisalimishe kwenye shule za msingi na sekondari na wakikaidi hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

Alisema katika kutekeleza agizo hilo, maofisa wote, watendaji wa kata, waratibu elimu kata na walimu wote wa shule za sekondari wametakiwa kuendelea kutoa adhabu kwa wanafunzi wao ambao wanabainika watoro na kuona umuhimu wa kuwaonya wazazi wa wanafunzi ambao wameshindwa kuwasimamia watoto wao na kuacha wakifanya vibarua badala ya kwenda shuleni.

Akiwa katika Shule ya Sekondari ya Ligoma, tarafa ya Namasakata, Mtatiro aliwaonya wazazi wa wanafunzi ambao ni watoro sugu kuwa hatua zinazoendelea kuchukuliwa wilayani humo ni kali dhidi yao. Alisema hata wazazi wakishindwa kuwadhiti watoto wao dhidi ya utoro, watachukuliwa hatua kali ikiwamo kuwapeleka mahakamani.

"Rais Magufuli na serikali yake ametenga Sh. billion 23.6 kila mwezi ili watoto msome bure. Ninyi na wazazi wenu mnachekeana na kupuuza masomo na kusababisha taifa kupoteza fedha nyingi. Hii haikubaliki hata kidogo," alisema.

Aidha, Mtatiro aliwaeleza maofisa wote wanaosimamia elimu na utawala katika ngazi za vijiji, kata na tarafa kuendelea na msako mkali kuhakikisha watoto wote wanaendelea na masomo na kuwachukulia hatua kali wazazi watakaoonyesha kukaidi agizo hilo.




# Ndalichako aonya maofisa elimu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, amewaonya maofisa elimu wa mikoa wanaomdanganya Rais kuwa wamemaliza tatizo la upungufu wa madarasa.

Kutokana na udanganyifu huo, amesema maofisa hao wanaongeza idadi ya wanafunzi katika shule za zamani na kusababisha wanafunzi hao kufanya vibaya katika matokeo ya mtihani wa mwisho.

Prof. Ndalichako alitoa onyo hilo jana alipofanya ukaguzi wa ukarabati wa Shule ya Sekondari ya Kilimo ya Kilosa mkoani Morogoro ambayo inakarabatiwa kwa Sh. 752,094,254 ambazo ni kutoka serikali kuu.

Alisema vitendo hivyo vinavyofanywa na maofisa elimu hao pia vinachangia walimu wa shule hizo kushindwa kufundisha kwa ufanisi na matokeo yake wanafunzi kushindwa kufanya vizuri katika masomo yao, huku shule zikitupiwa lawama kwa matokeo mabovu.

Alisema ameamua kutoa onyo hilo katika kipindi hiki ambacho matokeo ya mtihani wa darasa la saba yameshatoka na hivi sasa maofisa hao wako katika hatua ya kuwapangia shule wanafunzi wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza mwakani.

Waziri Ndalichako alisema kitendo cha kumdanganya Rais kuwa hakuna tatizo la madarasa wakati upungufu upo, hakitavumiliwa na atakayebainika atachukuliwa hatua kali.

Alisema Rais John Magufuli amekuwa akifanya jitihada nyingi za kukusanya kodi na kama kuna upungufu wa madarasa ana uwezo mkubwa wa kumaliza tatizo hilo kwa kuwa amedhamiria kutoa elimu bure.

Akizungumzia kuhusu fedha zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo, alipongeza kwa ukarabati huo na kuwa ya mfano katika shule zote zilizopewa baada kutumia Sh. 602,094,254 hadi kukamilika kati ya Sh. 752,094,254 walizopewa na kubakiwa na Sh. 150,000,000.

Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoy, alisema mafanikio ya ukarabati huo yanatokana na ofisi yake kusimamia kwa karibu zaidi ili kuhakikisha fedha hizo zinatumika vizuri na kuleta tija katika elimu.

Awali, Mkuu wa Shule hiyo, Mbaraka Kupela, alishukuru serikali kwa kuipatia fedha shule hiyo kwa ajili ya ukarabati ambao kwa sasa umefikia asilimia 75.

# Mahakama yaamuru Jamhuri kutoa kadi za washtakiwa

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi, jijini Dar es Salaam imeagiza upande wa Jamhuri kushughulikia kadi za benki zinazopitishiwa mishahara ya washtakiwa katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi wa uthamijishaji wa madini ya Almasi na Vito Tanzania (Tansort), Archard Kalugendo, na mwenzake ili familia zipate mahitaji muhimu.

Amri hiyo ilitolewa jana Hakimu Mkazi Mkuu Huruma Shaidi baada ya washtakiwa kuilalamikia mahakama kwamba mpaka sasa hawajarejeshewa kadi zao zinazopitishiwa mishahara na kwamba familia zinateseka.

Wakili wa Serikali, Deisy Makakala, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika na kuomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Kwa nyakati tofauti, washtakiwa waliomba mahakama kuagiza upande wa Jamhuri kuwarejeshea kadi hizo kwa ajili ya kutoa fedha za matumizi ya familia zao.

Hakimu alimtaka Wakili Makakala kufuatilia suala hilo kwa kushirikiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon ili familia za washtakiwa zipate mahitaji yao.

Wakili wa utetezi, Egbert Millanzi, aliiomba mahakama kuuagiza upande wa Jamhuri kuharakisha upelelezi wa kesi hiyo. Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa tena Novemba 15, mwaka huu itakapotajwa na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Mbali na Kalugendo, mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Mthamini wa Madini ya Almasi wa Serikali, Edward Rweyemamu.

Kalugendo na Rweyema ambao ni Watumishi kutoka Wizara ya Madini, kwa mara ya kwanza walifikishwa mahakamani hapo, Septemba 15, 2017 wakikabiliwa na shtaka la kuisababishia serikali hasara ya Sh.bilioni 2.4.

Katika hati ya mashtaka, washitakiwa hao wanadaiwa kutenda kosa hilo Agosti 25 na 31, 2017 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Shinyanga.

Kwa pamoja wakiwa wathaminishaji wa almasi wa serikali na waajiriwa wa Wizara ya Nishati na Madini, waliisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 1,118,291.43 ambazo ni sawa na Sh.bilioni 2.4.



Wafanyabiashara wa bidhaa zilizotumika wakiwa wamezitandaza kwenye sehemu kubwa ya barabara katika makutano ya Mtaa wa Nyamwezi na Kipata, Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo kinachosababisha usumbufu mkubwa kwa magari na wakazi wa eneo hilo. **PICHA: JOHN BADI**

# DC ataka uchunguzi gharama za ujenzi stendi ya daladala

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Morogoro, Regina Chonjo, ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ( Takukuru) katika wilaya hiyo kuchunguza na kupitia upya gharama za ujenzi wa stendi ya mabasi madogo (daladala) ya Manispaa ya Morogoro ambazo ni Sh. bilioni 5.2.

Pia amemwagiza Mkurugenzi wa Manispaa, wahandisi na Wakala wa Barabara za Mijini na vijijini (Tarura) wilaya kuchambua na kupitia upya gharama za ujenzi wa stendi hiyo ili kujiridhisha kama fedha hizo zinaendana na ukubwa wa mradi na kuona namna ya kuongeza maeneo zaidi ikiwamo ujenzi wa maduka tofauti na ilivyo sasa.

Chonjo alisema hayo jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Manispaa ya Morogoro, alipokaribishwa kuhudhuria kikao cha kawaida cha baraza hilo kilichofanyika katika ukumbi wa manispaa.

Alisema hayo baada ya hivi karibuni kufanya ziara kukagua miradi mbalimbali ukiwemo wa ujenzi wa stendi ya daladala inayojengwa eneo la Mafiga na kutoridhishwa na kasi ya mkandarasi na kutia shaka juu ya gharama za ujenzi huo.

" Namtaka Mkurugenzi wa Manispaa kuangalia upya mikataba ya ujenzi wa stendi hii ili kuhakikisha inaendana na hali halisi na kupitia upya gharama za ujenzi ambazo ni Sh. bilioni 5.2 ili kujiridhisha kama fedha hiyo inaendana na ukubwa wa mradi," alisema Chonjo.

Aliisema kwa mujibu wa mtaalamu mshauri wa mradi, Antonio Mpinga, kutoka kampuni ya Howard Humphrey, ujenzi wa stendi hiyo utagharimu Sh bilioni 5.2.

Chonjo alisema kwa mujibu wa mshauri wa mradi huo, kati ya fedha hizo jengo la utawala litagharimu zaidi ya Sh. milioni 450, stoo ya kubebea matangi ya maji Sh. milioni 49 na ujenzi matundu 18 ya vyoo ni Sh. milioni 256 na fedha inayosalia, Sh. Bilioni nne ni

INAENDELEA UK. 8



Wanafunzi wakipita jirani na takataka zilizotelekezwa bila ya kuzolewa kwenye sehemu ya waenda kwa miguu katika Barabara ya Kigogo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kigogo Takukuru amwandikia DPP kuomba yaishe

Distributed via ippmedia

**Na Hellen Mwango**

MCHUNGUZI Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Cosmas Batanyika (44) anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kushawishi rushwa ya zaidi ya Sh. milioni 300, kupokea na kutakatisha Dola za Marekani 20,000 amedai mahakamani amemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya kukiri makosa yake.

Batanyika alitoa madai hayo jana kesi yake ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kevini Mhina, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali, Glory Mwenda, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi haujakamilika.

Hata hivyo, mshtakiwa alidai kuwa amemwandikia barua DPP na kwenye makubaliano anasubiri majibu ndugu zake wanafuatilia.

Hakimu Mhina alisema kesi hiyo itatajwa tena Novemba 15, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu

Mapema mahakamani hapo upande wa Jamhuri, ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu Paul Kadushi, ulidai kuwa katika shtaka la kwanza kwamba Februari 9, mwaka huu, eneo la Upanga, mshtakiwa akiwa mwajiriwa na Takukuru katika nafasi ya Mchunguzi Mkuu, aliomba rushwa ya Sh. milioni 200 kutoka kwa Hussein Gulamal Hasham kwa lengo la kuharibu ushahidi wa tuhuma za kukwepa kodi zilizokuwa chini ya uchunguzi wa mwajiri wake.

Shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Februari 10, mwaka huu katika Viwanja vya Maonyesho ya Biashara, Sabasaba jijini Dar es Salaam, alijipatia Dola za Marekani 20,000 kutoka kwa Faizal Hasham kama kishawishi cha kuharibu ushahidi wa tuhuma za kukwepa kodi dhidi ya Hussein Gulamal Hasham.

Kadushi aliendelea kudai kuwa katika shtaka la tatu, Februari 13, mwaka huu, katika ofisi za Makao Makuu ya Takukuru, mshtakiwa akiwa mwajiriwa na Mchunguzi Mkuu wa Takukuru,

**INAENDELEA UK. 8**

# Mizigo yaongezeka bandari ya Lindi

**Na Mary Geofrey,** LINDI

TANI 856 za mizigo zimehudumiwa katika Bandari ya Lindi, katika kipindi cha miezi mitatu kulinganisha na tani 635 zilizohudumiwa kwa mwaka 2018.

Ongezeko hilo limetokana na ukarabati wa gati, uliofanywa na Mamlaka ya Bandari (TPA) kwa gharama ya Sh. bilioni 3.5.

Akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, Ofisa wa Bandari hiyo, Erick Nyagali, alisema kasi ya mizigo inayopita katika bandari hiyo inatarajiwa kuendelea kuongezeka.

"Hadi kufika mwaka wa fedha 2019/20 hali itakuwa nzuri na tani za mizigo zitaongezeka na kuvuka lengo tulilojiwekea kwa sababu bandari yetu imekuwa ya kisasa," alisema Nyagali.

Alitaja miongoni mwa mizigo inayopita katika bandari hiyo kuingia katika mkoa huo ni vyombo, vifaa vya umeme vikiwamo majokofu, pasi, majiko ya umeme, vyombo vya usafiri kama baiskeli ambavyo vinatokea Zanzibar.

Alisema mizigo mingine inayopitishwa katika bandari hiyo kuelekea Zanzibar ni mwani na mazao mengine ya chakula.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja Bandari ya Mtwara, Abdihal Salim, alisema ukarabati wa gati hilo ulikamilika Machi, mwaka huu.

Alisema mradi huo ulihusisha ujenzi wa makaravati, ukarabati wa boladi za kufungia meli, ujenzi wa kuta ya bahari pamoja na uongezaji wa kina cha bahari gatini ambao ulitekelezwa na Mkandarasi wa Kampuni ya Comfix and Engineering.

"Ukarabati ulihusisha ubadilishaji wa paa,uwekaji wa mageti mapya, ubomoaji wa ujenzi wa kuta dhaifu, uwekaji wa sakafu na ukarabati wa ofisi ya ofisa wa bandari. Kwa sasa pia mradi uko katika kipindi cha uangalizi tangu ukaguzi wa mwisho ulipofanyika Oktoba 25, mwaka jana na kukamilika Oktoba, mwaka huu," alisema Nyagali.


Alisema mkakati iliyojiwekea TPA ni kuwa gati za kisasa zinazopokea meli kubwa na ndogo kwa ajili ya kuboresha uchumi na mapato ya bandari pindi huduma zake zinapokua zinatolewa.

Alisema bandari ya Lindi inatumika kwa ajili ya kusafirisha bidhaa mbalimbali za mazao na aina nyingine.

Mbali na bandari hiyo, alisema bandari ya Kilwa Masoko, ilifanyiwa ukarabati wa gha a lililotumika kuhifadhia mizigo ya wateja lililogharimu Sh. milioni 81.2.

Alisema ukarabati wa ghala hilo ulianza Mei 10 na kukamilika Septemba 10 mwaka jana na ukarabati ulihusisha ubadilishaji wa paa, ubomoaji na ujenzi wa kuta dhaifu, uwekaji wa sakafu na ukarabati wa ofisi.

Alisema kwa sasa mradi upo katika kipindi cha uangalizi na ukaguzi wa mwisho uliofanyika Oktoba 25 mwaka huu na utakamilika Oktoba 2019.



PIN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA

APPLICATION
CIVIL/~~APPEAL~~/CASE NO. 44 OF 2019
ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION ~~PLAINTIFF~~/APPELLANT
VERSUS
HAPPINESS H. KILEWO & OTHERS ~~DEFENDANT~~/RESPONDENT

NOTICE OF ~~HEARING~~/ MENTION

TO: BENSON LYIMO
ARUSHA - TANZANIA


TAKE NOTICE that the above case has been fixed for mention in the Resident Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the ... day of ...11... 2019 at 8:30 am O'clock in the forenoon.

You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

TAKE FURTHER NOTICE that in default of your appearance on that day time ~~before~~ mention ~~or hearing~~ the Court may proceed in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this ... day of ...11... 2019

RESIDENT MAGISTRATE
ARUSHA



PIN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA
AT ARUSHA

APPLICATION
CIVIL/~~APPEAL~~/CASE NO. 44 OF 2019
ZANZIBAR INSURANCE CORPORATION ~~PLAINTIFF~~/APPELLANT
VERSUS
HAPPINESS H. KILEWO & OTHERS ~~DEFENDANT~~/RESPONDENT

NOTICE OF HEARING/ MENTION

TO ROBERT SIMON URASA
ARUSHA - TANZANIA

TAKE NOTICE that the above case has been fixed for mention in the Resident Magistrate's Court of Arusha at Arusha on the ... day of ...11... 2019 at 8:30 am O'clock in the forenoon.

You may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

TAKE FURTHER NOTICE that in default of your appearance on that day time ~~before~~ mention ~~or hearing~~ the Court may proceed in your absence.

Given under my hand and the seal of the court this ... day of ...11... 2019

RESIDENT MAGISTRATE
ARUSHA

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga inaweza wachezaji wakiandaliwa kisaikolojia

**KESHO** wawakilishi wa Tanzania katika michuano ya kimataifa, Klabu ya Yanga watashuka dimbani nchini Misri kucheza mechi yao ya mchujo ya marudiano dhidi ya wenyeji, Pyramids FC kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga ambayo iliangukia kucheza mechi hiyo ya mchujo baada ya kutolewa na Zesco ya Zambia kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika, katika mchezo huo inahitaji ushindi kuanzia mabao 2-0 ili kuweza kufuzu hatua ya makundi kufuatia mechi ya awali Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza kukubali kipigo cha mabao 2-1.

Tayari wawakilishi hao wa Tanzania waliobaki katika michuano ya kimataifa baada ya Simba, Azam, KMC, KMKM na Malindi kutolewa, wapo nchini Misri tangu alfajiri ya jana, hivyo macho na dua zote za Watanzania tunaamini zitakuwa zikielekezwa kwao ili kuweza kusonga mbele.

Yanga ambayo ilitua nchini Misri alfajiri ya jana, licha ya kupoteza mechi ya kwanza inaweza kupindua matokeo na kusonga mbele pamoja na wengi kuamini kwamba Waarabu hao tayari wamemaliza mchezo baada ya kushinda dakika 90 za awali hapa nchini.

Tunasema inawezekana hasa kutokana na rekodi nzuri ya Yanga ya kutokata tamaa ikiwa ugenini kufuatia kuichapa Township Rollers ya Botswana bao 1-0 ikiwa ni baada ya sare ya 1-1 hapa nchini kwenye mechi ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Lakini pia raundi ya kwanza ya michuano hiyo ikatoka sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa jijini kabla ya kwenda kutolewa kwa tabu na Zesco kwa mabao 2-1, jambo ambalo tunaamini inaweza kufanya makubwa zaidi na kuwashangaza wote wanaoibeza kwa kuona imekwenda kukamilisha ratiba tu kabla ya kurejea kuendelea na Ligi Kuu Bara.

Ingawa wengi wamekatishwa tamaa na kauli ya awali ya Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera aliyoitoa baada ya Yanga kukubali kipigo cha mabao 2-1 jijini Mwanza dhidi ya Waarabu hao, akieleza kuwa hakuna mchezaji hata mmoja kwenye kikosi chake anayeweza kufananishwa na ubora wa wachezaji wa Pyramids.

Huku pia akienda mbali zaidi kwa kueleza kwamba hakusajili kwa ajili ya michuano hiyo ya kimataifa na kwamba usajili wao ulikuwa maalum kwa michuano ya ndani hususan Ligi Kuu, bado hiyo haiwezi kuwa sababu kwetu kuitoa Yanga mapema kabla ya dakika 90 kukamilika.

Tunatambua Zahera inawezekana alitoa kauli hiyo kutokana na presha kubwa aliyoipata kutoka kwa mashabiki uwanjani hapo waliokuwa wakitamani kuona Yanga ikiibuka na ushindi, lakini pia kitendo cha kurushiwa chupa za maji baada ya matokeo hayo huenda kilichangia na kumpandisha hasira kocha huyo.

Hivyo, ushindi ama kupoteza kwa Yanga kutategemeana zaidi na namna Zahera na uongozi wa klabu hiyo ulivyoweza kuwaandaa wachezaji wa Yanga kisaikolojia kwa kuwaeleza waipuuze kauli hiyo ya kocha kwa kuwa ilitokana na hasira iliyochangiwa na presha kutoka kwa mashabiki.

Nipashe tunatambua itakuwa ni jambo gumu kuwarejesha wachezaji mchezoni, hususan kuwaaminisha kwamba wao ni wa kiwango cha juu na wanaweza kupambana na wapizani wao, lakini tunaamini hao ni kama askari vitani na wanajua ni lazima waamini katika ushindi.


Lakini pia wachezaji hawana budi kuipuza kauli hiyo hasa kwa kutanguliza maslahi yao mbele zaidi na kuonyesha kiwango cha juu kwani kwa kufanya hivyo kutasaidia kutangaza soko lao na kupata klabu kubwa nje ya Tanzania kwa kuwa michuano hiyo ni ya pili kwa ukubwa na utajiri barani Afrika baada ya ile ya Ligi ya Mabingwa, hivyo ni dhahiri kuna mawakala wengi kutoka ndani ya bara hili wanaoifuatilia.

Pamoja na hayo yote, Nipashe tukiwa kama wadau namba moja wa soka hapa nchini, lengo letu ni kuona Yanga ikisonga mbele ili Tanzania iendelee kuwa na nafasi kubwa ya kuvuna pointi na kuweza kuingiza timu nne katika michuano hiyo msimu ujao na hilo linawezekana kutokana na maandalizi mazuri iliyoyafanya, hivyo hatuna budi kuwatakia kila la kheri wawakilishi wetu hao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Yanga kuna'ni msimu huu?

Na Barnabas Maro

**"MTOTO** akililia wembe mpe." Maana yake mtoto auliliapo wembe, mpe; ukimkata atauogopa.

Methali hii hupigiwa mfano mtu anayeng'ang'ania kufanya jambo ambalo laweza kumdhuru. Ni heri kumwacha afanye atakalo ili ajifunze kutokana na matatizo atakayopata.

Pia "Mtoto mkaidi mngoje siku ya ngoma." Maana yake mtoto asiyesikia aambiwalo huishia kuzinduka apatapo matatizo.

Hutumiwa kumpigia mfano mtu mwenye tabia ya ukaidi na ubishi ambaye aghalabu huishia kufikwa na maafa na dhiki. Yapo mambo mengi yanayonipa wasiwasi kuhusu kocha wa Yanga, Mwinyi Zahera, raia wa DR Congo. Mwanzoni, kocha huyu alikuwa kipenzi cha wanachama na mashabiki (watu wenye mapenzi na hamasa kubwa juu ya jambo au kitu fulani) wa Yanga.

Aliingia mkataba na Yanga wakati timu hiyo ikiwa imedhoofika (kitendo cha jambo au hali kupungua nguvu au uwezo wake) kwa hali na mali.

Haikuwa na wachezaji wazuri wa kulinganishwa na Simba; haikuwa na fedha za kusajili wachezaji wazuri na waliokuwapo hawakumaliziwa fedha zao za usajili. Hata mishahara yao ililipwa kwa mafungu, tena kwa mbinde!

Ni kipindi alichoingia kocha Mwinyi Zahera kuifundisha timu ya Yanga. Alichukua timu ya wachezaji waliokata tamaa kutokana na ugumu wa kuendesha maisha yao.

Zahera akaingia kwenye uchangishaji fedha ili kuwanusuru wachezaji waliokata tamaa na matumaini kuendelea kuichezea timu ya Yanga! Kuna wakati alitoa fedha zake na hata kuchangisha fedha kwa wanachama na mashabiki ili kuwanusuru wachezaji.

Alipendwa na kusifiwa kila kona kwa jinsi alivyoijenga timu ya Yanga kiasi cha kuwa tishio kwa Simba iliyokuwa ikitetea ubingwa wake kwa msimu wa pili mfululizo.

Taratibu hali ya hewa ikabadilika pale Yanga ilipofungwa kwa mara ya kwanza msimu huo. M-babe wake ni timu ya Ruvu Shootinga ya Pwani.

Wahenga walisema "Hakuna mume wa waume" wakiwa na maana hakuna mtu anayeweza kuwashinda wanaume wenzake wote. Ni methali ya kutumiwa dhidi ya mtu anayejitia ubabe au anayejidai kuwa na nguvu kama njia ya kumnyamazisha.

Wanachama na mashabiki wa Yanga wasiokuwa na hekima/busara watadhani mimi niko upande mwingine. Nilijiunga na Yanga Desemba 2, mwaka 1966 kwa kadi namba 447. Kadi yangu ya nne yenye namba 007887 ambayo ndiyo inayotumika mpaka sasa niliipata Februari 7, mwaka 2008.

Imebidi nieleze yote hayo ili kuwanyamazisha wenye shaka (hali ya mtu kuwa na wasiwasi juu ya jambo) na mimi, hasa wasiotaka Yanga ikosolewe!

Msimamo wangu ni kwamba "Kweli ndio fimbo ya kukamata." Maana yake kweli ni silaha nzuri maishani. Hii ni methali ya kutukumbusha umuhimu wa kusema kweli hata kama kufanya hivyo tutaishia kuchukiwa na wenzetu.

Mwinyi Zahera alionekana kuwa 'mkombozi' wa Yanga. Wahenga walikuwa sahihi waliposema "Ngoma ya wana haikeshi." Kwamba ngoma inayochezwa na watoto au vijana haikawii kuvunjika kutokana na kutoelewana au kutokuwapo kiongozi wa kuwachezesha.

Methali hii hutumiwa na wazee kupigia mfano jambo la kitoto lililoishia kuharibika kwa kutokuwapo ushauri au kupuuzwa mashauri yanayofaa.

Pengine kuna waliosahau jinsi Mwinyi Zahera alivyopendwa hata kuwa kama 'Mwenyekiti Msaidizi' wa Yanga. Alikuwa kila kitu pale Yanga ingawa viongozi halisi waliochaguliwa na wanachama walikuwapo! Mwinyi Zahera alikuwa msemaji wa Yanga. Alichangisha fedha ndani na nje ya Dar es Salaam kwa ajili ya wachezaji. Alisaidia kutoa hela zake kuwasafirisha wachezaji nje ya nchi wakati klabu iliposhindwa kukamilisha fedha za nauli.

Aliwanunulia chakula wachezaji na kuwapa hela waliofanya vizuri uwanjani. Alikuwa baba mlezi wa wachezaji.

Kabla ya ligi ya msimu huu kuanza, alitoa mapendekezo yake kwa viongozi kuhusu wachezaji anaowataka. Aliwataja kwa majina na timu wanazochezea. Viongozi wa sasa wakamtimizia kila alichotaka na kumwachia ashindwe mwenyewe. Magazeti yetu ya michezo nayo yakawa mstari wa mbele kuichafua Yanga! Kwa vipi? Kila mchezaji aliyesajiliwa alisifiwa kupita kiasi. Kwamba mchezaji huyu akitua Yanga, timu zingine zitakwisha! Ikawa ni kazi ya kumsifu kila mchezaji aliyesajiliwa kuwa ni "moto wa kuotea mbali."

Je, ni kweli? Nionavyo, wachezaji hao ni "moto wa kuotea karibu sana" ndio upate joto lake kwani "Kula uhondo kwataka matendo." Ikiwa mtu anatamani kula vitamu lazima awe na matendo au afanye kazi kwa bidii.

Twanasihiwa tufanye kazi kwa bidii na juhudi ikiwa twataka mafanikio. Hamna jambo zuri linalojileta; sharti tuwe tayari kufanya kazi kwa bidii na maarifa.

Wachezaji wote waliotakiwa na kocha Zahera wamepatikana na kusajiliwa kwa mbwembwe. Bado hatujaona umahiri wao uwanjani! Wengi wao hawana tofauti na wachezaji wetu na baadhi yao wamepitwa kwa mbali na wachezaji wetu!

## Kiwanda kuchakata nyama kuanza mwakani

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Ukanda Maalum wa Uwekezaji (EPZA), imesema uzalishaji katika kiwanda kikubwa cha kuchakata nyama cha TanChoice kitakachokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,000 na mbuzi na kondoo 4,500 kwa siku unaanza rasmi mwanzoni mwa mwaka kesho.

Kiwanda hicho kilichojengwa kwa thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 23 na ambacho kitatoa ajira za moja kwa moja kwa watu zaidi ya 500, kilipata leseni ya ujenzi na uendelezaji katika maeneo maalum ya uwekezaji kutoka mamlaka ya EPZA mwaka jana.

Mkurugenzi Uwekezaji na Uwezeshaji wa EPZA, James Maziku, alisema kiwanda hicho ambacho kitakuwa na migawanyo mitano ya machinjio inakifanya kuwa kiwanda kikubwa cha nyama Afrika Mashariki na cha pili kwa ukubwa baada ya kile cha Ethiopia ambacho kina uwezo wa kuchinja ng'ombe 3,000, mbuzi pamoja na kondoo 6,000 na kuzalisha tani 300 za nyama kwa siku moja.

Pamoja na kuwa na asilimia 11 ya mifugo yote barani Afrika, mchango wa sekta ya mifugo kwa pato la taifa bado umekuwa mdogo (asilimia 7.4), wakati sekta hiyo inakuwa kwa wastani wa asilimia 2.6 kwa mwaka.

"Kiwanda hiki cha kuchinja na kuchakata nyama kitapunguza kwa kiasi utoroshaji wa mifugo kwenda nchi jirani ambao wamekuwa wakitumia fursa hii kuongeza uzalishaji kwenye viwanda vyao na mauzo nje ya nchi," alisema.

Takwimu kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaonyesha kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na ng'ombe zaidi ya milioni 13.5, kondoo milioni 5.5, mbuzi milioni 3.6, nguruwe 400,000 na kuku milioni 23.2.

Uwekezaji huo wa kiwanda cha kuchinja na kuchakata nyama unatarajiwa kuingizia nchi fedha za kigeni kwa kuuza nyama nchi za Ulaya na Uarabuni.

"Mradi huo unatekelezwa karibu na inapopita treni ya umeme ya SGR hivyo kukifaidisha kiwanda na wepesi wa kufikisha mizigo bandarini na pia kuleta ng'ombe kutoka sehemu mbalimbali nchini," alisema.

Alisema kiwanda cha TanChoice kitaweza kutengeneza biashara kubwa kwa vijana inayohusisha unenepeshaji wa mifugo ambayo itahitajika kama malighafi kwenye kiwanda cha nyama. Alisema mabaki yatakayotokana na kuchinja na uchakataji wa nyama yatauzwa ndani ya nchi na sehemu nyingine zitauzwa China ambako soko lake ni kubwa.

Pia mabaki kama damu ya mifugo inatumika katika kutengeneza chakula cha kuku na kuongeza fursa kwa wazalishaji wengine wa vyakula vya mifugo. Kwato na pembe za ng'ombe hutumika kutengeneza vifungo vya nguo na mabegi.

# Meya achukizwa wamama kupigiwa miluzi sokoni

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

NAIBU Meya wa Manispaa ya Shinyanga, John Kisandu, ameelezea kuchukizwa na kitendo cha udhalilishaji ambacho hufanyiwa wanawake sokoni kwa kutolewa lugha chafu za matusi na kupigiwa miluzi.

Kisandu alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha Madiwani wa Manispaa ya Shinyanga, viongozi wa masoko, maofisa maendeleo na ustawi wa jamii, kilichoandaliwa na Shirika la Agape la kutetea haki za wanawake, wasichana na watoto, kilichokuwa na lengo la kujadili namna ya kutokomeza ukatili sokoni.

Alisema huwa hapendi kuona wanawake wakidhalilishwa kwenye masoko na wanaume, ikiwamo kuzomewa, kutolewa lugha chafu za matusi ya nguoni na kupigiwa miluzi, hasa wanapokuwa wamevaa mavazi ya mitego. Badala yake alisema wanapokuwa katika hali hiyo, wanapaswa kuitwa na uongozi wa soko husika na kuonywa kuvaa nguo za aina hiyo.

"Mimi ni mmoja wa mashuhuda wa wanawake kufanyiwa ukatili kwenye masoko. Siku moja nilikuwa napita kwenye moja ya masoko ya hapa Shinyanga mjini, nilishuhudia mwanake mmoja akipigiwa yowe na vijana, wakimzomea na kumpigia miluzi kutokana na mavazi aliyovaa hadi nikajisikia vibaya," alisema Kisandu.

"Nawaomba madiwani, viongozi wa masoko, maofisa maendeleo na ustawi wa jamii, tupange mikakati sasa namna ya kutokomeza ukatili kwenye masoko dhidi ya wanawake na wasichana, pamoja na kutunga sheria ndogo na kuzipitisha kwenye baraza, ili watu ambao wanaendekeza ukatili wachukuliwe hatua kwa mujibu wa sheria," aliongeza. Naye Mratibu wa Dawati la Kuzuia Ukatili kwenye Masoko ya Manispaa ya Shinyanga Angel Mwaipopo, alisema ukatili kwa sasa umepungua na kuwaomba madiwani watunge haraka sheria ndogo na kuzipitisha, ili zitumike kuzuia ukatili dhidi ya wanawake na wasichana.



Mfanyabiashara wa nafaka akiondoa vumbi na taka kwenye maharage, wakati akisubiri wateja, katika Soko la Tandale, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Uchakachuaji mafuta wapungua kiwango kikubwa

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

UCHAKACHUAJI wa mafuta ya petroli na dizeli umepungua kutoka asilimia 78 kwa mwaka 2007 hadi asilimia nne mwaka huu, imeelezwa.

Hatua hiyo inatokana na programu ya kuweka vinasaba kwenye mafuta inayofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura).

Aidha, Sh. bilioni 121.6 zimeokolewa tangu mwaka wa fedha wa 2012/13 kutokana na uanzishwaji wa mfumo wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja.

Hayo yalisemwa jana jijini hapa na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Zinyangwa Mchany, wakati akizungumza katika semina ya waandishi wa habari.

Alisema mwaka 2010, Ewura ilianzisha programu ya kuweka vinasaba kwenye mafuta yanayotumika nchini ili kudhibiti uchakachuaji na ukwepaji wa kodi ikiwamo kuweka mazingira ya ushindani na haki.

"Uchakachuaji wa mafuta ni changamoto kubwa nchini na Ewura kwa kuliona hilo, imepambana na kupunguza uchakachuaji kutoka asilimia 78 mwaka 2007 hadi asilimia nne mwaka huu," alisema.

Mchany alisema kutokana na hatua hiyo, mwaka 2010 Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam (UDSM) kilifanya utafiti kuhusu matumizi ya vinasaba na kubaini kuwa mwaka 2010 hadi 2013 kulikuwa na ongezeko la mapato ya serikali (kodi) kwa Sh. bilioni 466.50 manufaa ambayo yanaendelea kupatikana.

kuhusu fedha zilizookolewa, Mchany alisema Ewura kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Nishati (wakati huo), iliandaa mfumo wa uagizaji wa pamoja wa mafuta (BPS) kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na UDSM Aprili 2014, ulibaini kuokolewa kwa Sh. bilioni 121.6.

Pia alisema utafiti ulibaini kupungua kwa gharama za usafirishaji na 'premium' kiasi cha Sh. bilioni 81.9 katika kipindi cha miaka miwili.

"Mbali na hayo, utafiti huo ulibaini kupungua kwa gharama za uhifadhi bandarini kwa Sh. bilioni 25.7, kupungua kwa kuotea kwa mafuta bandarini kwa Sh. bilioni 14 baada ya kubadilisha taratibu za uagizaji mafuta.

Aliweka bayana faida iliyopatikana kwa kutumia mfumo wa pamoja wa BPS kuwa ni kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi za ujazo wa mafuta yanayoingizwa nchini.

"Pia umerahisisha ukokotoaji wa bei za mafuta kwa mtindo uliowazi zaidi na kurahisisha udhibiti wa ubora wa mafuta yanayoingizwa nchini kwa mfumo huo,"alisema.

Naye Mkuu wa Mawasiliano na Uhusiano, Titus Kaguo, alisema uchakachuaji wa kuchanganya mafuta ya taa na dizeli umekwisha kwa sasa.

"Uchakachuaji uliopo ni wa mafuta yaliyolipiwa kodi kwa matumizi ya ndani na yale ambayo hayajalipiwa kodi ambayo yanasafirishwa nje ya nchi,"alisema.

## DC ataka uchunguzi gharama za ujenzi stendi ya daladala

INATOKA UK. 4

kwa ajili ya kujenga eneo la maegesho ya daladala 150.

Mkuu wa wilaya alieleza na kusikitishwa na ukubwa wa gharama hizo na kuwataka madiwani hao watambue kuwa fedha hizo ni za mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB) na zitatakiwa kurejeshwa, hivyo wawe wazalendo kwa nchi yao na makandarasi wawe wanaandika gharama zinazoendana na ukweli.

Alishangazwa pia kuona mchakato wote wa mradi huo umepitia katika kamati ya fedha ya halmashauri na Baraza la Madiwani kuridhia na gharama hizo za ujenzi wa stendi ya daladala hiyo.

Kutokana na hali hiyo, aliwataka madiwani kuweka wazi mikataba wanayoingia na makandarasi pamoja na maeneo wanayochukua kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ili kutoleta utata wakati wa ukusanyaji mapato.

Pamoja na hayo, alishangazwa na uamuzi wa Manispaa wa kuacha kutekeleza agizo lililotolewa na serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kwamba miradi yote ya kimkakati itumie 'force account' lakini wameamua kutumia makandarasi kutoka nje.

Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Sheila Lukuba, aliahidi kuchukua hatua na kushughulikia suala hilo ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kulingana na upatikanaji wa fedha.

# Sarakasi kila kona uchaguzi wa mitaa

INATOKA UK. 2

kujitokeza kwenye ofisi yako kwani umekuwa ukitoa maelekezo kwa njia ya simu ambayo leo yameenda kinyume cha majibu ya barua yako ya mwongozo.

"Kutokana na changamoto zinazoendelea hatuna imani na hila za makusudi za kuzuia fomu katika ofisi yako kinyume cha utaratibu, hivyo tuna shaka kuharibiwa fomu au kuchezewa kimaandishi fomu hizo, hivyo kupoteza haki ya mgombea."

Alisema kutokana na utata huo kwa matamko ya msimamizi msaidizi, wagombea wao kuwa hawatakuwa na sifa za kugombea unazidi kutia shaka kwa kuwa wamekosa fomu ya tamko kikanuni namba (16 e) pamoja na matishio ya matamko ya kuwa baadhi ya wanachama wetu hawatateuliwa.

Malalamiko mengine ni pamoja na vituo vya kupokea fomu za wagombea havifunguliwi kwa muda ulioainishwa kwenye kanuni na hiyo ni kwa asilimia 70 na kwamba hadi jana, vituo vyote vilifungwa jimbo zima.

Aidha, Mbatia amemwandikia barua yenye kumbukumbu namba NCCR/HIM/VOL.36/19 ya Novemba mosi, mwaka huu, Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Moshi kumwarifu kuhusu viashiria vya uvunjifu wa amani katika Jimbo la Vunjo.

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Tukosa Nyavanga, alisema hajapokea barua ya Mbatia na hajasikia lolote kuhusiana na malalamiko yanayotolewa.

### DAR WANYIMWA FOMU

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kinamlalamikia Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi jimbo la Kibamba, Lightness Shirima, kwa kumnyima fomu mgombea wa Chadema nafasi ya uwenyekiti.

Taarifa iliyotolewa jana na Ofisa Uhusiano wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tumaini Makene, ilimtaja aliyedaiwa kunyimwa fomu kuwa ni Said Mponda.

Aidha, taarifa hiyo ilieleza sababu za kunyimwa fomu kuwa ni kwamba zimeshachukuliwa na mtu mwingine ambaye ni Peter Urio.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilieleza kuwa Urio si mgombea wa chama hicho wala hakupatiwa barua ya kumthibitisha na kumdhamini mgombea.

"Msimamizi huyu amegoma kuwapa ushirikiano viongozi wa Chadema ambao wamefika pamoja na mgombea wa chama tangu asubuhi ili achukue, ajaze na kurejesha fomu za kugombea," ilisema taarifa hiyo.



James Mbatia

Taarifa hiyo ilieleza kuwa mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Chikaka Seti, aliyechukua fomu Jumanne na kuirejesha, ameenguliwa na CCM Makao Makuu juzi. "Hivyo, CCM kiutaratibu wameshajiwekea pingamizi kujiengua, wakateua mgombea mwingine Lazaro Sentimoja, ambaye ameenda leo (jana) mchana Ofisi ya Msimamizi Msaidizi Mtaa wa Muungano, Kata ya Goba na kuchukua fomu na amepewa akajaze, wakati mgombea halali wa Chadema kakataliwa," ileleza.

### MBEYA OFISI ZAFUNGWA

Jijini Mbeya, maofisa watendaji wa mitaa ya kata 14 wanadaiwa kufunga ofisi zao na kutoweka maeneo yao ya kazi, jambo lililosababisha kukwama kwa uchukuaji na urejeshaji wa fomu.

Hayo yalibainika wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani wa jiji hilo, ambao waliitaka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kuwachukulia hatua watendaji hao kwa madai kuwa wanaweza wakaharibu uchaguzi mzima.

Diwani wa Ilemi, Furaha Mwandalema, alisema katika kata yake na kata ya Ilomba watendaji wamezifunga ofisi kwa siku mbili bila taarifa yoyote, hivyo wagombea kushindwa kuchukua na kurudisha fomu.

Alimtaka Mkurugenzi wa Jiji hilo kuwaeleza madiwani kama juu ya hatua zilizochukuliwa dhidi ya watendaji hao wanaohatarisha jambo hilo.

"Hawa watendaji kwa sasa wana jukumu la kusimamia uchukuaji na urejeshaji wa fomu za wagombea kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa, lakini wengi wao mpaka sasa ni siku ya pili wamefunga ofisi, tunaomba tujuwe kama kuna hatua mkurugenzi amezichukua," alisema Mwandalema.

Naye Diwani wa Isyesye, Ibrahim Mwampwani, aliliomba baraza kujadili suala hilo kwa dharura ili lipatiwe ufumbuzi mapema kabla halijasababisha dosari kwenye uchaguzi.

Alisema endapo watendaji hao watabainika kuwa wamefanya hivyo kwa makusudi, wanatakiwa kuchukuliwa hatua kali za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine katika maeneo mengine ambao wana malengo kama hayo ya kuhujumu uchaguzi.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Oscar Kapinga, alithibitisha kuwapo kwa baadhi ya ofisi za watendaji ambazo zimefungwa na kwamba amemwagiza Ofisa Utumishi kufuatilia ili kujua walipo watendaji hao na sababu za kufunga ofisi zao.

Alisema watafuatilia ili kujua kama kuna kazi ambayo walikuwa wanafanya nje ya ofisi na kwamba ikibainika kuwa walifanya hivyo kwa makusudi watachukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria za nchi kwa madai kuwa kufanya hivyo ni kuwakosesha wananchi huduma bila sababu.

Alisema mtu yeyote ambaye atataka kuvuruga zoezi la uchaguzi lazima ashughulikiwe kwa mujibu wa sheria.

### ACT YATOA NENO

Uchambuzi uliofanywa na chama cha ACT Wazalendo, umebaini kuwapo kwa hujuma na njama ovu za wasimamizi wa uchaguzi dhidi ya demokrasia, vyama vya upinzani na wananchi kwa ujumla kunyimwa fursa ya kujiamulia nani awaongoze, nani awasimamie kutatua changamoto zilizopo katika maeneo yao na kushiriki kuleta mabadiliko na maendeleo.

Kwa mujibu wa taarifa kwa umma iliyotolewa na chama hicho, hujuma zilizoonekana ni kutokuwapo kwa maandalizi ya kutosha ya uchaguzi huo ikiwamo kukosekana kwa haki, usawa, uhuru na uwazi.

"Hujuma tulizoziona ni pamoja na fomu kudaiwa kuisha, fomu kutotolewa kwa ukamilifu (pungufu), wagombea kutakiwa kutolesha wenyewe nakala, kufungwa ofisi za wasimamizi wa uchaguzi, kukosekana mihuri, vitisho na kutekwa kwa wagombea na viongozi, wasimamizi kudai mambo yasiyoelezwa na kanuni na sheria (utambulisho toka mkoani)," ilibainisha taarifa hiyo na kuongeza:

"Jeshi la polisi kutochukua hatua sahihi kudhibiti uhalifu, kughushiwa kwa mihuri ya chama, wasimamizi kutokuwa na ufahamu sahihi wa masuala ya uchaguzi pia ni dosari."

Aidha, maeneo ambayo hujuma hiyo inadaiwa kufanyika fanyika ni Liwale, Bukombe, Songwe, Tabora, Busanda, Misungwi, Moshi Mjini, Morogoro Kusini Mashariki, Kasulu Vijijini, Tanga, Dar es Salaam, Newala, Mkoa wa Pwani na Mbeya.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, hawajaridhishwa na kauli ya Waziri kukemea suala hilo na kwamba, alipaswa kujua tofauti kati ya hujuma/njama ovu na dosari/upungufu.

"Zipo dosari kama kutokuwa na mihuri (Ruangwa) na baadaye mihuri hiyo kufika jimboni. Lakini huwezi kusema eti ni dosari pale inapotokea wasimamizi Jimbo zima hawapo ofisini (Liwale), fomu hazitolewi kwa wagombea wa Upinzani," alisema.

Aidha, ACT-Wazalendo imewaka viongozi na wanachama wake wote kusimama imara kudhibiti na kukabiliana na hujuma na njama ovu zinazopangwa dhidi ya viongozi na wagombea wa upinzani.

# Kigogo Takukuru amwandikia DPP kuomba yaishe

INATOKA UK. 5

alishawishi rushwa ya Dola za Marekani 50,000 kutoka kwa Thangavelu Nallavan Vall kama kishawishi cha kuharibu ushahidi wa tuhuma zilizokuwa zinamkabili za kukwepa kodi zilizokuwa zinamkabili.

Katika shtaka la nne, Wankyo alidai kuwa Februari 14,mwaka huu, mtaa wa Haile Selasie karibu na Merry Brown, Kinondoni, alishawishi rushwa ya Dola za Marekani 20,000 kutoka kwa Nallavan Vall kama kishawishi cha kuharibu ushahidi uliokuwa chini ya uchunguzi wake dhidi ya kukwepa kodi.

Wankyo aliendelea kwamba shtaka la tano, Februari 10, mwaka huu, eneo la Sabasaba, mshtakiwa akiwa mwajiriwa kama Mchunguzi Mkuu wa Takukuru, alipokea Dola za Marekani 20,000 wakati akijua ni zao la kutakatisha na zimetokana na rushwa.

Katika shtaka la sita, ilidaiwa kuwa Februari 19, mwaka huu, eneo la Village Super Market katika duka la kubadilishia fedha za kigeni la Electron, mshtakiwa alibadilisha sehemu ya Dola za Marekani 7,000 (alipata Sh. Milioni 16.1) kati ya 20,000 huku akijua ni zao la rushwa.

Katika shtaka la saba, ilidaiwa kuwa Februari 19, mwaka huu, eneo la Chamazi, Temeke jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alinunua ardhi eneo ambalo halijapimwa lenye thamani ya Sh. milioni 15.8 huku akijua fedha hizo ni za kutakatisha na ni zao la rushwa.

Kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za Uhujumu Uchumi, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote.



Wateja wakichagua nguo za mtumba katika barabara ya Anex, jijini Arusha jana. Wananchi wengi wa kipato cha kati na chini hupendelea matumizi ya bidhaa za mitumba kutokana na unafuu wa bei. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

Distributed via ippmedia

# Mkurugenzi atoa agizo kwa Ofisa Maendeleo ya Jamii Jiji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Halimashauri ya Jiji la Arusha, Dk. Maulidi Madeni,amemwagiza Ofisa Maendeleo ya Jamii wa jiji hilo, Mwanansiu Dosi, kuwaita ofisini kwake maofisa maendeleo wote wa Kata 25 ndani ya jiji kuweka utaratibu mzuri wa utoaji mikopo kwenye vikundi vya wananchi.

Alitoa agizo hilo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichokutana kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali ya maendeleo ya jiji hilo walifikia.

Madeni alisema kumekuwa na kelele nyingi toka kwa madiwani kuwa kuna upendeleo wa baadhi ya kata, hivyo ni vyema suala hilo likawekwa sawa na kuelimishana.

"Lakini nishauri pia nyie madiwani mnaolalamika wasaidieni wananchi wa maeneo yenu kubuni miradi yenye tija na kuwaingizia fedha haraka ili wanapoleta dokezo hapa lipite bila kutupwa maana si kila anayeleta hapa maombi anapata,' alisema.

Awali, baadhi ya madiwani, wakiongozwa na Diwani wa Levolosi, Ephata Nanyaro, walisema wanashangazwa na utaratibu wa utoaji mikopo unavyokwenda.

"Sisi tunaomba tuelezwe leo inakuwaje baadhi ya kata zinapewa mikopo vikundi zaidi ya viwili, wengine mpaka vikundi sita au vinne wakati kata zingine zinaambulia kikundi kimoja. Sasa hapa utaratibu upi unaangaliwa na sisi tukaeleze wananchi wetu," alisema.

Nanyaro alisema ni vyema kama kuna vigezo waelezwe ili wakaelimishe wananchi wao ambao wengi ni maskini wanahitaji mikopo hiyo ili wakabuni biashara na kujikomboa kiuchumi. Jiji la Arusha kwa mwaka 2018/19 lilishatoa mikopo ya zaidi ya Sh. Milioni 665 kwa vikundi 118 vya vijana na wenye ulemavu huku zaidi ya Sh. milioni 25 zikirejeshwa.

## Mil. 216/- kunufaisha wananchi Arusha DC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

HALMASHAURI ya Arusha DC wilayani Arumeru katika kipindi cha robo ya pili mwaka huu wa fedha 2019/20, imepokea zaidi ya Sh. milioni 216.98 kwa ajili ya kutekeleza miradi mitatu katika sekta ya elimu na miundombinu ya barabara.

Fedha hizo zimetolewa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), awamu ya III, kupitia miradi ya OPEC ulioanza kutekelezwa Juni, 2013 hadi sasa.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii ofisini kwake jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Arusha DC, Alvera Ndabagoye, alisema halmashauri yake, imepokea fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu.

Mkurugenzi huyo aliitaja miradi hiyo kuwa ni ujenzi wa kivuko cha Laroi, ujenzi wa nyumba mbili za walimu zenye sehemu za kuwezesha familia mbili kuishi kila moja katika Shule ya Msingi Lemuguru na Shule ya Msingi Losikito.

Pia alisema halmashauri imejipanga kutekeleza miradi hiyo kwa wakati na hasa kwa kuzingatia ubora unaoendana na thamani ya fedha zilizoletwa ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kupitia miradi hiyo, kama ilivyokusudiwa na serikali.

Aliwataka wananchi wa maeneo wanayonufaika na miradi hiyo, kujitoa kuchangia nguvu kazi ya asilimia 10 kama miongozo ya miradi ya Tasaf inavyoelekeza, ili utekelezaji uende kwa kasi na kukamilika kwa wakati na hatimaye kupata miradi minginei.

Akizungumza kwa niaba ya Mratibu wa Tasaf Halmashauri ya Arusha, Kabula Sukwa, alisema mchakato wa kupata makandarasi wa kutekeleza miradi hiyo uko hatua za awali na baada ya kukamilikahatua zote, miradi itaanza kutekelezwa na kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha.

# Mkurugenzi wa OBC ahenya rumande

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Kampuni ya Uwindaji ya Otterlo Business Coparation (OBC), inayomilikiwa na mwanamfalme wa Falme za Kiarabu, Isaya Mollel (59), amezidi kusota katika Gereza Kuu la Kisongo, baada ya kesi yake ya kuajiri raia 10 wa kigeni kinyume cha sheria, kuahirishwa hadi Novemba 13, mwaka huu.

Katika kesi hiyo Mollel ni mshtakiwa wa kwanza kwenye raia 10 wa kigeni waliokuwa washtakiwa sambamba na mkurugenzi huyo kwa kufanya kazi nchini bila vibali.

Raia hao wa kigeni walikiri makosa yao Oktoba 3, mwaka huu, na kulipa Sh. milioni 100 kisha kurejea katika nchi zao.

Akiomba kuahirishwa kwa kesi hiyo jana, Wakili wa Serikali Grace Madikenya, mbele ya Kaimu Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Arusha, Rose Ngoka, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine.


Baada ya maelezo hayo, Hakimu Ngoka aliuhoji upande wa utetezi uliowakilishwa na mawakili Goodluck Peter na Elvaison Maro kama una pingamizi juu ya hoja za upande huo na kujibu hauna pingamizi.

Baada ya majibu hayo, hakimu aliahirisha shauri hilo hadi Novemba 13 mwaka huu na mshtakiwa anaendelea kuwepo mahabusu licha ya shauri hilo kudhaminika kutokana na kukabiliwa na kesi nyingine ya uhujumu uchumi ambayo haina dhamana.

Machi 4, mwaka huu, Mollel alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha akikabiliwa na mashataka ya kuajiri raia 10 wa kigeni bila kufuata sheria za kutoa ajira kwa wageni. Raia hao, Darweshi Jumma, Riaz Aziz Khan, Mohammad Tayyab, Ali Bakhash, Abdulrahman Mohammed, Martin Crasta, Imtiaz Feyaz, Arshad Muhammad, Hamza Sharif na Zulfiqar Ali walitiwa hatiani baada ya kukutwa na kosa la kufanya kazi nchini bila kuwa na vibali.

Akimsomea mashtaka hayo, Wakili wa Serikali Elianenyi Njiro akisaidiwa na Wakili wa Idara ya Kazi Mkoa wa Arusha, Emmanuel Mweta, alidai kuwa mtuhumiwa huyo alitenda kosa hilo kati ya Novemba 2018 na Januari, mwaka huu, katika kampuni ya OBC, Loliondo, Ngorongoro mkoani Arusha.

Njiro alidai kuwa mtuhumiwa huyo aliajiri raia hao wa kigeni kinyume cha sheria ya kuratibu ajira na uhusiano kwa wageni, huku akijua ni kosa kisheria.



## HABARI KILIMANJARO

# Watoa maoni utafiti kahawa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

BAADHI ya wakulima wa kahawa wa wilaya za Siha na Hai, mkoani Kilimanjaro, wametoa maoni yao kuhusu utafiti wa kibaiolojia uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TACRi) kuhusu aina nne za wadudu wanaoweza kutumika kula wadudu wenzao waharibifu zao hilo.

Wamesema utafiti huo unaweza kuwa jibu sahihi la kuinua tena kahawa ya Tanzania katika soko la dunia.

Mkazi wa Kijiji cha Mlangoni, wilayani Siha, Jackson Abel, akizungumzia jana na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusiana na matokeo ya utafiti huo na hali ya kahawa nchini, alisema matokeo ya kisayansi yaliyotangazwa na taasisi hiyo yanapaswa kutumika kwa majaribio ili kuona kama yanaweza kuleta suluhisho.

Naye Gasper Olutu, mkazi wa Kijiji cha Kwa Sadala, Wilaya ya Hai, alisema kazi kubwa iliyofanywa na wataalam wa utafiti wa taasisi hiyo, kama utaungwa mkono na Wizara ya Kilimo unaweza kusaidia kuondoa umasikini na hata kuleta mabadiliko chanya katika kilimo hicho.

Hivi karibuni, TACRi katika ripoti yake ilisema wadudu hao wana uwezo mkubwa wa kuangamiza kabisa kizazi cha wadudu wa haribifu wa zao la kahawa likiwa shambani na kusaidia uzalishaji wa kahawa kuwa wenye tija kuanzia sasa.

Nipashe lilithibitishiwa kuwapo kwa mafanikio hayo na Mtafiti wa Wadudu wa TACRi, Fedrick Magina, kuhusu uthibisho huo wa kisayansi wa ugunduzi wa wadudu hao.

"Ni kweli tumegundua aina mpya nne za wadudu ambao tunaweza kuwatumia kuangamiza wadudu wanaoshambulia zao la kahawa, tunaamini kwamba wadudu hao watakuwa suluhisho la magonjwa ya kahawa yanayosababishwa na uvamizi wa wadudu tuliowazoea.

"Hii inaweza kuwa mafanikio makubwa na habari njema kwa wakulima wa kahawa nchini Tanzania, majibu ya kisayansi yanathibitisha kwamba wadudu hao wanaowashambulia na kuwala wadudu wenzao waharibifu wa zao la kahawa likiwa shambani wataongeza zaidi tija na ufanisi katika uzalishaji na uwekezaji wa kilimo cha kahawa," alisema

Kwa mujibu wa mtafiti huyo wa wadudu, aina mpya ya wadudu waliogunduliwa wamepewa jina la 'Dudukobe.'

Alipoulizwa ni kwa namna gani idara hiyo ndani ya TACRi imejipanga kuzalisha wadudu hao kwa wingi ili kuwasaidia wakulima wa kahawa kukabiliana na wadudu waharibifu, Magina alisema changamoto inayojitokeza kwa sasa ni namna ya kuwazalisha kwa wingi na kuwasambaza kwa wakulima.

Kwa ugunduzi huo, baadhi ya wakulima wa kahawa akiwamo Athanas Leba waliokuwa katika maadhimisho ya 26 ya wakulima wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara, wameeleza kufurahishwa kwao na ujio huo wa majibu ya kitafiti ya kukabiliana na magonjwa ya zao hilo.

# Wagoma kuhamia ofisi mpya halmashauri

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SARAKASI za madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi kutaka kupingana na agizo la Rais John Magufuli la kuhamisha ofisi kutoka mji wa Moshi na kwenda Kolila, zimeanza kuwagawa wanasiasa hao na watendaji.

Tangu Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Kastori Msigala, alipoutangazia umma kuwa ofisi hizo zitahama rasmi Novemba 5, mwaka huu, kwenda katika majengo ya iliyokuwa Shule ya Sekondari Kolila, madiwani na wabunge wa majimbo mawili ya uchaguzi wanapanga mikakati ya kwenda kukutana huruma ili wasihame eneo kwenye eneo la KDC.

Inaelezwa kwamba tayari baraza hilo limeunda kamati maalum ya wajumbe wanane ambao watakwenda kuwasilisha ombi la kutohamisha ofisi za halmashauri hiyo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Michael Kilawila (Chadema), wanaounda kamati hiyo inaongozwa na Mbunge wa Vunjo (NCCR-Mageuzi), James Mbatia, Mbunge wa Moshi Vijijini (Chadema) Anthony Komu na Lucy Owenya (Viti Maalum- Chadema).

Wengine ni Kilawila mwenyewe, Makamu Mwenyekiti, Exaud Mamuya (Chadema), Moris Makoi (CCM), Filbert Shayo (NCCR-Mageuzi) na Diwani wa Uru Kusini (Chadema), Wilhard Kitali. Kabla ya kutangazwa kwa kamati hiyo, Kitali aliwasilisha hoja maalum akisema madiwani waliridhia kuhamishia ofisi hizo katika Shule ya Sekondari Kolila na kazi ya kufanya usafi katika eneo hilo inaendelea, lakini wananchi wamepinga na kudai ofisi hizo zisihame kwa kuwa zipo katika eneo rafiki la wao kupata huduma. Alisema kutokana na maoni ya wananchi, wameamua kuunda kamati itakayokwenda kumuona Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, na kumweleza umuhimu wa ofisi hizo kutohamishwa.

Kwa mujibu wa Kitali, iwapo jambo hilo litashindikana, halmashauri hiyo yenye majimbo mawili ya Moshi Vijijini na Vunjo wataomba yagawanywe na kila jimbo liwe na halmashauri yake.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Raphael Choma, alisema wakiwa watumishi wa halmashauri wanatekeleza agizo la serikali na kwa sasa wanaendelea kufanya usafi Kolila na wanatarajia kuhama kuanzia Novemba 5, mwaka huu.

Oktoba 7, mwaka huu, Jafo alitangaza kuwa halmashauri 31 ikiwamo Moshi ambazo zina ofisi nje ya maeneo yao ya utawala kama hazitahama maeneo hayo katika kipindi cha siku 30, zitafutwa.

Shule ya Sekondari Kolila ambayo awali, ilikuwa ikimilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini, ilifungwa zaidi ya miaka 10 iliyopita kutokana na kushindwa kujiendesha.




Mkurugenzi wa Ununuzi na Ugavi wa Benki ya CRDB, Pendason Philemon (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 kwa Kaimu Mkuu wa Chuo cha Taaluma ya Polisi Moshi, Gemini Mushy, iliyotolewa na benki hiyo, kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya wanawake chuoni hapo, katika hafla iliyofanyika mjini Moshi, mkoani Kilimanjaro, juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Waitara afurahishwa ukarabati Umbwe

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, ameelezea kuridhishwa kwake na hatua iliyofikiwa kwenye ukarabati wa shule kongwe ya kitaifa ya sekondari ya Umbwe iliyoko wilayani Moshi.

Shule hiyo ilitengewa na serikali Sh. milioni 960 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu na madarasa ili kuirejeshea katika hali yake ya unadhifu kama ilivyokuwa zamani.

Akizungumza jana baada ya kukagua ukarabati unaoendelea, Waitara alisema wizara hiyo haina shaka na kiwango cha ujenzi huo, wala kasi ya mkandarasi aliyepewa kazi ya ukarabati kwa kuwa serikali ngazi ya Wilaya ya Moshi imetimiza wajibu wake vyema.

"Jambo la kwanza, Wizara tunasema tumeridhishwa na hatua hii ya ujenzi ulipofikia kwa sasa, lakini shukrani za pekee ni kwa Rais John Magufuli kuona umuhimu wa kutoa fedha ili kuzikarabati shule kongwe za umma hasa zilizoko katika Mkoa wa Kilimanjaro," alisema.

Awali, Diwani wa Kibosho Magharibi, Deogratius Mushi (CCM), akizungumza kwa niaba ya wananchi, alimweleza Naibu Waziri kwamba kabla ya serikali kuchukua uamuzi wa kuikarabati, majengo ya shule hiyo pamoja na miundombinu yake ilikuwa katika hali mbaya zaidi kiasi cha kuhatarisha usalama wa wanafunzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastori Msigalla alipoulizwa kuhusiana na mradi huo, alisema: "Bado kazi inaendelea na taratibu za mifumo kuruhusu kiasi cha fedha kutumika ili kubadili mandhari au mwonekano wa majengo ya shule hii kongwe ya kitaifa haina mashaka.

"Lengo la serikali katika utaratibu huu wa ukarabati wa shule kongwe ni kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuwa rafiki kwa watumishi na wanafunzi kwa ujumla wake. Lakini pia ni kurudisha au kuongeza hadhi ya shule hizi," alisema mkurugenzi huyo

Hadi sasa, shule mbili kongwe ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ambazo ni Umbwe na Ashira, zimekwishaingia kwenye mpango huo wa serikali wa kukarabati shule kongwe na tayari zimepatiwa fedha.

Aidha, Umbwe imepewa Sh. milioni 969,669,148 kwa ajili ya ukarabati.





Mkurugenzi Mtendaji wa Foundation for Civil Society (FCS), Francis Kiwanga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma juzi, kuhusu uzinduzi wa wiki ya Azaki 2019, itakayofanyika kitaifa Novemba 4 hadi 8, mkoani humo. Kushoto ni Mkurugenzi wa Wowap, Fatuma Towfq na Mwenyekiti wa Shivyawata Taifa, Ummy Nderiananga. **PICHA: PETER MKWAVILA**

Distributed via ippmedia

# Jafo aziagiza matumizi ya fursa mfumo ulioboreshwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amezitaka halmashauri nchini kuanza kutumia mfumo ulioboreshwa wa fursa na vikwazo kwa maendeleo. Jafo alitoa kauli hiyo juzi alipokuwa akiwatunuku wanafunzi 4,191 wa chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo tuzo za astashahada ya awali, kati na stashahada.

Alisema mfumo huo umeandaliwa na chuo hicho kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la maendeleo japan (Jica) kusaidia halmashauri kutumia fursa zinazopatikana kwenye maeneo yao.

"Mfumo huu ulioboreshwa utazisaidia halmashauri zetu katika kupambana na vikwazo vya maendeleo na kuona ni namna gani zinaweza kutumia fursa zinazopatikana katika maeneo hayo," alisema Jafo.

Alipongeza chuo hicho kwa kuwa wabobezi na mahiri katika maandiko yenye kutoa dira na mwelekeo wa kupambana na changamoto zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Aidha, Waziri Jafo aliwataka wanafunzi hao kwenda kufanya kazi kwa weledi na uaminifu ili waweze kutangaza sifa njema ya chuo hicho. "Najua wengi hapa mtaajiriwa na mtaajiriwa katika halmashauri zetu nataka muende mkazitendee haki halmashauri hizo, mkafanye kazi kwa bidii na kuleta mabadiliko chanya katika mamlaka zetu za serikali za mitaa," alisema.

Pia aliwataka kufuata sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma kwenye utendaji kazi wao wa kila siku.

"Mkafanye kazi kwa umakini mkubwa ili tuzidi kuwa na wataalamu wenye weledi ili maendeleo ya Taifa yaweze kufikiwa,"alisema.

Naye, Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Mpamila Madale, alisema chuo hicho mbali na kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi pia kimejikita katika utafiti, kutoa ushauri wa kitaalam na kuandaa machapisho ya kitaaluma.

Alisema mpaka sasa kina wanafunzi 7,436 na kulazimika kujenga darasa moja lenye uwezo wa kubeba wanafunzi 504 kwa kutumia mapato ya ndani.

Mkuu huyo alifafanua kuwa wahitimu waliohitimu ni wa astashahada ya awali ya ugavi na ununuzi, menejimenti ya rasilimali watu, utunzaji wa kumbukumbu na maendeleo ya jamii.

Kwa upande wa astashahada ya kati ni utawala katika serikali za mitaa, uhasibu na fedha katika serikali za mitaa, ugavi na ununuzi, menejimenti ya rasilimali watu, utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka na maendeleo ya jamii; Pia wanafunzi waliohitimu katika ngazi ya shahada ni wa fani za utawala katika serikali za mitaa, uhasibu na fedha katika serikali za mitaa, menejimenti ya rasilimali watu, maendeleo ya jamii, ugavi na ununuzi.

# Wajasiriamali Chamwino wapewa somo

**Na Peter Mkwavila ,** CHAMWINO

WAJASIRIAMALI wametakiwa kufuata misingi ya uendeshaji wa biashara kwa kuwa na mpango kazi na utafutaji masoko ili zisitetereke.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkufunzi kutoka Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (Sido), Crispine kapinga, ambaye pia ni Ofisa maendeleo ya biashara katika mafunzo ya usimamizi wa biashara zinazotokana na kilimo na mifugo wilayani hapa.

Mafunzo hayo yametolewa kwa viongozi wa vikundi 20 vijiji vya Fufu, Chiboli na Suli.

Kapinga alisema kuna mambo ya msingi yanayotakiwa kuangaliwa ili biashara isitetereke.

"Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha wananchi kuondokana na miradi isiyozingatia mazingira, hivyo kusababisha biashara kuanguka," alisema.

Alisema moja ya mambo yanayotakiwa ili biashara kukua ni wajasirimali hao kuwa na mpango kazi na utafutaji wa masoko.

"Msijifungie ndani tafuteni masoko pale mlipo na nje ya pale," alisema.

Naye Meneja Miradi wa Shirika la Good Neighbour, Hamis Ally, alisema wajasiriamali hao wamejifunza masuala ya masoko na biashara kutokana na kuzalisha mazao ya kilimo na mifugo na wapo kwenye vikundi vya hisa.

"Wengi wao hufanya biashara zao kwenye minada, changamoto kubwa kwa wajasiriamali wengi ni kwenye uelewa na kujaribu," alisema.

# Kamishna TRA ataja tiba utovu wa maadili

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NCHI wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zimetakiwa kutilia mkazo suala la maadili ili kutokomeza vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya watumishi wa mamlaka za mapato.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede, alisema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa 10 wa Mamlaka za Mapato Afrika Mashariki (EARATC) kuhusu maadili, unaoendelea jijini hapa huku akisema vitendo hivyo vinakwamisha ukusanyaji mzuri wa mapato.

Mkutano huo utajadili upitishaji wa mapato haramu mipakani na namna ya kushirikiana katika kutoa adhabu kwa wanaofanya makosa hayo.

"Pia masuala ya maadili kama vile utovu wa nidhamu kwa watumishi wetu wa mamlaka za mapato yatajadiliwa. Lakini pia tutaona namna ya kushirikishana katika kutoa adhabu kwa wafanyaji makosa katika upande mmoja aweze kudhibitiwa na upande mwingine," alisema Dk. Mhede.

Mwenyekiti anayeongoza mkutano huo, Dk. Protazio Begumisa, kutoka Uganda, alisema sababu ya kukutana mara mbili kila mwaka ni kujadili na kuweka mikakati itayosaidia kupambana na rushwa.

"Tunakutana mara mbili kila mwaka kwasababu sisi sote tunafahamu kwamba rushwa haiheshimu mipaka na tusipokuwa makini wafanyabiashara wengi wataendeleza rushwa toka Dar es Salaam, Mombasa, Burundi hadi Rwanda kwani hawa watu wanatafuta mianya katika kazi zetu na endapo tukizubaa kidogo tunapoteza mapato," alisema.

Naye Katibu wa Kamati ya EARATC, Esther Masibayi, kutoka Kenya, alieleza kupambana na rushwa, kukusanya kodi ni muhimu.

"Tunapokusanya kodi tujue kuwa kuna wengine wanakwepa kulipa kodi na kuendeleza vitendo hivyo viovu ndiyo maana lengo letu ni kuondoa hiyo tabia ya ukwepaji kodi ili tuongeze mapato katika serikali zetu.

"Tunapopambana na rushwa lazima tukamate na tuwafunge watu lakini hatuna magereza ya kutosha, hivyo kikubwa ni kuwaelimisha ili wabadilike ndiyo maana tunapaswa kubadili fikra zao ili waache kukwepa kodi. Wakibadilika hii itawafanya wawe watu wema katika kulipa kodi na serikali zetu zitapata mapato ya kutosha," alisema Masibayi.





Mfanyabiashara ndogo akipanga viatu wakati akisubiri wateja, katika eneo la Posta mpya, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mkuu wa Mkoa akemea kutandaza bidhaa chini

Distributed via ippmedia

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Khasan Khamis Khasan, ameeleza kukerwa na mtindo wa kuweka bidhaa chini na kuliagiza baraza la manispaa la mji huo kutengeneza maeneo ya wafanyabiashra ndogondogo ili kuzuia kuweka vyakula ,mboga na matunda chini.

Bidhaa huwekwa chini kwenye soko la Darajani maarufu kama Markiti ambalo pamoja na wazawa kununua vitu, hutumiwa pia na watalii kutoka mataifa mbalimbali.

Khasan alitoa agizo hizo mara baada ya kufanya ziara katika soko hilo na kujionea hali ya wafanyabiashara wengi ambao wametandaza bidhaa zao chini.

Alisema jambo hilo ni hatari kwa afya ya watumiaji hususani katika kipindi hiki cha mvua zinazoendelea kunyesha na kusomba taka za aina mbalimbali.

Alisema ni vyema baraza la manispaa likanusuru hali hiyo mara moja ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu watakaoutumia wafanya biashara hao na kuachana na mtindo wa kutandaza bidhaa zao chini.

Alisema ni muhimu kutii agizo hilo ili kulinda usalama wa afya za wauzaji na wanunuzi wa bidhaa mbali mbali katika soko hilo maarufu.

"Hii ni hatari sana kiafya , bidhaa hizi za vyakula kupangwa chini hususan wakati huu wa mvua, ni hatari . Viongozi hebu haraka angalieni namna gani wafanyabiashara hawa wataweza kuuza bidhaa zao kwa hali ya usalama ikilinganishwa na jinsi kulivyo sasa," aliagiza.

Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa ya Mjini Saidi Juma Ahmada, aliahidi kulifanyia kazi agizo hilo, ili kuweka mazingira ya mji kwenye usafi na kuvutia wageni wanaokuja kutembelea mji wa Zanzibar.

Alisema soko hilo la Darajani au Markiti linatumiwa na wafanyabiashra wengi hususan wakati wa jioni. Alisema pamoja nao wapo wataalii ambao hufika katika soko hilo kununua bidhaa mbalimbali vikiwamo viungo.

Wafanyabiashara wa soko hilo walieleza kufarijika na ziara ya Mkuu wa Mkoa iliyowezesha kutatua changamoto hiyo ya kuweka bidhaa chini.

## Mtaala elimu ya awali waanza kuimarishwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TAASISI ya Elimu Zanzibar, imeahidi kuendeleza juhudi za kuimarisha mfumo wa mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi ili taifa litoe na kupata elimu bora.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Zanzibar, Suleiman Yahya Ame, wakati akifungua mkutano wa uwasilishaji wa mfumo wa mtaala wa elimu ya maandalizi na msingi kwa wafanyakazi wa taasisi hiyo ili kutoa maoni yao.

Alisema lengo la kukusanyiko huko ni kupitia vyema mfumo wa ufundishaji ili kutoa mapendekezo yao na kupata mtaala bora wenye kukidhi mahitahi ya jamii pamoja na kuwezesha kutoa elimu bora kwa ngazi hizo.

Alisema ni vyema wafanyakazi wa taasisi hiyo kuwa makini pamoja na kuwasilisha mapendekezo bora yatakayoleta mafanikio kwa mtaala huo wa elimu ambao utatumiwa kwenye shule za maandalizi na zile za msingi.

" Muangalie mambo ambayo yateweza kukuza elimu yetu na kuifanya iwe bora kuanzia ngazi za chini. Maandalizi na msingi ndiyo nguzo katika kukuza elimu yetu hivyo matumaini yangu katika upitiaji wa mfumo huu uchunguzwe kwa kina,"alisema Ame.

Mkurugenzi huyo aliishukuru Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Wizara ya Elimu Zanzibar, kwa kuona umuhimu wa kuyafanyia marekebisho mambo muhimu ya mtaala huo.

# Unywaji kahawa watikisa visiwani Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA wa kahawa kutoka zaidi ya nchi 24 wanashiriki katika maonyesho ya kuandaa kinywaji cha kahawa yaliyoanza jana mjini Zanzibar na kuvutia wadau mbalimbali.

Nia ya kusanyiko hilo ni kuwawezesha wajasiriamali wa kahawa kuandaa kahawa kwa ladha mbali mbali zinazovutia wateja kutoka mataifa mbalimbali duniani.

Naibu Waziri wa Kilimo Maliasili Mifugo na Uvuvi Dk. Makame Ali Ussi, akiwa katika shughuli hiyo, alisema kuna haja ya kuhamasisha wananchi kulima kahawa ili kuanza uzalishaji kwa nia ya kukuza uchumi wa nchi .

Aliyasema hayo jana baada ya kufungua maonyesho ya kahawa yanayofanyika katika ukumbi wa hoteli ya kitalii iliyoko Mangapwani na kuwaambia washiriki kuwa zao hilo linaweza kukuza uchumi lakini pia kutoa ajira kwa wananchi.

Alisema asilimia kubwa ya Wazanzibari ni wapenzi wa kahawa ambao wanaitumia majumbani kama kiburudisho na wakati wa jioni kwenye baraza za mazungumzo ndiyo sababu ya kuwapo kwa wafanyabiashara wengi wanaouza kahawa katika migahawa na vibanda mbalimbali mjini Unguja na kwenye viunga vyake.

Aidha, aliwataka wakulima kujishajihisha katika kilimo cha kahawa pamoja na mazao mengine yanayostawi visiwani ili kuondoa uhaba wa chakula nchini.

Pia alisema kufanya hivyo kutawezesha upatikani wa mazao mbalimbali kwa wingi ambayo yatasaidia kupunguza uhaba wa chakula na pia yataongeza wingi wa mazao ya biashara nchini.

Naibu Waziri wa Kilimo wa Tanzania Bara Omar Mgumba, akizungumza kwenye uzinduzi huo, aliwataka wakulima wa kahawa kuzidisha bidii katika kuzalisha ili kujiongezea kipato katika soko la ndani na nje ya nchi .

Alitoa wito kwa wakulima hao kuzingatia utaalamu wanaoupata kwa walimu wao ili kuongoza soko la ndani pamoja na kuongeza uzalishaji kwa wingi.

Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TanTrade), Latifa Khamis, alisema fursa ya mafunzo kwa wauzaji wa kahawa yataweza kuleta mafanikio kwa wauzaji hao pamoja na sekta ya utalii kwa kupitia maonyesho haya.


Alisema upatikanaji wa wataalamu waliobora katika utengenezaji kahawa kutaweza kurudisha ari ya kunywa kahawa visiwani kwa kurudisha utamaduni huo wa Zanzibar . Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda imepokea na kusimamia mafunzo na maonyesho hayo kwa lengo la kutoa elimu kwa wauzaji na wapishi wa kahawa na kuwawezesha kuimarika zaidi katika kuandaa kutayarisha kahawa .

Kamal, ambaye ni ofisa tendaji wa kampuni moja kutoka Uganda alisema lengo la kuwafanyia mafunzo wauzaji wa kahawa ni kuwapa utaalamu zaidi ili kufikia viwango wanavyohitaji watumiaji.

Mwenyekiti wa umoja wa wauza kahawa Yussuf Suleiman Ali, alisema maonyesho hayo yatawawezesha wafanyabiashara kutengeneza kahawa yenye kiwango cha ubora na hadhi ya kimataifa.

Uwekezaji huo wa kunywa kahawa umefadhiliwa na Wizara ya Biashara na Viwanda, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara TanTrade na Bodi ya Kahawa Tanzania.

Nipashe BT



**TOKE AMFANYIA KUFURU MSAIDIZI WAKE** Soma UK.20

JUMAMOSI NOVEMBA 2, 2019



Distributed via ippmedia

## HAWAPATANI TENA

# Labda uje upepo wa kisulisuli

## BASI SAWA



## Ragvox kutambulisha singo mpya

MWIMBAJI anayechipukia katika muziki wa kizazi kipya Mansoor Rashid, maarufu kama 'Ragvox' ametaja ujio wa wimbo wake mpya hivi karibuni.

Amesema wimbo huo unaoitwa Dawa'utamletea heshima kipindi utakaamua kuutambulisha rasmi kwa mashabiki wake.

Kibao hicho kimerekodiwa na studio ya PMM kitakuwa hewani baada ya kumalizika mchakato wa kutengeneza video yake.



## Rich kweli hutaki kuwa upepo?

MWIGIZAJI mkongwe wa filamu, Single Mtambalike, amesema kitu anachopenda katika kazi zake ni kitendo cha kuingiliwa na mashabiki ili kwenda na fikra zao.

Akiongea na EATV na EA Radio, Single ambaye maarufu kama Rich, alisema ukimya wake una mambo mengi mazuri na kwamba yeye sio mtu  wa kupiga kelele kama wasanii wengine wanavyofanya.

"Ukisikia mtu amefanya kitu halafu anasema hivi na vile kama kuahidi vitu vinavyokuja halafu inakuwa kimya hamna kitu, lakini mimi tangu nimechukua tuzo nimekuwa hivi hivi sitaki kuburuzwa na style zinazokuja hapa katikati nikazifuata halafu nikapoteza muelekeo wangu " amesema.


Distributed via ippmedia

# Danzak amkaribisha Wema kiaina

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Danzak, amekanusha kuwa na uhusiano wa kimapenzi na Wema Sepetu, bali ukaribu wao unatokana na urafiki wa kawaida.

Akizungumza hivi karibuni, Danzak ambaye anafahamika pia kwa jina la Rubani, amesema moyo wake unampenda Wema na kamwe hawawezi kuachana urafiki wao kwa taarifa za uongo zinazosambaa mitandaoni.


"Unajua Wema na mimi tuna urafiki wa karibu, labda watu wanavyotuona wanadhani tuna uhusiano wa kimapenzi, lakini kama rafiki yangu nampenda," amesema Danzak.

## INSTA-TWITTER





Njia kubwa ya kushinda majaribu ni kukubali kuongozwa na Roho wa Mungu. Hapo utafanikiwa na shetani atabaki anakushangaa- **Muna Love.**



Nazeeka na utamu wangu. Nasikia utamu... Nasikia utamu... Nasikia utamuuu- **Faiza Ally.**



# Ommy Dimpoz asababisha Kiba, Mond kujadiliwa

STAA wa muziki wa Bongo Fleva, Omary Nyembo maarufu kwa jina 'Ommy Dimpoz' ameibua mjadala mkali mitandaoni baada ya kumuangusha bosi wake Alikiba kwa kunyakua Tuzo ya AFRIMMA 2019.

Katika sherehe za tuzo hizo zilizofanyika hivi karibuni Dallas nchini Marekani, Dimpoz aliibuka kupitia kipengele cha Msanii Bora wa Kiume Afrika Mashariki.

Katika komenti za watu mbalimbali mtandaoni wamekuwa wakihoji namna alivyompiga kumbo Kiba ambaye ni kiongozi wa lebo ya Rockstar4000 na Diamond Platnumz ambao wote waliwania tuzo moja.

"Wengi hatukutegemea kabisa kwanza kama tuzo hii itaenda kwa Dimpoz kutokana na ushindani uliokuwapo kwenye kipengele chake akiwemo Diamond na Kiba. Dimpoz ameonesha ujanja kwa hili na kuweza kumpiku hadi bosi wake," alikomenti mfuasi mmoja anayejiita Queen_aps.




**>>> Usikose Jarida hili la Burudani Tele (BT) ndani ya Gazeti lako la Nipashe kila Jumamosi, pia lipo kwenye mtandao wa kijamii Twitter, tu' follow**

**@burudanitele**

UNASEMAAA...

# Pole Idris, uvumilivu utakusaidia

BAADA ya msanii wa vichekesho, Idris Sultan, kuripoti kituo cha polisi Kati jijini Dar es Salaam, baadhi ya mashabiki wamemshauri kuwa mvumilivu.

Idris alijikuta akikabiliana na nguvu ya dola baada ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam, Paul Makonda, kuamuru akamatwe kutokana na kitendo chake cha kuhariri picha ya rais Magufuli.

Katika mitandao ya kijamii, watu mbalimbali walijitokeza kumpatia maneno ya kumtia moyo ikiwamo kumtaka kuwa mvumilivu katika kipindi kigumu anachokabiliana nacho.


Distributed via ippmedia

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag
**@burudanitele**



**Naona** unanishawishi nikuongezee kidada chako...mwanangu lakini mmmh-**Chuchu Hans.**



**Kuna** muda mawazo yanaweza kufanya ufike mbali hata kujua, ila usijaribu kuyapa nafasi mawazo yakutawale kaza moyo songa mbele-**Nandy.**



**Usiniletee** mambo ya darasa la pili unaniibia penseli alafu unanisaidia kutafuta. Mwanaume huwa anaongeaga mara moja tu, sasa ukitaka watu wajue unayonifanyia hata kwenye hilo tamasha hatokuja mtu. Sasa tuishie hapo nakutakia tamasha njema-**Ali Kiba.**

Kuumbe!



HAWAPATANI TENA

# Labda uje upepo wa kisulisuli

AMA kweli usemi wa mabeberu wawili kamwe hawatumiki kwa bwana mmoja umedhihirika baada ya wasanii wakubwa nchini, Diamond Platnumz na Ali Kiba, kuvuana nguo hadharani kwa kuonesha wana ugomvi usiokwisha.

Wasanii hao wiki hii wamejikuta wakipamba mitandao ya kijamii baada ya kutoleana povu huku wakitishia kutoleana siri kwa mambo wanayofanyiana ambayo yapo nyuma ya pazia.

Hata hivyo, baadhi ya watu wamekwenda mbali wakitaka ugomvi huo kuanikwa hadharani ili jamii wafahamu nini wanachotofautiana na yale wanayofanyiana ambayo Ali Kiba, ametishia kuyaanika hadharani.

Chanzo cha hali hiyo kutibuka ukuti jana na kitendo cha Diamond kuweka nia ya kumualika Ali Kiba katika tamasha lake la Wasafi Festival 2019 linalofanyika wiki inayokuja jijini Dar es Salaam.

Licha ya Ali Kiba kutajwa kuingizwa kwenye orodha ya wasanii watakaoalikwa, pia msanii mwingine Harmonize ambaye hivi karibuni alijiengua lebo ya WCB, naye alimtaja angependa kushiriki. Muda mfupi baada ya kutamka maneno hayo, haraka Ali Kiba alijitokeza na kumbwatukia Diamond kuacha kusema uongo na akatumia maneno makali akimtaka kuacha kuzungumzia suala hilo kwa kuwa bado anamfanyia mambo ya kiadui.

"Usiniletee mambo ya darasa la Pili unaniiibia penseli alafu unanisaidia kutafuta (UNIKOME). Mwanaume huwa anaongeaga mara moja tu sasa ukitaka nikuweke uchi watu wajue unayonifanyia hata kwenye hilo tamasha hatokuja mtu sasa tuishie hapo nakutakia tamasha njema @ diamondplatnumz,". Aliandika Ali Kiba kwa ghadhabu.

Baada ya ujumbe huo mkali, baadhi ya watu walionekana kushtushwa na hali hiyo na kuelezea imefikia wakati kwa wasanii hao kuyasema mambo hayo ili jamii ifahamu ugomvi wao.

Wanasema kwa sasa wasanii hao wanaonekana hawawezi tena kukaa chungu kimoja kutokana na maumivu wanayopeana, Hata hivyo Ali Kiba ndiye anaonyesha kuathirika zaidi na ndio maana akaamua kupasua jipu hadharani.

Baadhi ya mashabiki wanadhani labda kuwepo na maombi maalum ili uje upepo wa kisulisuli uwafikie na kuwatakatisha nyoyo zao kwa ajili ya kila mmoja asafike na kusamehe.




TWANGA PEPETA

# Hawa kiboko ya Twanga Pepeta

Na Adam Fungamwango

MWANZONI mwa miaka ya '90 na mwanzoni mwa miaka mwaka 2000 kulitokea mapinduzi makubwa ya muziki wa dansi nchini.

Kuliibuka aina ya muziki ambao uliathiriwa na bendi za Congo DR kama Wenge Musica, Extra Musica na nyingine zinazofanana na hizo.

Aina ya upigaji wao na ziara za bendi hizo hapa nchini ulisababisha kuundwa kwa bendi moja iliyoitwa Diamond Sound wana Kibindankoi ambayo kwa kiasi kikubwa iliiga nyimbo hizo, zingine ikizitoa kwa lugha ya Kikongo na kuziimba kiswahili.

Hili lilipokelewa vema na mashabiki wa muziki wa dansi nchini, kiasi cha kuathiri kidogo bendi zilizokuwa zikipiga rhumba kama Msondo, Sikinde na nyingine.

Miaka michache baadaye ikaundwa bendi inayoitwa African Stars, iliyotumia mtindo wa Twanga Pepeta. Bendi hii ilikuja kutetemesha na kufanya mapinduzi makubwa, kwa kuchukua vionjo vya bendi za Congo DR na kuziimba kiwa kiswahili, wakiongozwa na marehemu Ramdhani Masanja maarufu kama Banza Stone, Ally Choki na wengineo.

Baada ya kulitesa soko la muziki nchini, baadaye ziliundwa bendi zenye mlengo kama huo, ambazo zilipa ushindani mkubwa Twanga Pepeta na kunyang'anyana mashabiki na kuzua upinzani mkubwa kama wa Simba na Yanga.

**TOT PLUS BAND**

Ni bendi ya mwanzo kabisa iliyoanza kuitingisha Twanga Pepeta. Kwanza kabisa ilichofanya ni kumchukua kinara aliyekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu na kipenzi cha bendi hiyo, Banza Stone.

Kujiunga kwa Banza kwenye bendi ta TOT kulisababisha upinzani mkubwa wa bendi hizi mbili na pia kuipaisha.

Mwanzoni bendi ya TOT ilikuwa ndani ya sanaa za maonyesho na haikuwa inajitegemea yenyewe, lakini kujiunga na Banza kuliifanya bendi hiyo kutoka kwenye kundi hilo la sanaa na kuwa bendi kamili inayojitegemea.

Pili ikawa maarufu na kuwa mshindani halisi wa Twanga Pepeta, kiasi cha kuvuta mashabiki wengi zinapopambana laivu au kupambanishwa kwenye redio na TV.

**MCHINGA SOUND BAND**

Ilianzia mkoani Lindi, lakini ikaja kufanya makazi yake jijini Dar es Salaaam. Ni bendi ambayo nayo ilikuja kuisumbua mno Twanga Pepeta, kwa sababu iliwachukua baadhi ya wanamuziki wake kama Adolf Mbinga, Joseph Watugulu, Rogat Hega 'Katapila' na wengineo.

Hali hii ilisababisha mashabiki wa Twanga Pepeta kuiona si bendi rafiki kwao na kukawa na upinzani mkali si kati ya bendi hizo mbili tu, bali hata uongozi wa bendi hizo mbili nao mara kwa mara ulikuwa ukiingia kwenye mzozo wa kila moja kudai kuifanyia njama ya kuidhohofisha bendi nyingine.

**CHUCHU SOUND BAND**

Kama kuna bendi ambayo ilikuja kwa kasi na kuondoka kwa kasi vile vile ni hii. Chuchu Sound ni bendi ndogo tu ambayo iliundwa na baadhi ya wanamuziki wa Kikongo na Kitanzania, lakini ilitesa na kuzoa mashabiki wengi kwa muda mfupi na kuziacha bendi nyingine, ikiwemo Twanga Pepeta zikiulizana.

Sababu ni staili yao. Ilikuja na aina mpya ya muziki ambao ulikuwa ni wa kimwambao maarufu kama 'mduara' uliokuwa ukihanikizwa na vionjo kutoka kwa wanamuziki kama Omari Mkali, Chuchu Yusuph mwenyewe, Mao Santiago, Jenico Flower na wengineo.

Ilipiga muziki wa aina zote, kama wa bendi za Twanga Pepeta, na mduara pia, lakini nyimbo za mduana ndizo zilioitambulisha zaidi bendi hiyo na kupendwa, ikasababisha bendi nyingi ikiwemo TOT kuanza kuiga nao kupiga mduara.

**FM ACADEMIA**

Baada ya kuipa changamoto Diamond Sound Band, wakati huo ikiitwa FM Musica, ilibadilisha jina na kujiita FM Academia. Sasa ikahamia kuipa wakati mgumu Twanga Pepeta, ikiwa na kina Nyosi El Sadaat. Ni bendi ambayo kwa kipindi kirenfu imetoa ushindani mkubwa kwenye muziki wa dansi nchini hasa wa kizazi hicho kuanzia mwishoni mwa miaka ya '90 hadi leo.

**STONO MUSICA 'WAJELAJELA ORIGINAL'**

Historia ya bendi hii haitofautiani na ya Chuchu Sound. Ilikuja kwa moto mkali, lakini ukazimika ghafla. Ilisumbua na kutesa, si kwa Twanga Pepeta tu, bali bendi zote na hasa FM Academia ambapo wanamuziki wengi walitoka huko.

Baadhi ya wanamuziki wa FA Academia raia wa Congo DR walikamatwa kwa kuishi nchini bila vibali.

Walikaa rumande kwa muda na baada ya kutoka walitunga wimbo wa 'Prison' au 'Chozi la Mnyonge,' lakini muda mfupi tu baadaye, walijiengua kwenye bendi yao na kuunda Stono Musica ambayo iliyotoa vibao kama 'Binadamu', 'Jimmy Chocolate,' 'Majivuno' na nyingine nyingi

# Vijimambo

PICHA ILIYOPITA




1. Wanasema eti mimi chizi. Watanzania bwana kwa figisu! - Majuto Magazeti, Miyomboni Iringa.
2. Duuh! Jamani kazi kwanza, kuselifika baadae - Bahati, Kiwalani DSM.
3. Hii mitandao ya kijamii inatutesa. Kwa hii selfii kila mtu atakomenti 'nice' - Agatha Mbale, Moro Town.
4. Natafuta picha ya kutupia 'whatsap' - Dullah Dimoso, Tabata DSM.
5. Kijana hiyo simu imepitwa na wakati, ipeleke makumbusho - Oiso, Nyaishozi Tegeta DSM.
6. Ukisikia uchizi taslimu, basi ndio huo. Simu ya mezani na selfii! - Mama Nah, Manzese DSM.
7. Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.
8. Yes, hapa sasa pozi limekubali, ngoja nijifotoe sasa - Samwel Sungi, Utemini Singida.
9. Hii simu vipi, mbona sioni sehemu ya kujiselfisha? - Msabaha J. Msabaha, Mikindani Mtwara.
10. Lazima baby wangu aikubali hii picha, si selfii ya kitoto - Beneali Moussa Beneali, Migombani Zenji.
11. Hii inaitwa 'ekotite', muulizeni Kofi Olomide anaifahamu sana - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
12. Kweli ushamba mzigo. Wewe, sio kila simu unaweza kujiselfisha nayo - Mariam Beneali, Migombani Zenji.
13. Ha ha haaa, usitake ncheke mie! Hebu rudisha simu ya watu ofisini - Moussa Beneali, Migombani Zenji.
14. Hapo 'chacha'! Disco limeingia watu wa kabila lileee! Mtajuta kuijua selfii - Rehema Jumbe, Kwanjeka Tanga.
15. Mnashangaa nini? Mie sijiselfishi kama nyie, mie fundi simu jamani - Dully, Kiembesamaki Zenji.
16. Ukitaka kugombana naye, mwambie kuwa hiyo simu haiselfishi - Antar, Makumbusho Kijitonyama DSM.
17. Hapa sasa mademu wote wa 'bush stars' wangu - Nahoja Mazengo, Mbande Chamazi DSM.
18. Wewe! Hebu acha ushamba wako bwana, unawaabisha Wairinga wenzip - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
19. Hiyo selfii yako inanitia homa kwa kicheko - Bimkubwa Ausi Juma, Michenzani Unguja.
20. Hilo ndio tatizo la Wahehe wakishaingia mjini - Jimmy Mwaipiana, Keko Bora DSM.
21. Kaa hivyo hivyo, baada ya 'masaa' kadhaa utaona sehemu ya kupigia picha inajionyesha - Judi, Mbezi Mwisho DSM.

**SMS Bomba ya Leo:**
**Watu watajua najipiga selfii, watati mie namtoa mende kwenye simu - Dully, Kiembesamaki Zenji.**

PICHA MPYA



TUMA MESEJI - 0785652621




## Thamani Yangu Mchuma Janga hula na wa kwao

Distributed via ippmedia

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI mwingine binadamu anaweza kufanya jambo na ukawa unajiuliza alikuwa anafikiria nini. Kuna baadhi ya watu wana tabia ya kunyanyasa wenzao, wapenzi wao, mke au mumewe kwa sababu ambazo anazijua mwenyewe.

Kuna watu ambao hawana heshima kwenye ndoa, badala yake wananyanyasa wenzao na wanaona raha jinsi wanavyoumia. Hata hivyo wakati mwingine mambo hugeuka kwa sababu Mwenyezi Mungu hulipa hapa hapa duniani.

Filamu ya 'Thamani Yangu', inafundisha watu kuheshimu thamani ya ndoa zao, au wapenzi wao ambao wamewachagua wenyewe kwa hiari yao.

Kitendo cha kumpuuza, kumtesa, au kumnyanyasa mpenzi wako, au ndoa yako, ni jambo baya kwani huko mbele ya safari linaweza kugeuka

Imechezwa na wasanii Haji Salum Baba Haji, Mohamed Fungafunga'Mzee Jengua', Riyama Ally na wengineo. Filamu inaanza kuonyesha kuwa Beni ana mpenzi wake ambaye ni mlemavu wa mguu.

Ulemavu haukufanya kumpenda msichana huyo na kumuahidi kumuoa kama mambo yataenda kama yalivyopangwa.

Beni anaaga kijijini kuwa anakwenda mjini kutafuta maisha na mambo yakiwa mazuri atarejea kumchukua mpenzi wake na kusaidia wazazi wake.

Anafika Dar, jiji la raha na karaha, anafanikiwa kupata kazi kwenye kampuni moja ya saruji. Anapewa nyuma na gari ya kutembelea.

Mji unampokea Beni, kwani anasahau kila kitu. Anasahau wazazi hata mpenzi wake mlemavu aliyemuacha kijijini.

Kazi yake kubwa akitoka kazini ni starehe, kunywa pombe na kubadilisha wanawake kama nguo. Taarifa hizo zinafika kwa wazazi wake kijijini.

Nao wanatuma taarifa ya uongo kuwa mama yake kijijini ni mgonjwa sana na karibuni atakata roho. Nihilo tu lilimfanya Beni arejee kijijini na kukutana na asichotarajia. Anapofika anaambiwa amuoe mpenzi wake na kwenda naye mjini kwa sababu sasa ana kazi. Anafanya hivyo kwa shingo upande.

Anapofika mjini badala ya kuwa mke, anamgeuza kuwa mateka au mtumwa. Mkewe mlemavu analazwa stoo na kufanyiwa kazi kibabe na nzito, licha ya hali aliyonayo. Mahawara wa Beni, wakiongozwa na Riyama ndiyo wanafanya kazi ya kunyanyasa, kumkejeli, kumsuta na pia kumnyima chakula, kiasi cha dada huyo mlemavu kuamua kutoroka na kuingia mtaani kuwa ombaomba.

Anakutana na Baba Haji ambaye mbali na ulemavu aliuonao, alipomuangalia zaidi aligundua ni mwanamke mwenye kitu cha ziada. Akampenda. Akampeleka nyumbani kwake na kumuambia nia yake ni kutaka kumuoa.


Kabla ya yote anamsomesha na baadaye kumfungulia biashara. Mambo sasa yanamnyookea dada huyo mlemavu aliyekuwa mke wa Beni.

Siku moja dada huyo anakutaka na mumewe Beni akiwa katika hali mbaya kiuchumi. Alipomuuliza akamwambia kuwa amefukuzwa kazi na wanawake zake wote wamemkimbia. Huruma ikamuangia dada wa watu akaamua kumpeleka kwa mumewe mtarajiwa Baba Haji na hakutaka kumficha akamueleza kila kitu.

Pamoja na hayo akashauriwa kwenda kupima kwani afya yake haikuonekana kuwa ni nzuri. Anagundulika kuwa ana virusi vya ukimwi.

Taarifa hiyo inamshtua Baba Haji, naye anamwambia mpenzi wake waende wakapime. Wote wanakutwa safi. Kwa ridhaa yake, Beni anatoa talaka kwa mkewe ili kumpa nafasi aolewe na mwanaume mwingine ambaye ni Baba Haji, huku akijutia nafsi yake kwa yote aliyoyafanya huko nyuma.

Licha ya kubaguliwa, kukejeliwa, kunyanyaswa kwa ulemavu alionao, anapata mume mwema na maisha mazuri juu.



## KANISA LA SHETANI

# Lamwonya Kanye West

KANISA linalomwabudu shetani, limemjia juu rapa Kamye West, likimwonya kwenda kinyume na kanuni ya mafundisho yao baada ya kutoa albam yake mpya yenye jina la kumtukuza Yesu Kristo.

Albamu hiyo mpya ya Kanye West inaitwa 'Jesus is King' ikimaanisha 'Yesu ni Mfalme' ambayo aliitambulisha wiki hii.

Kanye tayari ametoa maelezo kwamba yeye kwa sasa amezaliwa upya, ndiye maana ameamua Albam yake kuipa jina hilo kwa lengo la kumtukuza Mungu.

Hata hivyo, kupitia ukurasa wake wa Twitter. Kanisa hilo limemuonya na kusema kinachofanywa na mwanamuziki huyo ni kinyume na kanuni ya Anton Szandor LaVey.

Sehemu ya kanuni ya kanisa hilo inasema

"Shetani ni rafiki wa kanisa,Shetani amekuwa rafiki mzuri zaidi wa Kanisa hili, kwani amekuwa akifanya biashara katika miaka hii yote."

Hii, pia, ni moja ya vifungu tisa za Shetani zilizoandikwa katika sura za utangulizi katika Biliblia ya Shetanin kulingana na jarida la habari la Urusi, Sputnik.

Kanye anasema katika Albamu yake ya tisa inazingatia uhusiano wake na Mungu pamoja na mapigano yake na Ibilisi, Ndani yake kuna nyimbo za amani lakini zikiimbwa kwa mtindo wa rap.

Mwanamuziki hivi karibuni amekuwa muumini wa dhati wa Ukristo na kila jumapili anafanya matamasha ya nje ya nyumba yake kumtukuza Mungu.

Anasemekana ameahidi kutofanya muziki wa kidunia tena na atazingatia kueneza injili pekee.

Katika mahojiano yaliyochapishwa wiki hii, rapa huyo alisema yuko katika huduma kamili kwa Mungu.

Akiongea na Apologia Studios wiki iliyopita, mchungaji anayemsimamia rapa huyo Adam Tyson, alisema kuwa Kanye alikuwa karibu kabisa kujiondoa kwenye muziki huo wakati fulani.

"Wakati mmoja, aliniambia kuwa hataki kubaki," alisisitiza Tyson. "Nilisema, 'Kwa nini?' Akanijibu 'Kweli, huo ni muziki wa Ibilisi.'

Aidha mchungaji huyo alimshauri kutumia muziki huo kwa ajili ya kumsifu |Mungu.

"Nadhani alikuwa tayari akiifikiria kidogo, lakini hakika nilisema, Halo, ndugu. Nadhani unahitaji kutumia talanta zako ambazo Mungu amekupa na utumie jukwaa hilo kwa Mungu. '"

Kanisa la Shetani limejibu kwa ukali kwa kutumia mtandao wa Sputnik na Twitter.

Distributed by ippmedia



# Mashabiki waipongeza mahakama kumfunga muuaji

MASHABIKI wa mwanamuziki Moses Ssekibogo maarufu Mowzey Radio ambaye aliuawa kwa kuchomwa kisu, wameipongeza mahakama baada ya kumpa kifungo Troy kwa kupatikana na hatia ya kuua.

Mahakama Kuu nchini Uganda imemuhukumu kifungo cha miaka 14 jela Godfrey Wamala maarufu Troy kwa kosa la kuua bila ya kukusudia.

Radio alifariki Februari 1, 2018 baada ya kupigana na Troy wakiwa baa.



## Kimoprah sema ukweli kama upo singo

ALIYEKUWA mshiriki wa Big Brother Naija (BBNaija) Kim Opara maarufu kama Kimoprah, ameamua kujitokeza bado yupo singo.

Kujitokeza kwa Kim kunatokana na taarifa zilizoenea mitandaoni kwamba amevishwa pete ya uchumba na hivi karibuni atafunga ndoa na mshiriki mwenzake wa shindano hilo.

Kulingana na maelezo yake, amesema bado yupo huru na gtaarifa hizo hazina ukweli na ni sehemu ya uvumi wa mitaani.

## P Diddy atokwa jasho kubadili jina

Distributed via ippmedia

RAPA mkongwe wa Marekani, Sean John Combs almaarufu kwa jina la P. Diddy, anakamilisha utaratibu wa kubadilisha jina lake la kati 'John' na kuitwa LOVE ili kwenda na mfumo wa maisha yake wa sasa.

P. Diddy ameamua kutoa jina la 'John' na kutumia Love, Kwa madai kuwa kwa sasa hayupo tayari kutumia majina aliyokuwa anayatumia kama vile P.Diddy, Puffy, Diddy na Puff Daddy.

Kwa mujibu wa mtandao wa ET, P. Diddy tayari ameshawasilisha ombi lake la kubadilisha jina hilo katika Mahakama Mjini Los Angeles, Marekani.





## Toke amfanyia kufuru msaidizi wake

STAA na mrembo kutoka Nigeria, Toke Makinwa amefanya kufuru baada ya kumzawadia gari msaidizi wake binafsi kusherehekea siku yake ya kuzaliwa.

Kulingana na taarifa hizo, Toke alikabidi zawadi hiyo kwa msaidizi waken Onise wakati wa hafla iliyohudhiriwa na marafiki zake wa karibu.

"Nilijua tayari kwamba nahitaji kutimiza miaka 35, kumnunulia gari msaidizi wangu ni jambo pekee ambalo litampa furaha, nafikiri Mungu atambariki," alisema Toke.

## Pete ya harusi ya Nicki Minaj usipime

KILA kukicha habari mpya zinazidi kuibuka zinazohusu ndoa ya siri ya rapa Nicki Minaj na mumewe Kenneth Petty.

Habari mpya ni pete aliyovishwa Minaj ambayo inaelezwa ina thamani ya dola milioni 1.1

Kulingana na mtandao wa TMZ, Nicki na mume wake walihakikisha wanapata pete ya thamani na ya kipekee kufanikisha harusi yao.



SAFU



MIONZI YA SHERIA

# Sababu, umuhimu kushiriki uchaguzi serikali za mitaa- 2

**Na John Juma 0716217615**

WIKI iliyopita tuliona kuwa ilipofika Mei 1969, ushuru wa mazao uliokuwa unatozwa na serikali za mitaa na vijiji, ulifutwa na uamuzi huo katika masuala mengi uliathiri kwa kiasi kikubwa mapato ya serikali za mitaa na vijiji nchini.

Licha ya kwamba serikali zilitegemea zaidi misaada na ruzuku kutoka serikali kuu baada ya vyanzo kadhaa vya mapato yake kufutwa, pia katika kipindi hicho hicho Hazina ilipunguza ruzuku kwa serikali hizo.

Uamuzi huo ulitokana na sababu kwamba Hazina au Serikali Kuu ilichukua baadhi ya majukumu ambayo hapo awali yalikuwa ya serikali za mitaa na vijiji. Mfano wa majukumu hayo ni kama vile ulipaji wa mishahara ya walimu wa shule za msingi wa daraja "A" na "B" na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kusomea'.

Wizara nyingine, kama ya Afya, Ujenzi na Madini nazo pia kwa wakati huo zilichukua baadhi ya majukumu ya serikali hizo hivyo tena, kupelekea upungufu wa mapato, na hatimaye halmashauri nyingi zilishindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, hali ambayo ilisababisha kujikuta katika migogoro na serikali kuu.

Kwa kifupi, madaraka mikoani au serikali za mitaa na vijiji yalirudishwa rasmi mwaka 1982 kisheria. Lengo likiwa ni kusogeza huduma zaidi za kimaamuzi kwa wananchi ili kurahisisha mbinu za kuwafikishia maendeleo.

Serikali za mitaa zinajumuisha mikoa, wilaya, vijiji na vitongoji huko wananchi wamepatiwa mamlaka ya kuchagua viongozi wao katika maeneo husika. Sanjari na kusimamia rasilimali zao kama vile ardhi, kukusanya mapato, kupanga bajeti na kusimamia matumizi.

Umuhimu wake ni kuwapatia wananchi mamlaka za kimaamuzi kupitia vikao vyao wenyewe kama vile katika halmashauri za wilaya au vijiji kupanga bajeti na kusimamia fedha zinazotolewa na serikali kuu kwa ajili ya maendeleo katika maeneo yao.

**MAJUKUMU**

Mwenyekiti wa Mtaa au Kijiji kikatiba ndiye mkuu wa serikali katika ngazi hiyo.

Ana wajibu wa kuitisha na kuongoza mikutano yote ya halmashauri ya ngazi hiyo, pamoja na mikutano mikuu ya pia.

Lakini endapo mwenyekiti hayupo katika mkutano wowote, wajumbe wa mkutano unaohusika wanaweza kuchagua mwenyekiti wa muda wa mkutano huo.

Mwakilishi wa mtaa au kijiji kwenye Kamati ya Maendeleo ya Kata Ward Development Commetee.

Ana jukumu la kuhudumia kwa usawa wana-mtaa au kijiji wote, bila kujali tofauti za kisiasa, kijinsia au za kidini na

Anatakiwa kuwa mfano wa uongozi na utendaji bora wa kazi, kwa kuwa na shughuli zake mwenyewe za kujitegemea kimapato ambazo zinaweza kuigwa na wana-mtaa wa kijiji wenzake.

**MADARAKA/ MAJUKUMU**

Mkutano Mkuu wa Kijiji ndiyo unaosimamia na kuwajibisha watendaji, kuweka taratibu za namna ya kuitisha vikao vya dharura.

Kupitia Mkutano Mkuu Maalum wa Uchaguzi huwachagua wenyeviti wa kijiji na wajumbe wa halmashauri ya kijiji.

Unahusika kujaza nafasi za viongozi wa halmashauri ya kijiji zilizo wazi. Aidha, hujadili na kupokea au kukataa taarifa za utekelezaji wa shughuli za kijiji kutoka halmashauri ya kijiji.

Jukumu jingine ni kupokea, kujadili na kupitisha au kukataa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha zakijiji,aidhahupokea, kujadili na kupitisha au kukataa mapendekezo ya kodi, ushuru na vyanzo vingine vya mapato ya kijiji.

Pia, hupokea na kujadili taarifa ya makusanyo ya fedha za kodi, ushuru na mapato mengine ya kijiji, kujadili na kufanyia maamuzi mapendekezo ya serikali ya kijiji ya kutunga sheria ndogo ndogo.

Kupokea na kujadili na kuyafanyia maamuzi masuala kuhusu ugawaji wa ardhi na matumizi ya rasilimali zingine za kijiji.

Kazi nyingine ni kuhoji, kudadisi, kukosoa, kukubali au kukataa taarifa na mapendekezo ya serikali ya kijiji.

Aidha, huhusika kuondoa madaraka serikali ya kijiji au mjumbe yeyote kabla ya muda wao na hupitisha azimio la kumkaripia rasmi mjumbe yoyote wa halmashauri au halmashauri kwa ujumla kwa utendaji mbovu.

Distributed via ippmedia



KALAMU YA MWALIMU

# Hukumu hii ni ushindi vita ndoa, mimba utotoni

**Na Reubeni Lumbagala**

NDOA za utotoni ni moja ya changamoto kubwa inayoikabili sekta ya elimu hapa nchini. Tatizo la ndoa za utotoni huwaathiri sana wanafunzi mabinti ambao safari yao ya kuendelea na elimu huwa mashakani kwani mshahara wake ni kufukuzwa shule.

Baadhi ya wazazi na walezi wanapoona watoto wamepata ujauzito, huamua katika umri mdogo na kuwakosesha haki yao ya msingi ya kupata elimu, lakini wakati mwingine sheria iliwaruhusu.

Kutokana na uwepo wa changamoto ya mimba za utotoni katika maeneo mengi ya nchi yetu hasa vijijini, jitihada mbalimbali zimekuwa zikifanywa na wadau kukomesha changamoto ya mimba za utotoni.

Pamoja na jitihada za kukomesha mimba za utotoni, kulikuwa na udhaifu wa sheria ambayo ilitoa mwanya wa mwendelezo wa mimba za utotoni na kusababisha wanafunzi mabinti kuwa katika hatari ya kushindwa kufikia elimu ya juu kutokana na baadhi yao kukwama katika safari ya kimasomo baada ya kupata mimba wakiwa shuleni.

Juma lililopita, serikali ilishindwa katika kesi ya ndoa za utotoni baada ya Mahakama ya Rufaa kutupilia mbali pingamizi la serikali lililokuwa likitaka sheria ya ndoa ya mwaka 1971 inayoruhusu mtoto kuolewa chini ya miaka 14 iendelee.

Taasisi ya Msichana Initiatives inayojihusisha na utetezi wa watoto wa kike katika kuhakikisha watoto wa kike wanapata haki zao ndiyo iliyofungua kesi kutaka sheria hiyo ya ndoa ya mwaka 1971 irekebishwe ili iruhusu mtoto wa kike aolewe akiwa na umri wa miaka 18 au zaidi na si miaka 14 kama ilivyo sasa.

Sheria ya ndoa ya mwaka 1971 inaruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na miaka 14 huku mtoto wa kiume akiruhusiwa kuoa akiwa na miaka 15.

Sheria hii inatoa mwaya kwa mtoto wa kike na wa kiume kujiingiza katika mahusiano ya ndoa akiwa katika umri mdogo wakati ambao alipaswa kuwa shuleni.

Naamini hukumu ya Mahakama ya Rufani kupendekeza umri wa kuolewa kwa mtoto wa kike uwe ni miaka 18 ni mwanzo mzuri kuelekea katika mafanikio ya vita ya ndoa za utotoni.

Hii ni kutokana na ukweli kuwa, yeyote anayeoa au kuolewa akiwa chini ya miaka 18 anakuwa amejiingiza katika ndoa za utotoni.

Hivyo basi, sheria ya ndoa ya mwaka 1971 ilitoa mwanya kwa wazazi na walezi kuwa huru kuozesha mabinti zao wakiwa katika umri mdogo kutokana na sheria hiyo kuunga mkono ukatili huu dhidi ya mtoto wa kike.

Mabinti wamekuwa wakiathirika katika jamii kutokana na uwepo wa mila na desturi potofu zinazowanyima haki zao muhimu.

Kutokana na tatizo hili, Umoja wa Mataifa (UN), umeweka mikakati mbalimbali ambayo serikali za nchi mbalimbali duniani zimekubaliana kutekeleza katika kuleta ukombozi wa mtoto wa kike hasa katika nyanja muhimu ya elimu. Mkakati mmojawapo ni mapambano dhidi ya ndoa za utotoni.

Nchi zote zimekuwa katika juhudi za kuhakikisha vikwazo vyote dhidi ya mtoto wa kike katika kupata elimu vinaondoshwa ili kuweka mazingira bora kwa ajili ya mabinti kusoma na hatimaye kuhitimu salama safari yao ya kutafuta elimu katika taasisi mbalimbali za elimu.

Kalamu ya Mwalimu inaungana na uamuzi wa Mahakama ya Rufani katika kupendekeza umri wa kuolewa mtoto wa kike uwe si chini ya miaka 18.

Ni wakati muafaka kwa serikali kuwasilisha bungeni mapendekezo ya marekebisho ya vifungu namba 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ili kubatilisha ridhaa ya sheria hiyo ya kuruhusu ndoa za utotoni na kuathiri moja kwa moja juhudi na kazi kubwa inayofanywa na serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo katika kukuza na kuiendeleza sekta ya elimu kwa maendeleo endelevu.

Hata hivyi watetezi wa haki za watoto teteeni jinsia zote, msiishie tu katika kumtetea mtoto wa kike huku mkisahau kuwa hata mtoto wa kiume hayuko salama kupitia sheria ya ndoa ya mwaka 1971. Watetezi wa haki za watoto waweke mkazo kuwa umri sahihi kwa mtoto wa kike kuolewa na mtoto wa kiume kuoa uwe si chini ya miaka 18.

Ndoa za utotoni zinawatumbukiza watoto wa kike na wa kiume katika majukumu ya kifamilia huku wakiwa bado hawajakomaa kiakili na kimwili kwenye kulea familia.

Kipaumbele cha wazazi na walezi kiwe kuwapa watoto wao elimu bora na si kuwaingiza katika ndoa za utotoni. Hukumu ya Mahakama ya Rufani ni mwelekeo mzuri wa ushindi dhidi ya ndoa na mimba za utotoni. Tafakari

**Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**

**Maoni: (+255) 764 666349.**




Balozi Paul Sherlock (kulia), Mwakilishi Mkazi wa UNFPA, Jacqueline Mahon na Mratibu wa Mradi wa HIV kutoka UNFPA Dk. Majaliwa Marwa, katika tukio la kusaini mkataba wa yuro 1,000,000.

# UNFPA inavyoigeuza Kigoma pepo ya kinamama, wasichana

**Na Sabato Kasika**

AFYA ya uzazi ni muhimu kwa ajili ya maendeleo endelevu kwani hili ni eneo linalohusu kumjali na kumhudumia binti ambaye ni mama mtarajiwa, kumtunza mjamzito ili apate mtoto kwa usalama na pia ulinzi kwa mchanga huyo ili kumwepusha na maradhi na udumavu.

Uzazi salama unaangalia pia mikakati ya kupata watoto kwa mpango, lakini bila kulisahau janga kubwa la kuondoa ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa wanawake na mabinti.

Haya ni mambo ambayo huongeza umaskini na kusababisha athari nyingi kama magonjwa ya kuambukiza hasa VVU na Ukimwi, aidha huchangia kinamama na wasichana kukosa elimu na haki nyingine nyingi za msingi.

Balozi wa Ireland nchini, Paul Sherlock, wiki hii jijini Dar es Salaam, anarejea umuhimu wa suala hili akisema usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wanawake ni mambo muhimu ili kuwawezesha wapate huduma za afya na pia upanuzi wa huduma za afya ya uzazi lazima uendane na kumwezesha mwanamke kiuchumi, kijamii na pia ukihusisha kuzuia ukatili wa kijinsia.

Anayaeleza hayo jijini Dar es Salaam kwenye hafla ya kusaini makubaliano ya kutoka na kupokea yuro 1,000,000 takribani Sh.bilioni 2.5 kwa ajili mradi wa kuboresha afya ya wanawake katika wilaya nne mkoani Kigoma.

Fedha hizo zinazotolewa kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani na Maendeleo (UNFPA) na Ubalozi wa Ireland.

Anaeleza kuwa takribani bilioni 2.5 zinaelekezwa kwenye mradi huo wa mwaka mmoja uitwao 'ujana wangu nguvu yangu'.

Wanufaika wa mradi huo ulioanza Agosti mwaka huu ni Wilaya za Kakonko, Kasulu Mjini, Kasulu Vijijini na Kibondo.

Balozi Sherlock anasema:"Tunaipongeza serikali ya Tanzania kwa kuboresha afya ya wanawake na watoto. Afya ya mama, mtoto, na vijana waliopevuka inapewa kipaumbele katika sera za afya Tanzania."

Anaeleza kuwa ushirikiano kati ya UNFPA na Ireland ni sehemu tu ya mchango wa nchi hiyo mkoani Kigoma na kupitia msaada huo, Shirika la Kuhudumia Watoto (UNICEF) linatekeleza mpango wa huduma ya afya ngazi ya jamii, na kutoa huduma kwa kaya masikini.

"Kuendeleza afya na usafi wakati wa hedhi ni muhimu kwa afya ya wanawake na mabinti wa rika linalopevuka, ili wasikose kuhuduria shule au wengine kuacha shule , wasichana wa rika hili lazima wawe na huduma muhimu pamoja na vyoo safi shuleni," anasema Balozi.

Aidha, anasema mradi huo utachangia ujenzi wa vyoo katika shule 12 zenye uhitaji mkoani Kigoma na kwamba Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) linaimarisha hospitali za wilaya, huku Shirika la Benjamin Mkapa(Benjamin Mkapa Foundation) linawezesha upatikanaji wa wahudumu wa afya vituoni.

Anafafanua kuwa pia kuna utafiti unafanyika ili kupata suluhisho endelevu kwa tatizo la uharibifu wa mazingira unaosababisha wanawake kuwa kazi nyingi za kutafuta nishati za kuni na mkaa.

"Kwa ujumla ni kwamba hadi sasa Ireland imechangia fedha kisasi cha yuro milioni 7.7, ambazo ni sawa na Sh. bilioni 19 kwa ajili ya kusaidia huduma za afya mkoani Kigoma," anasema.

NGUVU ZAIDI

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Jacqueline Mahon, anasema, mradi huo umeongezewa nguvu baada ya Ubalozi Ireland nchini kutoa kiasi hicho cha fedha ili kuhakikisha unafanikiwa.

Anasema, wanachokifanya ni moja ya vipaumbele vya serikali na kwamba kwa msaada uliotolewa na Ireland watahakikisha hakuna kijana anayebaki nyuma kwenye mradi huo.

"Tunataka kuwapa vijana wa Kigoma matumaini, kujua haki na mahitaji yao katika nyanja zote na hasa uamuzi kwenye mambo ya mahusiano ili waweze kuwa salama," anasema Mahon.

Anaema, ushirikiano kati ya Ireland na UNFPA ambao ulianza Julai mwaka jana umasaidia kutenga maeneo muhimu kwa ajili ya kuharakisha maendeleo kuhusu masuala ya kujamiiana na haki ya afya ya uzazi.

Anaeleza kuwa mwaka wa kwanza wa mradi huo, zaidi ya vijana 60,000 walipatikana na kuanzisha vituo vitatu katika kambi ya Nyarugusu kwa ajili kuelimishana mambo mbalimbali yanayohusu afya.

"Vituo hivyo pia ni kwa ajili ya utoaji wa taarifa sahihi kuhusu afya na jinsi ya kuwa na maamuzi kuhusu mambo ya kujamiiana na afya ya uzazi , ambazo vijana huwa wanazipata," anasema.

Anasema, UNFPA inataka kuwajengea uwezo vijana, hasa wa kike kwa kila njia na kuwapa maarifa kwa vile wanahitaji kujitambua na kujiongoza na hatimaye kufikia malengo waliojiwekea katika maisha.

KWANINI KIGOMA

Mratibu wa Mradi wa Ukimwi na VVU wa UNFPA Dk. Majaliwa Marwa, anasema, mkoa wa Kigoma unakabiliwa na changamoto nyingi zinazohusu afya ikiwamo kuwa na idadi kubwa ya vifo vya kinamama wakati wa kujifungua.

Anasema pia mimba za utotoni ni nyingi pamoja na vitendo vya ukatili wa kijinsia ni vingi, hivyo wameuchagua kutokana na sababu hizo na nyingine nyingi ili kusaidia kuboresha afya na kuondoa kasoro hizo.

"Kihistori mkoa wa Kigoma unapokea wakimbizi wengi na hadi sasa wapo zaidi ya 300,000, wakiwa katika kambi za Nyarugusu, Nduta na Mtendeni hawa wanatoka Burundi. Mfumo wa utoaji huduma ya afya katika kambi hizo inakuwa na changamoto hivyo ni muhimu kuuboresha," anasema Dk. Marwa.

Anaeleza kuwa mradi huo unalenga kuhakikisha vijana hasa wasichana wanapata huduma ya afya ya uzazi, na kwamba shirika hilo linashirikiana na serikali na wadau wengine kwa ajili kuufanikisha.

"Mwongozo wa serikali unataka kila kijiji kuwa na watoa huduma ya afya wawili, na sisi UNFPA kwa kushirikiana na wadau wengine tutahakikisha tunatoa mafunzo ili kufanikisha hilo," anasema.

Vile vile Dokta Marwa anasema, UNFPA itashirikiana na Wizara ya Afya, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), uongozi wa Kigoma na halmashauri za maeneo husika ili kuhakikisha kwamba mradi huo unaleta tija na mafanikio.

**MAKALA**

# Ni wakati wa Sumbawanga kufurahia 'mafuriko' ya maji

**Na Mwandishi Wetu**

HIKI ndicho tulichokuwa tunakitaka. Ndivyo wanavyosema wakazi wa Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, wanaosema hivyo baada ya kilio chao cha muda mrefu cha kukosa majisafi na salama kupata ufumbuzi.

Wanasumbawanga na viunga vyake takribani 70,932 wanafungua maji ya bomba baada ya kazi hiyo kukamilika na Rais Dk. John Magufuli kuuzindua mradi huo hivi karibuni akiwa ziarani Rukwa.

Anawaambia serikali kwa kushirikiana na Umoja wa Ulaya (EU) na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KFW) wamechangia upatikanaji wa maji kwa gharama ya Sh. milioni 35.

Wakati akizindua rasmi mradi huo mwezi uliopita Rais Magufuli, anasifu kazi hiyo na kuipongeza Wizara ya Maji kwa jitihada kubwa na kazi nzuri iliyofanyika.

Rais anawageukia wakazi wa Sumbawanga akiwataka kutunza na kuthamini huduma hiyo ili udumu kwa muda mrefu na inufaishe wateja wengi.

Anaeleza kuwa serikali itaendelea kuwekeza zaidi kwenye sekta ya maji ili kumaliza tatizo la maji na kuwafanya Watanzania wafurahie huduma ya uhakika ya maji ambayo ni bidhaa ya muhimu kwa ajili ya ustawi kiafya na kiuchumi kwa kila binadamu.

**TAARIFA YA MRADI**

Waziri wa Maji Profesa Makame Mbarawa, anaishukuru serikali kwa kuyapa maji umuhimu wa kipekee kwa kutoa kipaumbele cha kuanzishwa na kukamilishwa miradi mingi ambayo sasa kazi za uwekezaji kwenye sekta hiyo zimefikia zaidi ya miradi 547 ikiwamo 468 ya vijijini na 79 ya mijini.

Yote hiyo ikiwa na thamani ya Sh. trilioni 3.98 na kwamba mingi ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na umaliziaji.

Waziri Mbarawa, anazungumzia mradi wa Sumbawanga akieleza kuwa ulikamilika Novemba, mwaka 2017 na kwamba muda wa matazamio ulikuwa mwaka mmoja, ambao ulikwisha Desemba 2018.

Anasema katika mradi huo mengi yamefanyika baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni uchimbaji wa visima 17, ufungaji wa pampu kwenye visima hivyo vyenye uwezo wa kutoa maji lita milioni 13 kwa siku.

"Umehusisha pia kulaza mabomba yenye urefu wa kilometa 14.2 kutoka kwenye visima kwenda kwenye tangi la kukusanyia maji, kulaza bomba kuu za kupeleka maji mjini zenye urefu wa kilometa 21.8, kujenga mtandao wa usambazaji maji katika mji wa Sumbawanga wenye urefu wa kilometa 68 na ujenzi wa matangi ya maji sita ya kuhifadhia maji yenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 7,000." Anasema Mbarawa.



Maji na kuboresha huduma muhimu za kijamii imekuwa ajenda kuu ya awamu ya tano. Pichani, Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa (kulia), akikagua miradi ya maji katika moja ya ziara zake mikoani. **PICHA: MTANDAO.**

**UJENZI WA MRADI**

Ujenzi wa mradi huo umesimamiwa na Mamlaka ya

Majisafi na Usafi wa Mazingira, Manispaa ya Sumbawanga (Suwasa) na kujangwa na kuanzia, Machi 8, mwaka 2013 hadi 2017.

Akizungumzia mafanikio ya mradi huo, Kaimu Mkurugenzi wa Suwasa, mhandisi Gibon Nzoa, anasema umeongeza uzalishaji wa maji kwa kiwango cha lita 7,500,000 kwa siku na kufikia lita 20,500,000 kwa siku.

Ukilinganisha na mahitaji ya sasa kwa Manispaa ya Sumbawanga ni lita 13,000,000 kwa siku hivyo kuna ziada.

"Kimsingi huduma ya majisafi imeongezeka kutoka wakazi 70,935 sawa na asilimia 52 hadi kufikia wateja 106,400, sawa na asilimia 78, ukilinganisha na idadi ya wakazi katika Manispaa ya Sumbawanga ambao ni 136,414," anasema na kuongeza:

"Ubora wa maji yanayosambazwa kwa wananchi umeongezeka na kufikia viwango vinavyokubalika kimataifa , eneo lenye mtandao wa majisafi limeongezeka kutoka kilometa 134 sawa na asilimia 52 na kufikia kilometa 240 ambazo ni asilimia 80."

Hata uwezo wa matangi wa kutunza maji umeongezeka kutoka lita 1,350 hadi 8,350, huduma bora ya maji yanayopatikana itaendelea kuchangia katika maendeleo ya sekta nyingine zinazotegemea maji kama viwanda, hoteli, utalii na usafi wa mazingira ambao umeboreka baada ya uwepo wa magari ya kunyonya majitaka na ujenzi wa mabwawa yake."

**WATEJA WANASEMAJE?**

Mkazi wa Manispaa ya Sumbawanga, Halima

Wangao, anakiri kuwa mradi huo ni msaada mkubwa baada kuchoshwa na magonjwa ya mlipuko yaliyokuwa yakisababishwa na ukosefu wa majisafi na salama kutokana na matumizi ya maji yasiyo salama.

Anazungumzia pia gharama kubwa za ununuzi wa maji kuwa zimepungua baada ya wakazi wengi kuunganishiwa huduma ya maji na kuanza kulipia ankara za maji kila mwezi ambazo ni nafuu ukilinganisha na bei ya maji iliyofikia Sh. 1,000 kwa dumu.

"Tulikuwa tunapata shida sana wakati wa kutafuta majisafi na salama na wakati mwingine tulishirikiana na mifugo yetu lakini tuna mkombozi," anasema Wanguo.

Salum Mbalamwezi, anasema kuwa awali shida ya maji ilikuwa inasababisha migogoro katika ndoa kwani kinamama walikuwa wanatumia mwanya wa shida ya maji kukosa uaminifu.


**AHADI ZAIDI**

Mbunge wa Sumbawanga Mjini (CCM), Aeshi Hillaly, anasema pamoja na kukamilika kwa mradi huo, serikali imeendelea na mipango iliyopo ya uboreshaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Sumbawanga kwa kufanya jitihada za upanuzi wa mtandao wa majisafi.

"Mtandao wa majisafi umeongezeka kwa kilometa 18 na ununuzi wa dira za maji 1,200 kwa gharama ya Sh. milioni 409. "Utekelezaji wa mradi huu umewanufaisha wakazi wa maeneo ya Kisiwani, Sokolo, Majumba Sita, Kasisiwe, Katai, Muhama na Katusa.," anasema mbunge.

Anawaambia wananchi kuwa Sh. milioni 330 zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa mtandao wa majisafi katika manispaa hiyo na taratibu za ununuzi wa mabomba na viungio zinaendelea. Kukamilika kwa kazi hiyo kutawanufaisha wakazi wa maeneo ya Kashai, Utengule, Energy na Kasisiwe," anaahidi mbunge wao.

## CHEMSHABONGO NA NIPASHE NAMBA (00 18 00)



**Dondoo: Kulia**

1. Mkuu wa msafara wa miguu
6. Nyumba ya wanyama
7. Mkono wa kulia
9. Fanyia mzaha
10. Wekwa wazi
13. Maizika 14. Ago
16. Sherehe 19. Ubwabwa
20. Watu wa Ghana
22. kisimamo 23. Sadiki
24. Huzuia meli isichukuliwe na maji 26. Hutumika kukalia
27. Afrika kusini ya zamani

**Dondoo: Chini**

1. Mtu mwenye tabia ya kutoridhika na mambo ya wengine
2. Sanaa ni mji wake mkuu
3. Maoni 4. Mbwembwe
5. Mtumishi wa kuandika barua
8. Mtungo wa maneno juu ya jambo fulani 11. Kumi mara 2
12. Fanya upesi
14. Mwisho wa dunia
15. Kati ya 17. majani namna ya mpunga lakini huchanua maua namna ya pamba 18. Pigwa butwaa

**Jibu Na: 17**

| | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | S | U | M | B | I | J | I | | | M | | |
| A | | J | | A | | | N | J | A | M | A | |
| M | K | A | L | I | M | A | N | I | | A | | |
| L | | M | | N | | N | A | N | A | S | I | |
| A | L | A | M | A | | G | | A | | A | | K |
| K | | A | | | | A | | M | P | I | N | I |
| A | | | C | H | U | M | V | I | | | | T |
| | | K | | A | | I | | Z | O | N | G | A |
| U | | I | | B | | Z | A | I | D | I | | S |
| M | A | N | Y | A | T | A | | | E | N | D | A |
| B | | Y | | R | | | B | A | M | I | A | |
| U | K | A | R | I | M | U | | | B | | D | |
| A | | A | | | | | D | H | A | R | A | U |

Na Mwandishi Wetu

# 'Wabongo sikieni kiharusi siyo jini'

LICHA ya 'Wabongo' wengi kuamini kuwa kiharusi ni maradhi ya kutupiwa jini, ukweli ni kwamba ni ugonjwa unaotokana na kuathirika mishipa ya damu inayokwenda kwenye ubongo na ile inayopeleka chakula, hewa na virutubisho ubongoni.

Kama kinavyojulikana kwa kitaalamu kama 'stroke' kiharusi kinaelezwa kuwa si ugonjwa wa kuambukizwa kama maradhi mengine yanayosababishwa na vimelea na virusi . Ugonjwa huu umekuwa chanzo cha vifo na ulemavu miongoni mwa watu wengi duniani.

Watalaamu wanasema 'stroke' inatokea pale mishipa ya damu inayopeleka hewa safi, chakula na virutubisho ubongoni inapokuwa imezibwa kutokana na kibonge cha damu kuganda au kuvilia au imepasuka ghafla kutokana na sababu nyingi ikiwamo shinikizo la damu.

Damu ikivilia au mishipa kupasuka chembe hai au seli za sehemu ya ubongo iliyokuwa inapokea chakula na hewa safi kupitia mishipa hiyo zinakufa mara moja.

Tatizo la kiharusi limeripotiwa wiki hii na wataalamu wa mishipa ya fahamu na ubongo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili wanaoeleza kuwa wastani wa wagonjwa watatu hadi watano wa kiharusi hufikishwa hospitalini hapo kila siku.

Akizungumza wakati wa Siku ya Kiharusi Duniani inayofanyika kila mwaka Oktoba 29, Dk. Patience Njenje, anasema maradhi haya yanakuwa tishio kwa Watanzania kwa vile wengi wanaathirika kuanzia vijana, wazee na watoto lakini kibaya zaidi hufika hospitalini wakiwa wamezidiwa tena kwa kuchelewa.

Dokta Patience Njenje, anasema iwapo mgonjwa atafika hospitalini ndani ya saa sita baada ya kupata tatizo anatibiwa na anaweza kuendelea na maisha yake na afya kama ilivyokuwa mwanzo. Hivyo ni vizuri kuwahi.

Watu wengi wanaamini kuwa kiharusi ni ugonjwa wa kurushiwa 'jini' na wanauita 'kipapai' na baadhi hukimbilia kwa waganga wa kienyeji na kuendelea kupata matibabu ya asilia ikiwamo wengine kulishwa dawa ambazo huenda hazina tiba.

**CHANZO**

'Stroke' inasababishwa na kuganda kwa damu inayotengeneza kibonge au kuvilia kwenye mshipa wa damu wakati inapokwenda ubongoni hivyo kuzuia damu nyingine kushindwa kwenda kwa utaratibu.

Wakati mwingine mishipa ya damu inayokwenda ubongoni hupasuka na kuvuruga mtiririko wa damu inayokwenda kwenye ubongo inayobeba chakula, virutubisho na hewa safi.

Aina hii ya kiharusi huitwa 'hemorrhagic stroke,' kwa hutokana na damu. Wataalamu wanasema chanzo hiki kinachangia asilimia 87 ya kiharusi kinachotokea kwa watu wengi.

Chanzo kikubwa cha kupasuka kwa mishipa ya damu ni shinikizo la juu la damu ambalo mara nyingi halijapatiwa tiba.



Wagonjwa wa kiharusi wasikimbilie kwa waganga wa kienyeji. **PICHA MTANDAO.**

Distributed via ippmedia



Damu kuvilia ubongo kama hivi inatajwa kuwa ni chanzo kikubwa cha kiharusi kwa watu wengi. Hali hii ya kupooza upande mmoja siyo kutupiwa jini bali na maradhi ambayo huwapata watu duniani kote. **PICHA: MTANDAO.**

Aina nyingine ya kiharusi hujulikana kitaalamu kama 'transient ischemic attack' au shambulio dogo la kiharusi ambalo linatokana na kuganda kidogo kwa damu ndani ya mishipa ya fahamu na kusababisha kibonge kidogo au kuvilia kiasi kwa damu kwenye mishipa ya damu. Shambulio dogo la kiharusi linaelezwa kuwa linakuwa kama ujumbe wa kukutahadharisha kuwa kuna hatari inakuja mbele ni vyema kuchukua hatua mapema .

Zama hizi watu wengi wanadhani kuwa kiharusi kinatokana na matatizo yanayoanzia moyoni lakini ukweli ni kwamba sivyo. Tatizo linaanzia kichwani au ubongoni.

Wakati mwingine hutokea tatizo la kiharusi ambalo ni kubwa mno linahusishwa na kuathiri mwili mzima. Kawaida watu wanapopata kiharusi eneo au upande mmoja wa mwili huathirika. Inaweza kuwa kulia au kushoto.

Chanzo chake ni kuathirika kwa sehemu kubwa ya ubongo na kusababisha mgonjwa kuwa taabani asiyeweza kufanya chochote kuanzia kuongea , kusogeza kiungo chochote cha mwili au kufanya chochote.

**ATHARI ZA KIHARUSI**

Madhara makubwa ya kiharusi ni kuumiza ubongo kwa vile ubongo ni kama mashine au moyo wa mwili wa binadamu unaosimamia kazi za kila kitu mwilini.

Kwa hiyo kama kiharusi kikitokea sehemu ya mwili iliyokuwa inategemea upande wa ubongo huo ili kufanyakazi zake, haitaweza kutekeleza majukumu yake kama ilivyokuwa kawaida ya mwili.

**KUAMINI WAGANGA**

Tatizo walilonalo Watanzania wengi bila kujali wapo mijini au vijijini ni kuamini kuwa kiharusi ni matokeo ya uchawi kwa hiyo mtu anapopooza upande mmoja , tatizo hilo linatokana na kurogwa au kutupiwa majini. Mara nyingi inaonekana kuwa 'jini' hilo humpata mtu akiwa chooni au bafuni.

Ukanda wa pwani watu huamini kuwa kuna majini vyooni ambayo ndiyo 'yanayomvaa' mtu na kumsababishia kiharusi au kupooza upande mmoja maarufu kupigwa kipapai.

Licha ya kwamba wataalamu wanaeleza kuwa ni ukosefu wa hewa safi na chakula ubongoni unaotokana na damu kuvilia ndani ya mishipa kwa muda au kupasuka kwa mishipa ya damu inayoelekea ubongoni watu wameendelea kuamini kuwa wanarogwa.

Wagonjwa wakipelekwa kwa waganga hao huwatibu waathirika kwa kuwachua kwa mafuta wakati mwingine ya mizeituni au jamii nyingine na kuwafanyisha mazoezi, lakini ikimbukwe kuwa kama kuna damu imevilia au kuganda ubongoni kuchua huko pekee pengine haiwezi kusaidia kumaliza maradhi.

Hii ni kwa sababu huenda mgonjwa anahitaji kufanyiwa upasuaji na kutibiwa eneo lililoathiriwa na kibonge cha damu kilichoganda au kuvilia ubongoni.

Aidha, inawezekana pia damu imevuja ubongoni hivyo kukimbilia kilingeni au kwa mganga anayepiga tunguri si ufumbuzi wa tatizo hilo.

Kwa madaktari wa Tanzania, inahitajika kufanyika utafiti ili kufahamu zaidi kwanini watu wanapata kiharusi wakiwa chooni au bafuni. Kuna uhusiano gani na maradhi hayo?

Japo kuna baadhi ya maelezo kuwa ukiingia chooni wakati wa kuchuchumaa unaweza kuanguka au inawezekana ukijimwagia maji unaweza kusababisha hitilafu kwenye mzunguko wa damu kichwani, bado ni mambo ambayo hayajapata majibu ya kikamilifu watu wanapohusisha tatizo la kiharusi na choo au bafu.

Hata hivyo, taarifa za Muhimbili na maelezo kuwa ugonjwa huu unapona mgonjwa akiwahi hospitalini zitumike kuhamasisha watu kuwahi hospitalini badala ya kukimbilia kwa waganga wa kienyeji.

Hakuna sababu za kuendelea kwenda kwa waganga kilingeni kama unaweza kutibiwa hospitalini.

**UGHALI WA TIBA**

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe wiki hii baada ya kupata maelezo ya Dk. Njenje kuwa kiharusi kinapona iwapo mgonjwa atawahishwa hospitalini umebaini kuwa gharama za vipimo zinaweza kusababisha wagonjwa kuumia zaidi.

Uchunguzi ulibaini kuwa mgonjwa anapofikishwa kwenye huduma za dharura kwenye hospitali za serikali, anatakiwa kulipia taribani 150,000 ili kupokelewa 'emergency'.

Aidha kipimo cha CT Scan kuchunguza athari ubongoni kinaweza kugharamu Sh. 200,000 jambo ambalo si jepesi kwa familia maskini.

Kwa hiyo ili kuokoa maisha ya watu ni vyema gharama za wagonjwa wa kiharusi zikapunguzwa ili kuokoa maisha.

## Rwanda yadaka genge la wadukuzi

**KIGALI,** Rwanda

KIKUNDI cha wadukuzi kutoka mataifa ya Kenya, Uganda na Rwanda kimekamatwa nchini Rwanda kikijaribu kuiibia benki moja ya biashara.

Kikundi cha wadukuzi hao kinachowajumuisha raia kutoka mataifa ya Afrika mashariki kilinaswa nchini Rwanda kilipokuwa kikijaribu kuingilia mifumo ya benki.

Ofisi ya Taifa ya Upelelezi nchini Rwanda (Rwanda Investigation Bureau), ilisema kuwa wadukuzi hao walipanga kuiba pesa kutoka kwenye akaunti ya mteja wa benki ya Equity, lakini haikusema ni lini jaribio hilo lilifanyika.

Aidha, ofisi hiyo ilisema kuwa kikundi cha wadukuzi kinawajumuisha Wakenya wanane, Wanyarwanda watatu na Mganda mmoja.

Benki ya Equity ni moja ya benki kubwa katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati ikiwa na matawi yake katika mataifa ya Kenya, Uganda, Tanzania, Rwanda, Sudan Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo.

Ofisi ya taifa ya upelelezi nchini Rwanda ilisema kuwa awali kikundi hicho cha wadukuaji kilifanikiwa kuingilia mifumo ya benki hiyo katika nchi za Kenya na Uganda.

Mwanzoni mwa mwaka huu Mkurugenzi Mtendaji wa Equity Bank, James Mwangi alinukuliwa akisema kuwa benki hiyo ilikabiliwa na majaribio 14,000 ya udukuzi wa mifumo yake.

Machi 2017, nchini Kenya mwanaume mmoja, alishtakiwa kwa tuhuma za kudukua mfumo wa kifedha wa Mamlaka ya Mapato ya Kenya (KRA).

Udukuzi huo ulidaiwa kusababisha mamlaka hiyo kupoteza Sh. bilioni nne za Kenya takribani dola 39 milioni za Marekani. **BBC**



# Mlimbwende 'aliyebakwa' na Jammeh amkaanga

**BANJUL,** Gambia

MALKIA wa urembo nchini Gambia, amemshutumu rais wa zamani wa taifa hilo Yahya Jammeh kwa 'kumbaka' baada ya kukataa kufunga naye ndoa.

Akitoa ushahidi kwa tume ya maridhiano na ukarabati , mrembo, Fatou Jallow alisema kwamba Jammeh alimnyanyasa kingono katika chumba kimoja ili kumuadhibu.

Tume hiyo ilibuniwa ili kuchunguza madai ya unyanyasaji dhidi ya Jammeh wakati wa kipindi chake cha utawala wa miaka 22. Ushahidi wa Jallow ulikamilisha kikao cha wiki tatu kilichoangazia udhalilishaji wa kingono. Jammeh alitoroka Gambia mwaka 2017 baada ya kukataa kustaafu kufuatia kushindwa kwake katika uchaguzi wa urais.

Kwa sasa anaishi mafichoni nchini Guinea ya Ikweta.

Ushahidi wake ni miongoni mwa ripoti ya shirika la haki za kibinadamu la Human Rights Watch ambayo inaelezea madai mengine ya ubakaji na unyanyasaji wa kingono uliotekelezwa na Jammeh.

BBC ilijaribu kuwasiliana na Jemmeh ambaye kwa sasa anaishi mafichoni Equatorial Guinea, kuhusu madai hayo.

Awali msemaji wa chama chake cha APPR alikana madai hayo yaliyotolewa dhidi ya Jammeh.

**Rais huyo wa zamani hana muda wa kujibu uongo na kampeni za kumuharibia jina. Ni mtu anayemuogopa mungu ambaye anaheshimu sana wanawake wa Gambia.**

"Sisi kama chama na raia wa Gambia tumechoka na murururu wa madai ambayo yameripotiwa dhidi ya rais wa zamani," alisema Ousman Rambo Jatta katika taarifa iliotumwa kwa BBC.

"Rais huyo wa zamani hana muda wa kujibu uongo na kampeni za kumuharibia jina. Ni mtu anayemuogopa mungu ambaye anaheshimu sana wanawake wa Gambia", alisema naibu wa kiongozi wa chama hicho cha APPR.

Awali Jallow aliiambia BBC alitaka kukutana na Jammeh mwenye umri wa miaka 54 mahakamani ili ashtakiwe.

Tume hiyo ya maridhiano na marekebisho inachunguza ukiukaji wa haki za kibinadamu wakati wa utawala wa miaka 22 wa Jammeh, ikiwamo ripoti za mauaji ya kiholela, ukatili na kukamatwa na kuzuiliwa kiholela.

Alilazimishwa kutoka madarakani mnamo mwezi Januari 2017 baada ya mataifa jirani kutuma vikosi vya kijeshi alipokatalia madaraka.

Alieleza kuwa akiwa na umri wa miaka 18 wakati alipokutana na Jammeh baada ya kushinda shindano la malkia wa urembo wa 2014 katika mji mkuu wa Banjul.

Miezi kadhaa baada ya kupata taji hilo, anasema kwamba rais huyo wa zamani alijifanya kama mzazi wakati alipokutana naye akimpatia ushauri, zawadi na fedha na kuandaa maji kupelekwa katika nyumba yao ya familia.

Na katika chakula cha jioni kilichoandaliwa na msaidizi wa rais huyo, anasema alimuuliza iwapo wangeoana. Alikataa wazo hilo mbali na zawadi alizokuwa akipatiwa.

Mrembo Jallow alisema kuwa msaidizi huyo baadaye alisisitiza kwamba anafaa kuhudhuria sherehe ya kidini katika ikulu ya rais kama malkia wa urembo iliyofanywa Juni 2015.

Lakini alipowasili , alipelekwa katika makazi binafsi ya rais huyo."Ilikuwa wazi kile ambacho kingetokea", alisema akitaja hasira ya Jammeh baada ya yeye kukataa kufunga naye ndoa.

Mlimbwende alisema alipigwa kofi na kudungwa sindano mkono mwake. alifuta sehemu zake za siri usoni mwangu, akanisukuma nipige magoti na kunifanyia vibaya" alisema kwa uchungu. **BBC**

Distributed via ippmedia



Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ujasusi, Adam Schiff. **PICHA: DW**

# Ikulu yalikosoa bunge kumchunguza Rais Trump

**WASHINGTON,** Marekani

IKULU ya Marekani imesema hatua ya bunge la nchi hiyo kuidhinisha azimio la uchunguzi dhidi ya Rais Donald Trump, unaokusudia kumuondoa madarakani haukuzingatia haki na kwamba ni kinyume cha katiba.

Akizungumza muda mfupi baada ya azimio hilo kupitishwa, msemaji wa Ikulu ya Marekani, Stephanie Grisham, alisema Trump hajafanya chochote kibaya na kwamba kitendo cha wanachama wa Democratic ni ukiukaji katiba usiokubalika.

Kwa upande wake, Meneja wa Kampeni wa Rais Trump, Brad Parscale, alisema wapiga kura watawaadhibu wanachama wa Democratic wanaounga mkono suala hilo na kwamba kiongozi huyo wa Marekani atachaguliwa tena kwa urahisi.

Alhamisi wiki hii, Bunge la Marekani lilipitisha azimio hilo kwa kura 232 dhidi ya 196, huku wabunge wote wa Chama cha Republican wakilipinga, wakiungwa mkono na wabunge wawili wa chama cha Democratic.

Azimio hilo linafungua njia ya sheria za msingi za kumchunguza Rais na siyo kura ya kuamua iwapo wamchunguze rais au lah.

Huo ni ushindi kwa chama cha Democratic ambacho ndicho kinachodhibiti uchunguzi huo katika bunge.

Uchunguzi huo utaangazia iwapo Trump aliishinikiza Ukraine kwa kuweka masharti ili iweze kumchunguza mpinzani wake kisiasa Joe Biden pamoja na mtoto wake wa kiume Hunter.

Ofisa wa zamani wa ngazi ya juu wa Ikulu ya Marekani, Tim Morrison , alithibitisha kuwa msaada wa kijeshi ulizuiwa na Trump kama sharti la kuitaka Ukraine ambayo ni mshirika wake kumchunguza Biden, lakini alithibitisha kwa mtazamo wake kuwa haikuwa kinyume cha sheria.

Baada ya kura hiyo, Trump aliandika kwenye ukurasa wake wa Twitter akisema hiyo "ni kampeni mbaya na kubwa dhidi yake katika historia ya Marekani.'

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kijasusi, Adam Schiff, alisema iwapo Rais atatumia vibaya ofisi yake na kushindwa kuitetea katiba kutokana na ajenda binafsi au za kisiasa waanzilishi wa nchi hiyo waliweka utaratibu wa suluhisho ambao ni kuchunguzwa.

Kiongozi wa walio wachache bungeni, Kevin McCarthy, alisema wa Democrats wanatumia vibaya madaraka yao na wanaichafua demokrasia kwa kujaribu kumuondoa madarakani rais, kwa sababu wanaogopa hawawezi kupambana naye katika sanduku la kura. **DW**

# HADITHI

WASWAHILI wana msemo wao unaosema kuwa ufukara ni jereha la ulimwengu. Wakiwa na maana, mtu fukara mara nyingi hukutana na mitihani mikubwa duniani, ambayo mingi husababishwa na baadhi ya binadamu wengine wenye vipato kwa kuwaona hawana thamani na hawahitajiki kuwa na kitu chochote cha thamani.

Kijana anayetoka kwenye familia duni Kadili, anatokea kupendwa na msichana mrembo anayetoka kwenye familia ya kitajiri, Edina. Lakini kitendo hicho kinamsababishia kijana huyo matatizo makubwa ambayo hajawahi kuyapata katika maisha yake, kiasi cha maisha yake kuwa hatarini. Fuatilia mkasa huu wa aina yake.

# JUMBA JEKUNDU- 25

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

**Na Adam Fungamwango**

KWA upande mwingine kifo cha Pauline kinaweza kuwa ni chanzo cha misukosuko kwake na kuonekana kwa familia ya mama huyo kuwa huenda yeye ndiye aliyesababisha hayo. Hili halikumuondoka kichwani.

Kama alikamatwa na kupelekwa kwenye jumba jekundu la hayati mama Pauline na kuteswa, akateseka kwa kitu ambacho hakukifanya na hakipo, familia haiwezi kushindwa kudhani kuwa anahusika.

Kitu kingine kilichomuuliza ni kujua alipo Edina. "Yuko wapi?" Alichokuwa na uhakika ni kwamba Edina atakuwa amemtoroka mume kwa sababu aliozwa bila ridhaa yake. Aliozwa kwa nguvu tu na mama yake na hakuwa anampenda mume huyo. Mama alitaka tu binti yake aolewe na mtu tajiri, mwenye uwezo, msomi au vyote kwa pamoja, lakini si mtu fukara ili mradi tu mwenyewe binti amependa.

"Amekimbilia wapi? Anaishi kwa nani?" Hili ni swali lililomtesa moyoni mwake.

"Inawezekana Edina ana mwanaume ambaye anampenda na ametorokea huko anaishi kwake?" Aliwaza na kujiuliza mwenyewe. Kwa mbali wivu ulianza kumuingia.

Yoyote atakayekuwa mpenzi wa Edina atakuwa mtu mwenye maarifa sana, akisaidiwa na binti huyo kwani yeye hajulikani kwao na hata marehemu Madame Pauline hakujua chochote kuhusu mtu huyo na badala yake yeye Kadili ndiye mtu wa kusukumiwa mzigo kuwa ndiye anayemharibu Edina wakati si kweli.

Pamoja na yote hayo, wazo la kwenda Oysterbay kwenye msiba halikuja kabisa. Alijua akitia pua yake tu, anawezwa kubebwa msobemsobe ama na madausa au na polisi kwa kusababisha kifo cha mama hiyo, kwani huenda wakajua kuwa Edina anaweza kuwa alitorokea kwake.

Pia hakuwa na uhakika kuwa binti huyo atakuwepo msibani kwani taarifa inasema kuwa tangu atoroke kwa mumewe hajaonekana. Ina maana hata nyumbani kwao hakwenda ndiyo maana mama yake akapatwa na mshtuko, hivyo hana uhakika kama atakuwepo kwenye msiba, au atasubiri kwanza sakata liishe ndipo arudi nyumbani kwani kwa msiba huu, Edina ana hatia ya kusababasha umauti wa mama yake, ingawa hawezi kukamatwa na polisi, lakini machoni mwa waombolezaji, ndugu na jamaa ataonekana ni 'muuaji' aliyesababisha kifo cha mama yake bila kukusudia.

Maswali yamekuwa ni mengi kwake kuliko majibu. Kadili alionekana kutatizwa na mambo mengi yaliyompata tangu alipokamatwa na kupelekwa kwenye jengo hile, mateso aliyoyapata, alipotoka, kuolewa kwa Edina, kutoroka kwa mumewe hadi kifo cha mama Pauline, lakini hakuwa na mtu wa kumuuliza.




**Taratibu kioo kilishuka chini kwa madaha. Ni kama vile aliona macho yake alimdanganya. "Ni yeye kweli?" Asema lakini si kwa sauti. "Pita upande wa pili upande ndani ya gari." Sauti ya aliyekuwa anaendesha gari ilimwambia kwa utulivu.**

Aliyakumbuka maneno ya kifedhuli ya marehemu mama Pauline, lakini pia na baadhi ya yale yaliyomburudisha.

Kuna kitu kimoja tu ambacho kilimpa faraja.

"Nisikilize kwa makini. Leo nakusamehe kwa sababu binti yangu Edina amelia sana kwa sababu yako ili usiuawe. Saa hizi tayari ungekuwa umeshawasili kuzimu. Yoyote anayeingia kwenye jumba hili kwa sababu kama zako, au zingine za utovu wa nidhamu huwa hatoki salama. Nadhani ulitembezwa kwenye yale makaburi ya wajinga wenzako. Kuanzia leo sitaki umfuatilie tena mwanangu. Umuogope kama ukoma. Sitaki kusikia habari zako tena hapa. Nikisikia chochote kile juu yako na binti yangu, au kutoa siri ya hiki kilichomo kwenye nyumba hii, basi tusilaumiane. Kwa sababu ni lazima uuawe." Yalikuwa ni maneno ya Mama Paulime siku za nyuma alipokamatwa na kupelekwa kwenye jumba lake Oysterbay.

Faraja ya maneno hayo ni kwamba kumbe Edina ndiye aliyesababisha yeye kutoka hai mle ndani kwa sababu hakuna binadamu yoyote anayeingia mle na kutoka. Edina alilia kwa ajili yake ili asiuawe. Na kweli hakuuawa, akachiwa.

Hii ilimfanya Kadili apate wazo moja tu. Baada ya mazishi kupita, amsake Edina popote pale, hata kama atakuwa na mwanaume mwingine haidhuru, lakini akiwa na nia ya kupata ukweli au ufafanuzi ya mambo yote yale yaliyotokea na kumuumiza kichwa. Kwa nini yalitokea. Na mwisho alitaka kujua hadi siri ya kifo cha mama Pauline.

***************************************

Mwezi mmoja ulipita. Kila kitu kilirudi kwenye hali yake ya kawaida. Kila mmoja alirejea kwenye shughuli zake. Kadili alianza kusahau kila kitu kuhusu mambo yote yaliyotokea. Akili yake sasa ilianza kumuwaza Eliza.

Akakumbuka maneno aliyoambiwa na mama yake.

"Nilikwambia mwanangu, yule msichana ni mtoto wa kitajiri huwezi kumpata.

Wiki iliyopita nilikwenda Mtoni Mtongani kwa mjomba wako Polly. Katika maongezi tuliyoongea ni kwamba tumekubaliana wewe umuoe binti yake Eliza."

Habari hiyo mpya ilimshtua Kadili. Anamfahamu Eliza. Ni ndugu yake. Ni mpwa wake. Binti ya mjomba wake aliyezaliwa na mama yake. Ni msichana mrembo na anafaa kuwa mke.

"Mbona Eliza ni mzuri tu, tena huyu ni mtu wetu wa karibu, hatokuumiza kijana wangu." Akakumbuka siku mama yake alipomkalisha chini na kumuelezea habari hizo.

Akiwa maeneo ya Tandale Yemen, anavuka barabara kuu ya Tandale, itokayo Magomeni kupitia Kwa Mtogole kwenda Sinza Kijiweni, alimuona mtoto mmoja akimfuata mbio hadi alipomfikia.

"Kaka unaitwa pale kwenye gari ile." Yalikuwa ni maneno mafupi ya mtoto huyo wa kiume, akimuonyesha Kadili gari moja aina ya Toyota Crown lililokuwa limesimama mita kadhaa pembeni kabisa mwa barabara.

Ilikuwa nje ya saluni moja ya kiume ambayo kuna wakati huwa anakwenda kunyoa.

Kama mtu yoyote ambaye amepitia matatizo siku za karibuni, wito ule ulimshtua. Akili yake ikarudi nyuma kwa kuona kabisa kuwa yale matatizo ya kupotea kwa Edina na kifo cha mama Pauline huenda bado hayajaisha.

Kwanza kabisa alidhani kuwa gari ile inawezekana ikawa ya polisi wamekuja kumchukua kama alivyokuwa akijitabiria huko myuma.

Lakini mawazo mengine yakamjia kuwa huenda ni mabaunsa wa mama Pauline ambao wamekuja kumchukua kama walivyofanya huko nyuma.

Akikumbuka mateso makali aliyoyapata kwenye jumba jekundu chini ya usimamizi wa marehemu Mama Pauline, hakutaka kabisa yarudie kwenye mwili wake. Wazo la haraka haraka lilimtuma atimue mbio.

Kabla hajafanya chochote alijiuliza kama mbio itakuwa ni kutatua tatizo la kudumu au la muda.

Mwisho kabisa hakudhani kuwa kukimbia ni suluhisho. "Nikimbia kama ni polisi basi nitakuwa nimeahirisha tu tatizo, hata baada ya miaka 10, nikikamatwa bambo yatakuwa pale pale. Kama ni mabaunsa, hawa wanapafahamu hata nyumbani na walishawahi kuja na kugonga mlango, hivyo kuwakimbia ni kazi bure, kwani wanaweza kuja hata usiku wa manane." Alijiambia.

Kwa hatua za kunyata, alilisogelea gari lile taratibu ili kujua mtu anayemwita. Lilikuwa na vioo ambavyo watoto wa mjini wanavyiita 'tintedi'. Yaani havimuonyeshi mtu akiwa ndani. Na vilikuwa vimefungwa.

Moyo ulikuwa unamuenda mbio, asijue afanye nini. Alijikuta akisimama kwenye mlango wa mbele wa yoyote aliyekuwa anaendesha gari hilo.

Taratibu kioo kilishuka chini kwa madaha. Ni kama vile aliona macho yake alimdanganya. "Ni yeye kweli?" Asema lakini si kwa sauti. "Pita upande wa pili upande ndani ya gari." Sauti ya aliyekuwa anaendesha gari ilimwambia kwa utulivu.

"Hakuna mtu mwingine ndani ya gari?" Kadili alijikuta akiropoka." Kicheko mwanana kilifuatia.

"Kadili umeanza kuwa mwoga siku hizi, hakuna mtu yoyote, njoo upande mara moja."

Kwa asilimia nyingi Kadili alimuamini dereva huyo. Hakuna mwingine ila ni Edina.

Alionekana kuendelea kuwa mrembo zaidi. Kadiri aliushangaa uzuri wa asili wa msichana huyo kwani kutokana na matatizo yote ambayo ameyasikia juu yake, kumtoroka mumewe, kukaa kusikojulikana na kufiwa na mama yake, bado hakuonekana kama amedhohofika au kusawijika kama alivyotarajia kuwa anaweza kuwa. Ndiyo kwanza aliendelea kunawiri wakati mwingine ni zaidi ya alivyokuwa akimuona miaka michache iliyopita 'Blue Hotel' walipokuwa akicheza disco.

"Umepajuaji hapa Edina." Lilikuwa ni swali la kwanza la Kadili baada ya kuketi kwenye gari.

Edina alirejea kicheko chake kama cha awali. "Hukumbuki kuwa ulishawahi kuniambia unaishi Tandale?"

"Unaitwa nani?"

"Kadili."

**Itaendelea Jumamosi**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MCHANGANYIKO

**LAND CRUISER INAUZWA TOYOTA LANDCRUISER VX AMAZON, DIESEL, AUTOMATIC, INATEMBEA IPO KWENYE HALI NZURI. TSHS 24.5 Milioni. 0719 774 474.**

2 ACRE YARD FOR RENT

Facing New Julius Nyerere International Airport. Call: +255 754 375 967. Email: gold@goldtz.net

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZWA**

Shamba la Ekari 13 linauzwa liko Mlandizi barabara iendayo Bagamoyo, lina miti ya matunda inayozaa, lina umeme. Lina maji ya DAWASCO na maji ni matamu. Pia kuna kisima kirefu. Kwa mawasiliano piga simu namba 0655 099825 / 0767 237404 / 0715 237404.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BID-


## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI PIKIPIKI

**RAMADHANI WILSON MAGOMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BOXER** yenye namba za usajili **MC 499 APF** Chassis namba **MD2A21BZ7DWE26574** **Engine no PFZWDE15263.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **TAN/TAN/RB/403645/2019.**

115496702

JAMHURI YA MUUNGANO WA TA NZANIA
KA TIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILA YA YA DODOMA
MAHALI DODOMA
MA OMBI NA. 204 YA 2019 BAINA YA
GIDION AY UB SENY AG WA …..MKAZA HUKUM U
DHIDI YA

RAJABU KUNDULU
MUSA MWANYIKA
MOSES MANYONO
ALOYCE NGONDA
EVANCE LYIMO……WAKAZIWA HUKUMU
MASE MWANYIKA
VINI CHISATU
MUGUSHA BASILISA
BRAISON ZAMANI
MAONEZI FUMBI
CHINO CHIGAHE
KWA: RAJABU KUNDULU
MUSA MWANYIKA
MOSES MANYONO
ALOYCE NGONDA
EVANCE LYIMO……WAKAZIWA HUKUMU
MASE MWANYIKA
VINI CHISATU
MUGUSHA BASILISA
BRAISON ZAMANI
MAONEZI FUMBI
CHINO CHIGAHE
KWA:
YAH: KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake maelezo yake yameelezwa katiak nakala ya maombi ambayo inapatikana katika baraza hili.

Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika baraza hii wewe binfsi,wakili au mwakilishi yeyote ambaye anahusiwa kisheria tareh 5/11/2019 saa 3;00 asubuhi kwa mujibu wa maombi hayo mntakiwa kuleta uetetzi wenu kwa maandishi.

Anglizo: kama hamkuhudhua taehe iliyotajwa hapo juu, Baraza likithibitisha kuwa mmepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yenu.

Hati hii imetolewa kwa am yangu na lakiri/muhuri wa Baraza hili leo 01/11/2019.

H.E. Mwihava,
MWENYEKITI,
Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya,
DODOMA.

115496802

## SUNDI (T) LIMITED

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**Kwa idhini tuliopewa na Akiba Commercial Bank PLC tunauza kwa mnada wa hadhara nyumba nane(8) za wadaiwa sugu**

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANI NA MAHALI ILIPO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 008 | ASIA TIMOTHY KITUMBUKA | ASIA T. KITUMBUKA | NYUMBA IPO KILUNGULE - MKURANGA | 28/11/2019 SAA 4:00 |

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo
2. mnunuzi atatakiwa kulipa asilimia 20% siku hiyo ya mnada ya bei iliyofikiwa
3. Malipo ya asilimia 75%yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote ukishidwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona,kukagua,kuhamisha umiliki, na zingine zitamuhusu mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NASI KUPITIA ANUANI**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**SUNDI (T) LIMITED**
**P.O BOX 40057**
**DAR ES SALAAM**
**0715549782 AU 0713893706.**

15496402

## KUPOTELEWA NA KADI ZA PIKIPIKI

MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD anatangaza kupotelewa na kadi za Pikipiki zenye namba za usajili MC 125CFD, MC180CFD, MC618CFJ, MC919CFJ, MC393CGA, MC545CEW, MC962CFF, MC314CFD, MC314CFD, MC456CGP, MC MC484CGP, MC720CGD, MC817CHF, MC642CFA, MC646CFA, MC208CFF.

Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/CEN/RB/432575/2019.

154961


## KUPOTEA KWA CHETI



**HIDAYA ATHUMAN HASSAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0215/034 kilichotolewa na MTWARA GIRLS mwaka 1990.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: MS/RB/2750/2019.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMILY MARTIN MASSAY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0168/010 kilichotolewa na SANU SEMINARY mwaka 1989.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **NDN/RB/273/2010.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Moses Wazuri Urio** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Fuso Mitsubish yenye namba za usajili na. T137 BCX Chassis namba FK417KZ750005. Engine namba 6D1770172. .

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/428398/2019**

115495802

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. OF 2019
Distributed via ippmedia
In the matter of the Estate of the late IBRAHIM TITO KIVIKE DODMA MUNICIPALITY
And
In the matter of the Application for letters of Administration by TITUS SAGENI KAVIKE

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN. 369 Of 1963)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate or letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 14TH day of Aug 2019.

The will of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Date at Dodoma this 31st day of July 2019

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE BODOMA REGION

115495602

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. OF 2019**
**In the matter of the Estate of the LATE HILDA MKWAWI BWANAMZURI**
**And**
**In the matter of the Application for letters of Administration by ANTHONY CHALO BWANAMZURI**

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate or letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before **20TH day of November, 2019.**

The will of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Date at Dodoma this 30th day of Oct 2019

Resident Magistrate
DODOMA

115495702


Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# POCHETTINO AZIDI KUNUKIA BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

KLABU ya Beyern Munich imeripotiwa kwamba inamtaka Mauricio Pochettino kwenda kumbadili Niko Kovac kwenye kikosi hicho cha mabingwa wa Bundesliga.

Pochettino amekuwa hana uhakika wa maisha marefu kwenye kikosi cha Tottenham Hotspur baada ya timu hiyo kuwa na mwenendo wa ovyo kwenye Ligi Kuu England na michuano mingine.

Kwa mujibu wa Sport1, kocha huyo Muargenntina ameanza kuwavutia mabingwa hao wa Ujerumani. Pochettino mwenyewe amekiri kwa mara ya kwanza kwamba kibarua chake kipo kwenye mashaka makubwa, lakini amegoma kuishi kwenye hofu zaidi.

Spurs wameachwa pointi nane kuifikia Top Four baada ya kukusanya pointi 12 katika mechi 10 za kwanza kwenye Ligi Kuu England. Wachezaji wa timu hiyo wanasema bado wanapambana kwa ajili ya kocha wao, ambapo Dele Alli alisema: "Kwa asilimia 1,000 tunamsapoti kocha." Pochettino amesifiwa kutokana na kuibadili Spurs.

Distributed via ippmedia

# Guardiola chali makocha bora

**LONDON,** England

PEP Guardiola amepigwa chini kwenye orodha ya makocha watano wanaowekwa kuwania tuzo ya Kocha Bora wa Mwaka licha ya Mhispaniola huyo kubeba mataji matatu ya ligi ya ndani huko England msimu uliopita.


Kocha huyo wa Manchester City aliiongoza timu hiyo kutetea ubingwa wa Ligi Kuu England na kisha kubeba mataji mengine, Kombe la FA na la Ligi, ikinyakua yote ya ligi za ndani.

Lakini, licha ya kutajwa kama mmoja wa makocha bora kabisa duniani, Guardiola hakuonekana kama anastahili kuwekwa kwenye ushindi wa tuzo za ubora duniani za Globe Soccer Awards.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp aliyekosa kidogo kubeba Ligi Kuu England msimu uliopita, lakini akaiongoza timu hiyo kubeba Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu 2005, amewekwa kwenye orodha hiyo.

Makocha wengine waliopo kwenye orodha hiyo ya kushindania tuzo ni Massimiliano Allegri, Erik ten Hag, Djamel Belmadi na Fernando Santos.

Allegri alishinda mataji matano mfululizo ya Serie A akiwa na Juventus kabla ya kuachana na timu hiyo mwishoni mwa msimu uliopita, wakati Ten Hag aliiongoza Ajax kushinda taji la Eredivisie na kuifikisha timu hiyo nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.





# *Mourinho kuandikia rekodi Arsenal*

**LONDON,** England

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho amewaambia rafiki zake anataka kuwa kocha wa kwanza England kuchukua ubingwa wa England na Ulaya na klabu tofauti.

Hilo linaweza kuinufaisha Arsenal ambayo imetabiriwa inaweza kuanza mchakato wa kutafuta kocha mpya muda si mrefu kuanzia sasa kama kocha wao Unai Emery ataendelea na mwendo wa kusuasua klabuni hapo.

Mourinho amekuwa hana kazi tangu alipotimuliwa na Manchester United Desemba mwaka jana baada ya matokeo mabovu pamoja na uhusiano yake mbovu na wachezaji na nafasi yake ilichukuliwa na kocha wa sasa, Ole Gunnar Solskjaer.

Kuanzia hapo amegomea kazi nyingi zilizoletwa mezani kwake na inadaiwa klabu za Sporting Lisbon, Borussia Dortmund na Lyon ya Ufaransa ziliweka ofa mezani kwake lakini akaona hazina hadhi ya kwake kwenda kufundisha.

April mwaka huu, Mourinho pia alikataa kazi ya ukocha katika klabu tajiri ya Guangzhou Evergrande ya China ambayo ilimpa mkataba wa Euro milioni 100 ambao ungemfanya kuwa kocha anayelipwa pesa nyingi zaidi katika historia ya soka duniani.

Inaaminika kwamba lengo la Mourinho ni kuendelea kubakia katika Ligi Kuu ya England na kuacha rekodi isiyofutika kwa urahisi huku mpaka sasa kukiwa hakuna kocha ambaye amewahi kutwaa mataji matatu ya Ligi au Ulaya ak-

## HABARI MICHEZO

# Klopp amtaka Werner Liver

**LIVERPOOL** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp anapanga kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Timo Werner, kwa mujibu wa ESPN.

Klopp ameripotiwa kwamba, anataka kumsajili mchezaji huyo wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari ili kuimarisha safu yake ya ushambuliaji.

Hata hivyo, Liverpool inaangalia zaidi uwezekano wa kumchukua staa huyo na kumuacha klabuni hapo kwa mkopo mpaka mwishoni mwa msimu huu, lakini italazimika kupambana na Bayern Munich na Manchester United ambayo pia inamsaka kwa nguvu staa huyo.

United imekuwa na tatizo la ufungaji mabao na Werner anaonekana kuendelea kuwa kwenye kiwango cha juu zaidi msimu huu baada ya kufunga mabao 10 na kupika matatu katika mechi 14 alizocheza kwenye michuano mbalimbali.

Mbali na kuwa na Sadio Mane, Mohamed Salah na Firmino kwenye safu yake ya ushambuliaji, Liverpool imekuwa ikipata shida pindi mmoja kati ya mastaa wake hao anapopata majeraha na kutokuwapo uwanjani





# TUCHEL AMTAKA CAVANI APIGANIE NAMBA PSG

**PARIS,** Ufaransa

THOMAS Tuchel amempa changamoto Edinson Cavani kujipanga na kupigania namba kwenye kikosi cha kwanza cha Paris Saint-Germain.

PSG imefunga mabao 17 kwenye mechi zake nne zilizopita za mashindano yote, huku mshambuliaji Cavani akiwa na wakati mgumu wa kupigania namba kwenye kikosi cha kwanza.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, aliangalia mechi za ushindi dhidi ya Nice na Club Brugge akiwa benchi na alicheza kwa dakika 19 tu wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Marseille, ikiwa ni mara ya kwanza kucheza tangu alipopona majeraha yake.

Mauro Icardi sasa ndiye amekuwa kama mbadala wake kwenye kikosi cha kwanza na haitakuwa kazi rahisi kwa Cavani, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

"Hana furaha kwa sababu alikuwa majeruhi na pia hakuweza kutusaidia," alisema Tuchel.

"Ni kitu cha kawaida. Anataka kutusaidia na tunamhitaji, lakini anatakiwa kupigania namba kwenye kikosi cha kwanza kama mchezaji mwingine yeyote. Ni ngumu kwa sababu timu ilifanya vizuri wakati yeye hakuwapo.

"Nafasi yake imebadilika kwa kiasi kikubwa, najua kwamba, anataka kuonyesha mchango wake."

# *Xhaka aomba radhi, aelezea*

**LONDON,** England

NAHODHA wa Arsenal, Granit Xhaka ameelezea namna "alivyochemka" kwenye mchezo dhidi ya Crystal Palace baada ya kushutumiwa mno kwenye mtandao pamoja na kutishiwa kifo.

Xhaka alionyesha ishara ya kushika masikio kwa kuwaambia mashabiki waliokuwa wanamzomea kwamba, hasikii, wakati timu yake ikitoka sare ya kufungana mabao 2-2 kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu, halafu alivua jezi wakati akiingia kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

Kocha, Unai Emery alisema Jumanne kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, anatakiwa kuomba radhi kwa mashabiki kwa kitendo chake hicho, huku wachezaji wa zamani wa Arsenal wakitaka avuliwe unahodha.

Katika taarifa yake ya Jumanne kwenye twitter ya Arsenal, Xhaka aliomba radhi kwa kitendo hicho na kusema kwamba, alishutumiwa na kutishiwa kuuawa.


"Baada ya kukaa kwa muda na kuangalia kile kilichotokea Jumapili mchana, napenda kutoa maelezo yangu," alisema. "Tukio lile lilitokea wakati mimi nikitolewa nje na limeniumiza kwa kiasi kikubwa. Mara zote naipenda klabu na najitokea kwa asilimia 100 nikiwa uwanjani.

"Hisia zangu hazikueleweka kwa mashabiki na walirudia kunishambulia kwa kuandika ujumbe wa kunitishia maisha kwa kipindi cha miezi kadhaa, lakini kubwa ni kwamba naomba radhi.

"Watu waliandika vitu kama: 'tutakuvunja miguu yako', 'tutamuua mke wako na ikiwezekana hata mtoto wako wa kike'.

"Hilo kwa kiasi kikubwa lilinitisha mimi na kuniacha kwenye wakati mgumu zaidi na hasira zinakifanya nifanye vile Jumapili.

Xhaka hakuwa kwenye kikosi cha Arsenal kwenye mchezo wa Jumatano wa Kombe la Ligi ['EFL Cup'] dhidi ya Liverpool ambao walitolewa kwa changamoto ya mikwaju ya penalti baada ya matokeo ya mabao 5-5 katika muda wa kawaida.



## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



Distributed via ippmedia

# MESSI AREJEA ARGENTINA KUIVAA BRAZIL, URUGUAY

### Icardi, Di Maria watoswa wakati mshambuliaji kinda wa Arsenal, Martinez akijumuishwa...

**BUENOS AIRES,** Argentina

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Lionel Messi amerejea katika kikosi cha timu ya Taifa ya Argentina kwa ajili ya mechi ya kirafiki dhidi ya Brazil na Uruguay baada ya kumaliza kutumikia adhabu yake ya kufungiwa kwa miezi mitatu.

**Messi alifungiwa Agosti mwaka huu na Shirikisho la Soka la Amerika Kusini (CONMEBOL) na kisha kupigwa faini ya dola 50,000 kwa kutuhumu chombo hicho kuwapo mkono wa rushwa kufuatia timu yao kupoteza mchezo wa nusu fainali dhidi ya Brazil kwenye Copa America.**

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 32, amekosa mechi nne zilizopita za Argentina - zote zikiwa za kirafiki, lakini sasa yupo katika mstari wa kurejea mwezi huu baada ya kutajwa katika kikosi cha sasa cha wachezaji 26 cha kocha Lionel Scaloni.

Straika wa Manchester City, Sergio Aguero pia amejumuishwa kwa mara ya kwanza tangu Argentina inayoshika nafasi ya tatu kushinda 2-1 mechi ya mchujo dhidi ya Chile kwenye Copa America, wakati kiungo wa Tottenham, Giovani Lo Celso akirejea baada ya kuwa nje mwezi uliopita wakati wakitoka sare na Ujerumani na wakishinda dhidi ya Ecuador.

Bado hakuna nafasi katika kikosi hicho kwa mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Mauro Icardi, ingawa alitimiza kuichezea timu hiyo mechi nyingi zaidi walipocheza dhidi ya Mexico Novemba 2018, lakini mshambuliaji kinda wa Arsenal, Emiliano Martinez akijumuishwa.

Mchezaji mwenza wa Icardi hapo PSG, Angel Di Maria, ambaye hajaichezea timu hiyo tangu michuano ya Copa America, pia hajajumuishwa tena.

Argentina itakutana na Brazil mjini Riyadh, Saudi Arabia, Novemba 15, mwaka huu na kisha kusafiri hadi Tel Aviv, Israel, kuivaa Uruguay siku tatu baadaye tarehe ya mwisho wa kalenda ya mwaka ya mapumziko ya mechi za kimataifa.

Kikosi cha Argentina kilichoitwa kwa ajili mechi hizo za kirafiki na klabu wanazozichezea zikiwa kwenye mabano ni: Agustin Marchesin (Porto), Emiliano Martinez (Arsenal), Esteban Andrada (Boca Juniors), Juan Musso (Udinese); German Pezzella (Fiorentina), Juan Foyth (Tottenham), Marcos Rojo (Manchester United), Nehuen Perez (Famalicao) na Nicolas Otamendi kutoka Manchester City.

Wengine ni Nicolas Tagliafico (Ajax), Renzo Saravia (Porto), Walter Kannemann (Gremio); Giovani Lo Celso (Tottenham), Guido Rodriguez (Club America), Leandro Paredes (Paris Saint-Germain), Lucas Ocampos (Sevilla), Marcos Acuna (Sporting CP) na Nicolas Dominguez anayeichezea Velez Sarsfield.

Kadhalika, wamo Roberto Pereyra (Watford), Rodrigo de Paul (Udinese); Lautaro Martinez (Inter), Lionel Messi (Barcelona), Lucas Alario (Bayer Leverkusen), Nicolas Gonzalez (Stuttgart), Paulo Dybala (Juventus) na Sergio Aguero anayekipiga Manchester City.

## ZISIKUPITE

### MANCITY YAMTAKA COMAN

MANCHESTER City ni miongoni mwa klabu zinazomfuatilia mshambuliaji wa Steaua Bucharest, Mromania Florinel Coman, 21. ***(Mail)***

### MARTINEZ AIVUTIA UNITED

MANCHESTER United inavutiwa na mshambuliaji wa Inter Milan, 22, Muargentina Lautaro Martinez - straika huyo anaweza kuwagharimu pauni milioni 95.6. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### YANOGEWA NA SMALLING

ROMA inataka kukamilisha kumsajili jumla beki wa kati wa England, Chris Smalling kwa pauni milioni 18. Beki huyo wa Manchester United mwenye umri wa miaka 29 anaichezea miamba hiyo ya Serie A kwa mkopo wa muda mrefu. ***(Corriere dello Sport - in Italian)***

### LIVERPOOL KUUNDA TIMU 2

LIVERPOOL inazingatia uwezekano wa kuwa na timu mbili siku moja kushiriki robo fainali ya Kombe la Ligi ['Carabao Cup'] dhidi ya Aston Villa na nyingine nusu fainali ya Klabu Bingwa Dunia . ***(Mirror)***

### 'CAVANI HANA FURAHA PSG'

EDINSON Cavani si mwenye " furaha" iliyokamilika, amesema kocha wa Paris St-Germain, Thomas Tuchel, kufuatia mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kutoanza tangu arejee akitokea chumba cha majeruhi. ***(Le Parisien - in French)***

### YAMFUATILIA ONYANGO

EVERTON haraka imeanza kufuatilia maendeleo ya kiungo English U-16, Tyler Onyango. ***(Liverpool Echo)***

### MASENETA KUJADILI PENALT

MASENETA wawili wa Italia wamesema wataleta mjadala katika kikao chao cha maseneta ili kuwahakikishia mashabiki wa Serie A "kutokuwa na usawa" kufuatia maamuzi mawili ya penalti ya utata katika mechi ikati ya Napoli na Juventus. ***(ESPN)***

### BREWSTER AWINDWA PALACE

CRYSTAL Palace ni miongoni mwa timu zinazovutiwa kumsajili kwa mkopo msimu huu, mshambuliaji wa Liverpool na England U-21, Rhian Brewster, 19. ***(Sun)***

### INTER YAMMULIKA DARMIAN

INTER Milan imetupia jicho lake kwa beki wa kulia wa Parma, Mtaliano Matteo Darmian, 29. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### CARROLL KUANZA NA W. HAM

MSHAMBULIAJI wa Newcastle, Andy Carroll, 30, anajiandaa kucheza dhidi ya klabu yake ya zamani West Ham baada ya kurudi kujifua akitoka kuuguza majeraha yake ya nyonga. ***(Newcastle Chronicle)***

### PALACE KUPANUA AKADEMI

CRYSTAL Palace imeanika mpango wake wa kutumia pauni milioni 15-hadi 20 kwa ajili ya kuendeleza akademi yao ambayo itawafanya kuwa klabu ya kwanza Kusini mwa London yenye hadhi kubwa. ***(Evening Standard)***

## TFF, ZFF sasa kujifungia J'5

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HATIMAYE uongozi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), na ule wa Zanzibar (ZFF), unatarajia kukutana Jumatano ijayo ili kujadili masuala mbalimbali yaliyojitokeza kati yao hususan mgawo wa fedha kutoka Shirikisho la Soka duniani, Fifa.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini Zanzibar, Katibu wa ZFF, Mohmed Ali Hilali, alisema mkutano huo utalenga kuyapatia ufumbuzi madai yao kwa TFF na kutafuta ufumbuzi wa kudumu ambao hautaathiri maendeleo ya soka kwa pande zote mbili.

Alisema mada kuu tano zitazungumzwa katika mkutano huo huku ya kwanza ikiwa ni fedha za ruzuku zinazotoka Fifa kupitia TFF, timu ya Taifa ya Zanzibar, ushirikishwaji wa timu ya Taifa ya Tanzania, ushirikiano baina ya TFF na ZFF pamoja na utekelezaji wa suala la fedha za wachezaji waliohamia klabu za Tanzania Bara wakitokea zile za Zanzibar.

Aidha, alisema ripoti za mikutano yote miwili itawasilishwa kwa marais wote wawili yaani wa ZFF na TFF juu ya kile kilichojadiliwa katika mkutano huo kwa pamoja.

## Mashabiki Simba waletewa bosi wao

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuendelea kujitanua zaidi uongozi wa klabu ya Simba umethibitisha kuteuliwa mabosi wapya wawili ambao uteuzi wao ulianza tangu Oktoba Mosi, mwaka huu mmoja kati yao akiwa ni Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, Rispa Hatibu ameteuliwa kuwa msaidizi wa Mtendaji Mkuu wakati Hashim Mbaga akiteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki wa klabu hiyo.

"Klabu inapenda kuthibitisha kuteuliwa kwa Rispa Hatibu kuwa Msaidizi wa Mtendaji Mkuu na Hashim Mbaga kuwa Mkurugenzi wa Wanachama na Mashabiki.

"Tunawakaribisha klabuni tukiwa na matarajio makubwa ya kuiwezesha klabu kupiga hatua na kuhakikisha kuwa jukumu la mabadiliko linafikiwa," ilieleza taarifa hiyo.

**Wakati huo huo**, Bodi ya Wakurugenzi kupitia kwa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Senzo Mazingiza, imetangaza kuwapo kwa mkutano mkuu wa kawaida wa wanachama wa klabu hiyo utakaofanyika Desemba 12, mwaka huu katika Ukumbi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere jijini Dar es Salaam huku ikiahidi kusambaza ajenda za mkutano huo siku saba kabla ya kufanyika.

# NDAYIRAGIJE AMTAJA MIRAJI, KAGERE AKIFUNGUKA MAPRO

**Na Focus Nicus**

WAKATI baadhi ya wadau wa soka wakitaka idadi ya wachezaji wa kigeni ['mapro'] wanaozitumikia klabu za Ligi Kuu Bara kupunguzwa, Kocha Mkuu wa timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije ametoa maoni yake ambayo kwa timu kongwe Simba, Yanga na Azam inayochipukia zinaweza kuyapokea kwa mikono miwili.

**Simba, Yanga na Azam ndizo klabu hapa nchini zinazoongoza kwa kusajili wachezaji wengi wa kigeni kati ya 20 zinazoshiriki Ligi Kuu Bara.**

Kwa mujibu wa kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), klabu hairuhusiwi kusajili wachezaji wa kigeni zaidi ya 10, idadi ambayo bado baadhi ya wadau wa soka nchini wanaona ni wengi akiwamo Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe naye aliwahi kupaza sauti akitaka ipunguzwe ili kutoa nafasi zaidi kwa wazawa kucheza.

Lakini Ndayiragije akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, alisema kuna faida kubwa kwa wachezaji wazawa kupata fursa ya kucheza na nyota wa kigeni wanaosakata kabumbu hapa nchini.

Ndayiragije ambaye amepewa rasmi mikoba ya Emmanuel Amunike katika kikosi hicho cha Stars, alisema kwa kuwa wachezaji wengi wa Tanzania wanacheza soka hapa nchini, wanapata fursa ya kujifunza kutoka kwa wageni waliosajiliwa na klabu za Ligi Kuu.

"Mfano mzuri ni hivi karibuni nilimsikia Miraji Athumani alipofanyiwa mahojiano na redio moja, alisema anajifunza mengi kutoka kwa Middie Kagera na kufafanua kuwa Kagere amekuwa akimwelekeza mambo mengi," Ndayiragije alisema.

"Hivyo, kama tutazuia ama kupunguza wageni hii itatunyima pia nafasi ya wachezaji wetu kujifunza, kinachotakiwa ni wachezaji wanaosajiliwa kutoka nje wawe na uwezo wa juu kuliko wale wa ndani."

Alipoulizwa kama angetamani kuwa na mshambuliaji kama Kagere akiwa katika kikosi chake cha Stars, alisema "mimi ningependa kuona wachezaji wengi wanaenda kucheza soka nje ya nchi ili baadaye niwe na kina [Mbwana] Samatta wengi".

Kuhusu kutomjumuisha Kipa wa Simba, Aishi Manula katika kikosi chake, Ndayiragije alisema mlinda mlango huyo alimuomba kumpa muda wa kutosha kupumzika ili kujiweka fiti kutokana na majeraha ya muda mrefu aliyokuwa nayo.

"Baadhi ya mashabiki wanalalamika kwamba katika kikosi cha Taifa Stars ninaita wachezaji wengi wa Simba na Azam tu, hilo halina maana kwa kuwa ninachojua wote ni Watanzania na ninatazama kiwango zaidi."

**MILIKI...**



Mchezaji wa timu ya Cobra Veteran, Ibrahim Makemba (kushoto), akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wenzake wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya nje ya Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mwambusi alia utulivu Alliance ikiwashika*

**Na Focus Nicus**

BAADA ya kushindwa kuendeleza ushindi kama alivyoahidi walipoichapa Mbao FC mabao 2-1 Jumatatu wiki hii, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Juma Mwambusi amelilia kukosekana kwa utulivu katika kikosi chake kufuatia sare tasa waliyoipata dhidi ya Alliance FC juzi.

Ikiwa katika Uwanja wa CCM Kirumba Jumatatu, Mbeya City ilipata ushindi wa kwanza katika mechi saba na Mwambusi akasema kikosi chake kimeanza kuimarika na kumuelewa, jambo ambalo alisema sasa kazi imeanza.

Lakini katika Uwanja wa Nyamagana juzi, Mbeya City ilishindwa kutumia faida ya Alliance kubaki 10 dimbani baada ya wachezaji wao wawili kutolewa kwa kadi nyekundu na kujikuta wakilazimishwa sare tasa. Hata hivyo, baada ya mechi hiyo Mwambusi alimwambia mwandishi wetu kuwa wachezaji wake walikosa utulivu hivyo kushindwa kuifunga Alliance kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu.

"Wachezaji wangu walishindwa kuwa makini kumalizia nafasi tulizotengeneza kwani nafasi ya kushinda ilikuwa kwetu kwa sasa inabidi kuendelea kukiboresha hususan kwa makosa tuliyofanya kuelekea michezo mingine inayofuata," alisema.

Mchezo huo ni wa nane kwa Mbeya City msimu huu wakati huu ikiwa nafasi ya 16 na pointi nane baada ya kushuka dimbani mara nane ikishinda mechi moja, sare tano na kupoteza miwili.



## Messi arejea Argentina kuivaa Brazil, Uruguay

UKURASA 30

**'BIRTHDAY...!'**



Wachezaji wa Simba wakimpaka matope, Nahodha Msaidizi wa timu hiyo, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', ikiwa ni sehemu ya kumbukumbu ya sherehe yake ya kuzaliwa, mara baada ya kumaliza mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Mbeya City katika viwanja vya Gymkyana jijini Dar es Salaam jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Simba hawamtishi Mwambusi kesho

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kuvuna pointi nne katika jiji la Mwanza, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Juma Mwambusi, amesema kuwa kikosi chake kitaingia kuwakabili mabingwa watetezi, Simba, bila wasiwasi wala presha kama wanavyocheza katika mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mbeya City imewasili jijini Dar es Salaam jana ikitokea Mwanza ambapo ilipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mbao FC katika mchezo uliochezwa Jumatatu iliyopita na juzi ilitoka suluhu na Alliance FC, kwenye Uwanja wa Nyamagana.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwambusi, alisema timu yake ina wachezaji wengi wachanga na sasa inajengwa upya, kutokana na wachezaji wake waliokuwa na uzoefu wa ligi hiyo kuondoka klabuni hapo.

Mwambusi alisema kuwa ataingia kuivaa Simba kwa umakini, kutokana na kuifahamu vema timu hiyo, lakini akiamini kwamba kama wachezaji wake watatulia, wanaweza kupata matokeo mazuri katika mchezo huo unaotarajiwa kuchezwa kesho kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

Kocha huyo alisema kuwa kikosi chake kinahitaji kupata muda ili kiweze kupambana na ushindani ulioko katika ligi hiyo, lakini anaamini nafasi ya kubakia wanayo.

"Ligi ni ngumu sana, na mimi nina wachezaji wachanga, ndio ninakijenga kikosi, hata ile Mbeya City iliyokuwa tishio, nilitumia miaka miwili kuifikisha pale, haikutokea tu kibahati, iliandaliwa vema, naamini kikosi hiki pia kikiendelea kukaa pamoja, tutasumbua huko mbele," alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema "kila mechi mnayocheza mnajifunza kitu, tumeona tulipokosea Shinyanga, tunayafanyia kazi upungufu wetu ili turejee katika mbio zetu za kutetea ubingwa tunaoushikilia, kikubwa hakuna majeruhi yaliyoongezeka katika kikosi chetu, tukutane Jumapili," alisema meneja huyo.

# Zahera kaimaliza Yanga kisaikolojia

## ●●● Uongozi wafanya kazi kuwarudisha wachezaji mchezoni baada ya kocha huyo kuwapaisha Pyramids huku...

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa, Yanga, wakitarajia kushuka dimbani nchini Misri kesho kuivaa Pyramids FC, Kocha Mkuu wa klabu hiyo ya Mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam, Mwinyi Zahera, ana kazi kubwa ya kuwarejesha mchezoni wachezaji kisaikolojia baada ya kuwashusha, imeelezwa.

**Katika mechi hiyo ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, Yanga inahitaji ushindi wa kuanzia mabao 2-0 ili kuweza kusonga mbele baada ya kuruhusu kupigwa 2-1 kwenye mchezo wa awali uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba Jumapili iliyopita.**

Hata hivyo, kauli ya Zahera aliyoitoa baada ya mechi hiyo akieleza kuwa Yanga haiwezi kushindana na timu ya kiwango cha juu kama Pyramids na badala yake saizi yake ni timu za kutoka Afrika Mashariki kama Burundi na nyinginezo, inaelezwa kuwa mwiba mkali kisaikolojia kwa wachezaji.

Akizungumza na mwandishi wetu kwa sharti la kutotajwa jina gazetini, Mjumbe mmoja wa Kamati ya Utendaji, alisema kuwa kocha, Zahera hakupaswa kutoa kauli hiyo kwa kuwa yeye ndiye "Amiri Jeshi Mkuu" kwa upande wa timu anayeiongoza kwenda vitani.

"Unajua kiongozi kama kocha akishakata tamaa, unategemea wachezaji watafanya nini, inamaanisha wanaingia uwanjani wakijua hata tukifungwa hakuna tatizo kwa kuwa kocha mwenyewe anajua wapinzani wetu ni wa daraja la juu hatuna uwezo wa kupambana nao," alisema.

"Kocha alikuwa anatakiwa kutoa hamasa kwa wachezaji na kuwajenga kisaikolojia kuwa wao wameweza kutufunga hapa nyumbani kwa nini tushindwe kuwafunga kwao, kama ambavyo tulifanya kwa Township Rollers ya Botswana, lakini sasa itakuwa kazi kubwa kuwarejesha mchezoni kwa kuwaaminisha wanaweza kushinda.

"Tazama, anasema hadharani kuwa hakuna mchezaji hata mmoja katika kikosi chake ambaye anaweza kumlinganisha na wachezaji wa Pyramids, sasa ukishatoa kauli hiyo unawezaje kuwaaminisha kwamba wanaweza kushinda?" alihoji na kuongeza.

"Kwa ujumla tunaushukuru sana uongozi wa timu kuanzia Ofisa Habari ['Hassan Bumbuli'] na Ofisa Mhamasishaji, [Antonio] Nugaz ambao wanaendelea kutoa kauli za faraja kwa wachezaji na mashabiki kuwa kupindua meza inawezekana, lakini kocha ameshawapoteza wachezaji.

"Kadhalika, nimpongeze Makamu Mwenyekiti wetu, Fredrick Mwakalebela ambaye anafanya kazi kubwa kuwarejesha mchezoni wachezaji huko Misri, lakini pia akitupa matumaini ambayo angalau yanaweza kutuhamasisha kukaa kwenye TV kesho kuangalia mechi hiyo."

Mwakalebela ambaye alitangulia Misri kuiandalia mazingira mazuri timu hiyo kabla ya jana alfajiri kukipokea kikosi hicho, ameeleza kuwa timu hiyo ni ya kawaida na kwamba ana uhakika watapambana kupata matokeo.

Alisema wana matumaini ya ushindi baada ya kugundua kuwa huko Misri Pyramds inazungumziwa kama timu ya kawaida suala ambalo linawapa nguvu.

"Hapa Misri Pyramids wanaisema ni timu ya kawaida kabisa, hivyo inatupa nguvu kuelekea mechi ya marudiano, ninaimani tutafanya vizuri," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >